ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo laTumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji Kwanza	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.

21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi zaWanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani

46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 20 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho)alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kuweka Hati mezani kuhusu Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyokubaliana jana kwamba leo moja kwa moja baada ya uwasilishwaji wa Hati Mezani, kazi ambayo imeshafanyika tunakwenda moja kwa moja kwenye majumuisho ya Hotuba ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Kwa mnasaba huo basi sasa naomba nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyenijaalia kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu nikiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyetupa jukumu hili kubwa la kuhitimisha wizara hii. Pia nimshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa miongozo yao katika kutekeleza kazi yetu. Nimshukuru sana kwa aina ya pekee Mhe. Waziri wangu Abdillahi Jihad Hassan kwa ushirikiano mkubwa sana anaonipa wakati nikitekeleza kazi zangu. (*Makofi*).

Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru sana Katibu Mkuu wa wizara hii, Dkt. Kassim Gharib Juma pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano wote wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*).

Nyengine niwashukuru wanafamilia wangu wote, akiwemo mama yangu mzazi kwa kunivumilia wakati nikitekeleza majukumu yangu, lakini la mwisho kwa umuhimu mkubwa sana niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpendae kwa kunipa heshima kubwa sana kwa kusimama katika Baraza lako hili Tukufu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, na mimi sasa niingie moja kwa moja kwenye hoja, kabla sijasahau ninataka niseme tu naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Spika, na mimi nitajaribu kujibu hoja za baadhi ya Wajumbe na Mhe. Waziri wangu atakuja kuhitimisha ili basi tuone muskabali mzuri, lakini kabla sijaanza hoja hii, ningewaomba Waheshimiwa wote Wawakilishi ili watuunge mkono tupitishe bajeti yetu, kama munavyojua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni bajeti ya wananchi na bajeti halisia kabisa.

Mhe. Spika, nianze kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar mvuvi mwenzetu mwenye jina la wizara yetu kutoka Kojani kama ifuatavyo. Yeye alikuwa na hoja kadhaa, alisema aliahidiwa vijana wawili kwenda kusoma katika Chuo cha Uvuvi. Ninataka nimjibu tu moja kwa moja kuwa wizara imetenga bajeti na tayari tutamchukua kijana mmoja kutoka Kojani ili kumpeleka Mbegani kusoma uvuvi. Mhe. Spika, mara tu baada ya bajeti hii atuone

wizarani ili basi atambue jina lake moja ili tuhakikishe Kojani nayo imepata manufaa katika wizara hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, hoja ya pili ilikuwa anataka kujua kuwa wanajamii na wafugaji wa mazao ya baharini waliopelekwa kujifunza China.

Nataka kusema tu Mhe. Spika, wale vijana waliopelekwa China wamepata manufaa makubwa sana. Baadhi yao wamekuwa wakifanya uzuri sana katika ufugaji wa mazao ya baharini, lakini kubwa zaidi tulikuwa tukifanya *study tours* kubadilishana uzoefu ili waweze sehemu mbali mbali kuwafunza wenziwao na kupata tija zaidi katika mazao haya ya baharini hasa katika ufugaji wa samaki, kaa, pamoja na chaza.

Mhe. Spika, hoja ya tatu ilikuwa ni Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya 2010. Alikuwa akieleza kuwa haina nia thabiti ya kuwaendeleza wavuvi hali ambayo inawakandamiza. Nataka nimjibu tu Mhe. Mwakilishi kuwa sheria hii ina nia thabiti ya kuendeleza uvuvi na itakapotekelezwa, itakuwa ni mkombozi wa sekta ya uvuvi hapa Zanzibar.

Sheria hii itatayarishwa na kupatiwa maoni ya wadau mbali mbali kuanzia katika Shehia hadi katika ngazi ya Serikali Kuu. Mhe. Spika, inaonekana kwamba matumizi ya vioo, gesi na viatu vya shughuli za uvuvi yanachangia kuharibu mazingira ya bahari. Hata hivyo, wizara imepokea ushauri wa kuipitia sheria hii ya uvuvi ili kurekebisha mapungufu yote ambayo yapo.

Lakini ninataka kusema Mhe. Spika, kuwa vioo bado vimeonesha dhamira kubwa ya kuwa vinaharibu ile miundombinu ya bahari. Kwa hivyo, bado tutaipitia sheria hii na kama wavuvi wenyewe kwa sababu tutaileta tangu kuanzia katika ngazi ya Shehia, lakini kama tutaiona ina manufaa kwa sote tutaitelekeza, lakini sote tukiona wadau wote wameikataa, tutafuata wadau jinsi gani wanavyotaka.

Tatizo kubwa ambalo tulilokuwa tukiliona hapa, tatizo hili tusije tukaifanya bahari yetu kuwa jangwa, hata wale samaki kidogo kidogo tunaowapata isije kuwa hatupati kabisa. Hili ndio maana tutafanya hivi, lakini tutarudi katika ngazi ya Shehia, tutawajumuisha watu mbali mbali ili kuona manufaa yamepatikana.

Mhe. Spika, nichukue fursa hiii kumjibu ndugu yangu Mhe. Ali Salum Haji. Yeye alikuwa anataka kujua tu mapato kwa kilo ya samaki ya maji ya ndani au bahari kuu yanatoka vipi takwimu zake. Sasa naomba kumjibu. Takwimu za samaki zinaonesha katika ukurasa wa 5 ni za maji ya ndani zinazohusisha wavuvi wetu wadogo wadogo. Zile takwimu kubwa hatuwezi kuzipanga kwa sababu ni meli nyingi tu ambazo zinachukua vibali, ni meli za nje zinaweza kuwa katika bahari kuu, hatuchukui takwimu kama hizi, ambazo tunachukua ni takwimu za hapa.

Baadae takwimu hizo zinazotokana katika madiko, hizo takwimu tunazozichukua tunachukua tuna watu wetu maafisa wetu wa uvuvi katika madiko mbali mbali. Ndio wanaochukua takwimu hizo, halafu wanatuletea na sisi tuna-*compile* kwa pamoja na tunaweka kwenye vitabu na tunazo za kila mwezi, tunao utaratibu wa kuweka takwimu hizo.

Hoja nyengine alizungumza hoja za nyumba za wizara, nyengine zinafanywa mambo yaliyokuwa sio katika sehemu ya Maruhubi. Ninataka kumwambia kuhusu zile nyumba za Maruhubi, ushauri wake tunauchukua na tutaufanyia kazi basi tuone nyumba zile tunazifanya nini.

Suala alilolizungumza kama wizara haitambui kuwa nyumba zile zinafanywa vyenginevyo. Tunajua kuwa nyumba zile zipo na zipo chakavu sana. Kwa kipindi kirefu sana. Sasa tutazifanyia kazi ili tuone ushauri wake aliotupa tumeutekeleza kwa busara zaidi.

Nyumba nyengine alizozingumza ni nyumba za Mazizini. Nyumba za Mazizini tayari moja imesharejeshwa. Zile nyumba zilikuwa nne na mbili tunazo hivi sasa, mbili bado zipo. Tangu kuwa kwenye Kamati hii ya Mifugo na Utalii ilikuwa ikipigia kelele sana kuhusu nyumba hizi, lakini nyumba mbili tayari tunazo na nyumba mbili tulipoona bado tunashindwa, tulipeleka barua kwa Makamu wa Pili wa Rais ili naye awaandikie. Na kwa ushahidi amewaandikia na sijajua tumefikia wapi, lakini *inshaallah* tutalifuatilia tuweze kujua kuwa nyumba zile zimerejeshwa.

Nyumba ambayo imerejeshwa ni nyumba ya Mhe. Abdisalam Issa Khatib. Ile sasa tunayo na tunaifanyia marekebisho ili kuweza kuwapa wafanyakazi wetu wakae kwenye nyumba ile. Nyumba ambayo haijarejeshwa ni nyumba ya Mhe. Waride Bakari Jabu na nyumba ya Mhe. Burhan Saadat Haji, lakini bado tunaendelea kuzifuatilia ili tuone nyumba hizi tumerejeshewa mikononi na kuweza kuwapatia watu wetu.

Hoja nyengine ilikuwa amesema kujitokeza kwa migogoro kwa wavuvi wa baina ya Tumbatu na Kivunge. Kiini cha mgogoro ni nini na hatua zilizochukuliwa au zilizotatuliwa kuhusu mgogoro huo.

Mhe. Spika, jawabu yake ni kwamba kiini cha mgogoro huo baina ya wavuvi wa Tumbatu na Kivunge, huo ni uvuvi haramu na unafanywa katika eneo hilo lililozunguka bahari ya Tumbatu. Uvuvi huo ulifanywa na watu wa Kivunge na kuleta athari kubwa katika maeneo yale ya Tumbatu.

Sasa hili lina mnasaba sana na lile alilolisema Mhe. Hassana Hamad Omar kuwa kwa nini tuwe tunaweka hifadhi, wale wavuvi watapata wapi sehemu ya kuvua. Sasa kuweka hifadhi Mhe. Spika, ninataka niingilie hili suala niseme tu, kuwa tunaweka hifadhi ili uvuvi haramu usiweze kufanyika, lakini hata hivyo, tunajitahidi kutoa elimu na ndio ukaona hatukukamata watu wengi pamoja na doria tunazozifanya, kwa sababu wavuvi sasa hivi wameanza kuelewa nia thabiti ya kuondokana na uvuvi haramu. Tunaweza tukasababisha jangwa kubwa katika bahari ili tuwe hatuna samaki hata kidogo.

Lakini niombe tu Mhe. Spika, nichukue hii kuwaomba ndugu zangu wote wavuvi wenzangu ili basi tujitahidi tusifanye uvuvi huu haramu, lakini hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kukutana na wahusika wa Tumbatu na Kivunge mara mbili kwa lengo la kufuatilia ufumbuzi wa suala hilo.

Aidha, Mhe. Spika, Rais aliunda Kamati maalum chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kutatua mgogoro huo. Kamati hii ilifanya mikutano na wavuvi maeneo yote husika pamoja na kamati zao. Hivi sasa mzozo huo umeshatatuliwa na shughuli za uvuvi zinaendelea kama kawaida.

Aidha, wizara yangu Mhe. Spika, ikishirikiana na KMKM inafanya doria mara kwa mara ili kudhibiti vitendo hivyo viovu.

Mhe. Spika, hoja nambari tatu ilichangiwa sana ilikuwa ni bei ndogo ya mwani. Hii ilitoa changamoto kubwa sana. Hoja hii ilichangiwa na Waheshimiwa saba, nao ni:-

1. Mhe. Kazija Khamis Kona
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
3. Mhe. Mussa Ali Hassan
4. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
5. Mhe. Salum Abdalla Hamad
6. Mhe. Salma Mussa Bilali; na
7. Mhe. Saleh Nassor Juma

Waheshimiwa hawa waliichangia sana.

Mhe. Spika, lakini jawabu tu ni kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeleta wataalamu kutoka *UNIDO* na kufanya utafiti na uzalishaji wa kiwanda cha usarifu wa mwani na kupata mazao yatakayouzwa Zanzibar. Ili kupata soko la ndani, bidhaa hizo ni pamoja na matumizi ya mwani, kukuza mimea kama vile mbolea. Hivyo matokeo ya mwani kuhusu utafiti huo utasaidia kupatikana ufumbuzi katika bei ya mwani.

Ninadhani tukianza tu matumizi yetu wenyewe bei hii itakuwa kubwa, lakini wengi kama Mhe. Mussa Ali Hassan alisema Mhe. Spika, kuwa apewe nafasi sasa ya kwenda nje. Sisi hatuna pingamizi hata kidogo, kama Mheshimiwa utatafuta vyanzo vyako tutakuelekeza, kuna nchi 11 sasa ambazo zinachukua mwani ili uende utusaidie.

Najua wewe ni mtaalamu zaidi wa kwenda kutusaidia na sisi tunataka tuchukue ushauri wako, tukae na wewe karibu ili utupe tuone basi jinsi gani tutaweza kutekeleza hili soko la mwani. (*Makofi*).

Tutakwita ofisini kwa sababu wewe ni Mjumbe wa Kamati yetu, tutakaa na wewe pamoja, tushirikiane na tuone basi njia bora ambazo tunaweza kuwapatia wakulima wetu wa mwani. Sisi tunajua na tuna hakika sana kuwa bei ya mwani ni ndogo, lakini kutokana na soko lilivyo hivi sasa, wizara haina uwezo wa kuzidisha bei, lakini wale ambao wananunua, tunajaribu kwenda nao kila pahala na kama nilivyokwambia tu vitu vingi ambavyo tutarekebisha.

Hata hivyo, wizara yangu pia kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (*FAO*) imeanza kazi ya ufuatiliaji wa kuwezesha jamii katika mambo ya masoko ya mwani na mazao mengine ya baharini. hivyo, tayari imeanzishwa njia nyengine ya kutumia mawe na mipira ya *rubber bands*. Aidha, wananchi wanahamasishwa kupanda miti ili kupata vijiti kwa urahisi zaidi.

Mhe. Spika, nakuja kwenye hoja namba nne ilikuwa ni mwelekeo wa kesi ya vibali feki. Mhe. Spika, ninataka niseme tu kuwa hii kesi imekuwa ni ya muda mrefu sana. Nataka nikiri kuwa kesi hii imechukua zaidi ya mwaka mmoja hivi sasa tangu ilivyoibuliwa katika mwaka uliopita. Kesi hii ya kughushi leseni imepelekwa katika vyombo husika vya serikali ambavyo hatua za kisheria zinataka zitekelezwe.

Wizara imeanza kufuatilia mwenendo wa kesi hiyo na kwa kushirikiana na kutoa ushahidi mkubwa sana Polisi. Hata mimi mwenyewe nilikuwa nikienda sana kumuona Mkuu wa Upelelezi wa Kesi za Jinai kuweza kunipa basi matokeo ya kesi hii, lakini mara ya mwisho ilikuwa Machi ambayo tulipata barua yenye Nam. *CID/HQ/2/C5/4/4/ACFS/26* ambayo iliyokuwa ikituelekeza kuwa madai hayo sasa yamepelekwa kwa *DPP* ambayo yanashauriwa kuweza kufungua kesi Mahakamani.

Ninataka kusema kwamba Mhe. Spika, watu walikaa nao nje ya Mahakama na mimi ndiye niliokaa nao mwanzo wa nje ya kesi kabla hatujaipeleka kesi hii Polisi ili tuweze kutatua kabla ya hapo, lakini tulishindwa. Mimi nilishindwa kwa sababu leseni zilizokuwa zimeghushiwa ni kesi 10, lakini walisema wao ni leseni 8 wamelipa na wanataka kulipa leseni 2.

Sasa leseni 2 kati ya 10 ni kizungumkuti Mhe. Spika, hatuwezi kukubali, tulishindwa kabisa kuweza kukaa na ku-*compromise* tukaweza kupatana na kuweza kuiondoa hii kesi, lakini kama itatokea mazungumzo, kama watakubali kulipa hizi zilizokuwepo, basi kesi hii hatutoipeleka Mahakamani ili kuona serikali inapata mapato ya uhakika na tuone basi mambo ya kushtakiana wananchi wa hapa Zanzibar hatuwezi kushtakiana, lakini waweze kulipa tu hivi ili tuone basi kitu gani kinafanyika.

Tumekaa nao nje, walikataa kulipa boti mbili, wizara imesema hakuna, hatuwezi kukubali kuweza kufanya hivyo, lakini ninataka kusema bado wizara yangu inafuatilia kwa karibu na nimshukuru sana Mkurugenzi wangu Zahor Al-Harous kwa kufuatilia kwa umakini zaidi, lakini kila anapofuatilia hunipa taarifa na mimi wakati mwengine huwa ninafuatilia mwenyewe.

Hata nilimfuatilia *DPP* kumuuliza, aliniambia kweli jalada hili amelipata na liko kwake na linafanyiwa kazi. Kwa hivyo, ndugu yangu Mhe. Ali Salum Haji nataka ujue kwamba kazi hii ambayo umetupa tunaifuatilia kwa karibu zaidi pamoja na watendaji wangu wote.

Hoja nyengine ilikuwa ni hatua zipi zimechukuliwa katika ujenzi wa chinjio la Kisakasaka. Nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi wameonesha nia hiyo ya kuuliza soko hili miundombinu yake, akiwemo Mhe. Wanu Hafidh Ameir; Mwakilishi wa vijana kupitia Mkoa wa Kusini Unguja.

Mhe. Spika, nataka niseme tu chinjio limefanyiwa matengenezo makubwa ya mradi wa *ASPL* ikiwemo sakafu, kuziba nyufa, kupaka rangi, ujenzi wa chumba cha kusafisha matumbo, ofisi, vyoo pamoja na mambo yote na kutia umeme. Wizara inafahamu fika kwamba chinjio hilo ni dogo na hivi sasa tumefanya michoro mingi mikubwa ambayo tukipata wafadhili basi tunaweza kujenga soko kubwa sana.

Vile vile ndugu yangu Ali Salum Haji alielezea kifungu namba 220401 ununuzi wa petroli kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ikiidhinishwa shilingi 660,000 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imeongezeka hadi kufikia milioni 3,331,000. Jawabu ni kwamba awali *WHO* ilikuwa ikifadhili ununuzi wa mafuta kwa ajili ya mradi wa kichaa cha mbwa Pemba, mradi huu unatarajiwa kumaliza mwaka huu, hivyo idara imeongeza ununuzi wa mafuta kwa ajili ya kuendesha shughuli hizo za mradi na uchanjaji na ufuatiliaji wa ugonjwa huo, ndio maana utaona fungu hilo limeongezeka kwa hivi sasa; mwanzotulikuwa na wafadhili lakini sasa wameshaondoka.

Pia Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe alizungumzia kifungu namba 221102 mafunzo ya ndani kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hakikupangiwa, lakini kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015 kimeombewa shilingi 14,820,000. Jawabu ni kwamba mwaka jana kifungu hicho hakikutiwa fedha kutokana na kuwa hakukufanyika mafunzo, lakini mwaka huu tuna wafanyakazi wawili tunawalipia mafunzo *SUA* na tumesisitiza sana kupata wataalamu, hivyo tunakuwa tumejipanga zaidi kuweza kupata wataalamu walio bora na wenye ufanisi, sasa hivi ndio tumeanza kusomesha huko Tunguu.

Vile vile kifungu chengine kilikuwa 221199 cha vifaa vya mafunzo; *training materials* hakijawekewa fedha kutokana na kwamba gharama zote za mafunzo pamoja na *training materials*, zimetiwa katika kifungu namba 221102.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni hoja namba saba. Je wizara ina mpango gani wa kuziendeleza nyumba zilizopo Mtoni. Hoja hii tayari Mheshimiwa nimeshaitolea ufafanuzi. Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mwakilishi wa Viti Maluum Kaskazini Pemba, alizungumza mambo ya chumvi inataka kuzalishwa baharini, lakini Wizara ya Mifugo na Uvuvi haishughuliki na suala hilo.

Hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad; Mwakilishi wa Jimbo la Chambani, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Rufai Said Rufai wa Jimbo kubwa la Tumbe. Jawabu ni kwamba, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haishughuliki na uzalishaji wa chumvi, kama isivyoshughulika na uzalishaji wa mafuta baharini, gesi na nishati ya mawimbi. Isipokuwa inashughulika na mazao ya baharini, kwa vile viumbe vyenye uhai kama vile samaki, pweza, chaza, mwani na majongoo ya baharini. Nataka kusema tu kwamba chumvi ni maliasili na wala haihusiani kabisa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni mpango wa kuwaendeleza vijana wa Micheweni kwa kuwapatia mbuzi wa maziwa. Mhe. Spika, wafugaji wa mbuzi wa Micheweni wameendelezwa kwa kupatiwa mbuzi wa maziwa 24 kupitia vikundi vya vijana katika Shehia za Majenzi na Wingwi Mapofu. Pia taaluma za ufugaji bora zimetolewa kwa kupitia Maofisa wa ugani wa eneo la Micheweni.

Mhe. Spika, kinachoonekana hapa ni kuwa Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako hili tukufu, huwa wanasema maneno ya nadharia zaidi kuliko vitendo, hawaendi katika zile sehemu zao. Mimi nilitembelea kule, lakini niliwapata Waheshimiwa Wajumbe kadhaa ambao tulitembelea kule na wewe utakuwa shahidi nilileta karatasi ya kuweza kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe nitembee katika maeneo yao. Kwa hivyo, hili linatuvunja moyo sana kwa kuuliza mambo ambapo mambo makubwa yako kule kwenye Shehia zao na katika Majimbo yao.

Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwaomba sana Wajumbe wawepo na wasiulize mambo kinadharia. Mhe. Spika, utakuta hata maswali ambayo yanaulizwa, tayari tunatoa tumeshawapatia ufafanuzi na tunakwenda kule ili kuzungumza na wale wahusika wenyewe wote.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni hoja ya vikundi vingapi vidogo vidogo vimesaidiwa kwa upande wa Tumbe; Pemba. Utakumbuka hata jana asubuhi nilisema nitalitoa kwa maandishi swali hili, lakini naomba kwanza niweze kulijibu hili swali la Mhe. Bikame Yussuf kama ifuatavyo;

Vikundi viwili vya mwani vya Tumbe Mashariki na Tumbe Magharibi, vimesaidiwa vifaa vya mwani, jengo la ofisi na ghala la kuhifadhia mwani, pia boti ya kubebea mwani na mashine yake.

Mhe. Spika, ya pili Shehia ya Tumbe imesaidiwa ujenzi wa ofisi ya usimamizi wa magofu ya Chwaka na ukarabati wake. Jengine wanajamii walipatiwa taaluma pamoja na kufanya utafiti wa kilimo cha mwani wa *cottonii* katika kina kirefu cha maji, tayari baadhi ya wakulima wameshaanza kulima huo mwani wenye tija wa *cottonii*.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ilikuwa ni hoja namba nne Mjumbe alitaka kujua matokeo ya upembuzi yakinifu katika Kiwanda cha Maziwa. Mhe. Spika, niseme tu matokeo ya upembuzi yakinifu wa Kiwanda cha Maziwa Fumba yameonesha kwamba maziwa kutoka kwa wafugaji wadogo wadogo yatatoa mchango wa kuendesha kiwanda hicho. Kwa kuwa mahitaji ya kiwanda hicho ni makubwa kuliko uzalishaji wa maziwa hivi sasa, kuwepo kwa kiwanda hiki kutashajihisha wafugaji kuongeza uzalishaji wa maziwa yao kwa bidii kubwa sana.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni takwimu za mifugo na mazao zinazoletwa hapa Zanzibar. Hoja hii imechangiwa na Mhe. Fatma Mbarouk Said; Mwakilishi wa Jimbo la Amani, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Salma Mohammed Ali na Mhe. Asha Abdu Haji alichangia kwa maandishi.

Jawabu ni kwamba uzalishaji wa maziwa na mayai uliotolewa katika kitabu cha bajeti ni wa ndani, na umetokana na wafugaji wetu wanaofuga mifugo hiyo ya kisasa na ya kiasili. Uzalishaji wa nyama wa ng'ombe, umechanganya takwimu za nyama ya ng'ombe waliofugwa hapa nchini na wale wanaotoka Tanzania Bara, wala hawakusema kwamba wote tu wanatoka Bara, lakini takwimu hizi zilichanganya kwa wote. Tunaweka takwimu hizo kwa vile uzalishaji wa ndani wa nyama hiyo inazalishwa hapa nchini, na sio wa nyama inayouzwa kutoka nje ya nchi.

Aidha, zipo takwimu za mazao ya mifugo zinazoingia kutoka nje ya nchi ya Zanzibar kama ifuatavyo. Maziwa kwa mwaka 2012 ni tani 2.2, mwaka 2013 ni tani 2.6, mayai kwa mwaka 2012 ni tani 1.05, mwaka 2013 ni tani 1.339, nyama ya ng'ombe mwaka 2012 ni tani 34, mwaka 2013 ni tani 68.

Takwimu zilizokusanywa ni takwimu za Unguja na Pemba kwa kila wilaya na shehia. Idara imekata maeneo ambayo yana shehia mbili hadi nne na kila eneo litakuwa na bwawa la mifugo ambalo linachukua takwimu za uzalishaji na zilizopelekwa wilayani na hatimaye Makao Makuu ya Idara, ambako huhakikiwa na kuwekwa kuwa ni kumbukumbu rasmi.

Mhe. Spika, kwanza kabisa tunapokea pongezi kubwa sana zilizotoka kwa Mhe. Asha Abdu Haji, ambaye alichangia kwa maandishi kuhusu huduma zetu ambazo tunazitoa kule Jambiani. Mhe. Spika, niende kwenye hoja ya Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Naomba anisikilize vizuri, kwa sababu mmoja katika wale ambao nilitembea nao majimboni mwao, basi yeye alikuwa ni mmoja na nimpongeze sana, kwa kuwa ndiye Mheshimiwa wa mwanzo kujitokeza ili kutembea naye kule kwa wafugaji wake wa samaki, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Yeye hoja yake alisema kuwa kinamama wengi wanaoshughulika na shughuli za mazao ya baharini, wana kikundi cha wafugaji wa chaza cha Makombeni.

Jawabu nasema kwamba Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, kikundi hiki kimekuwa kama ambacho tumekiajiri. Hili suala nadhani, sina hakika na ninayoyasema uliuliza kinadharia hukwenda kuwauliza wale wenyewe, sasa nataka nikujibu kuwa kikundi cha wafugaji wa chaza cha Makombeni ni kikundi muhimu sana kwa wizara, na wizara inakitambua na imekisaidia sana kikundi hiki kwa kufanya mambo yafuatayo.

Kwanza kuwajengea ofisi yao, lakini pili kuwapatia boti, mashine na vifaa vyengine vya kufugia chaza. Pia wamepatiwa mashine ya kusarifu maganda ya chaza, mafunzo ya usarifu na wizara imeshirikiana na *FAO* katika kupata ufumbuzi wa soko lile ambalo wanafanya. Nadhani pale wanatoa chaza za lulu. Napenda kukuhakikishia kwamba hata mimi mwenyewe nilikwenda kuwakabidhi mashine hii, na nimepata zawadi ambayo nimeitundika nyumbani ya mkoba mzuri sana kutoka Makombeni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mwakilishi wa kudumu wa Jimbo la Wete na yeye alikuwa na hoja kadhaa. Soko la Tumbe alisema limefikia wapi? Hoja hii imechangiwa na Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Fatma Mbarouk Said ambao wote walikuwa wanataka kujua tu soko hili limefikia wapi na limejengwa kwa kiasi gani.

Mhe. Spika, nataka kusema jawabu ni kwamba soko limejengwa na Kampuni ya Ujenzi ya Ngogo, kwa gharama ya shilingi 712,500,000 kwa fedha za mradi wa *MACEMP*, kwa kuwawezesha wavuvi wa Kaskazini Pemba kuuza samaki wao katika hali ya ubora na unadhifu.

Ujenzi umeanza mwaka 2012 na kumalizika mwaka 2013, lakini hadi leo bado soko hilo halijakabidhiwa. Soko hili lina sehemu ya kuwekea mtambo wa barafu ambao umeshanunuliwa na hivi sasa umehifadhiwa katika ghala zetu za jengo letu la Minai liliopo Kizimkazi, bado kwa kuupeleka Pemba. Soko bado halijakabidhiwa kwa wizara na Mkandarasi anaendelea kurekebisha kasoro ndogo ndogo za pale.

Mhe. Spika, labda niseme tu kuwa nimetembea muda mwingi na tumezungumza na ndugu yetu huyu wa Ngogo, ili kurudi na kuweza kufanya marekebisho ambayo wizara imeona na yeye amekubali, na sasa matengenezo makubwa yale yamefanywa.

Mimi mwenyewe hata wiki mbili nyuma zilizopita, nilikwenda kulitembelea na kuona jinsi gani ukarabati ule unavyoendelea. Ukarabati ule nataka niseme Mhe. Spika, mbele ya Baraza lako Tukufu, kuwa ukarabati ule unaendelea vizuri sana, maana yake nilipanda mpaka juu mimi mwenyewe kuangalia ile *floor* ambayo ilikuwa inavuja, hivi sasa mambo mengi yamekaa sawa. Kwa hivyo, nataka niwaahidi Waheshimiwa wa Tumbe, Mhe. Bikame Yussuf Hamad na Mhe. Rufai Said Rufai kuwa soko lile hivi karibuni litamalizika.

Mhe. Spika, lakini niseme kuhusu hoja ile ya wananchi kudai pesa za pale. Mhe. Spika, niseme jambo hili ni gumu sana kwa wizara, tumejaribu kulifuatilia mara mbili au tatu, lakini kitu kilichojitokeza ni mikataba ilikuwa ni yao wenyewe, na hakuna mkataba wowote ambao ulifanyika pale, sasa tutalipa kwa njia gani.

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi, bado waende kwa Mkandarasi wajadiliane naye, kama atakuwa amekataa basi wapeleke kwenye vyombo vya sheria na sisi tutakuwa ni mashahidi wa pale, lakini kwa

kusema tu sisi moja kwa moja, hatuwezi kuingilia kati. Kwa sababu tangu wanakopeshana hawajatushirikisha katika mpango ule.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni hoja ya kuwapatia maposho wafanyakazi waliokwenda safari za nje. Waheshimiwa Wajumbe walitaka kujua wizara ina msimamo gani. Maposho ni haki ya kila mfanyakazi anayesafiri wizarani kuelekea katika safari ya nje, lakini hali ya kifedha inaporuhusu. Wakati mwengine tunapowaambia waende, hali ya fedha hairuhusu wizarani lakini safari ile ipo. Kwa hivyo, tunawaambia tu waende, inategemea tu pale mtu anao wasaa wa kwenda na kufanya hivyo. Tukiweza kuizuia ile safari basi tutakuwa tumepoteza jambo jengine zaidi.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kaka yangu wa Jimbo la Kitope jimbo kubwa hili yeye alitupongeza na tunamshukuru sana, lakini vile vile nimpongeze sana na yeye kuwa ni mdau wetu mkubwa sana. Mhe. Spika, kwa taarifa tu ya Baraza lako kuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ana bwawa kubwa la samaki, na sasa tuko karibu na yeye ili kuweza kulimaliza, tunampongeza sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis; Mwakilishi wa Jimbo la Konde, yeye alikuwa na hoja kama ifuatavyo. Je, wizara ina mpango gani wa kuwaajiri wataalamu katika fani ya mifugo? Jawabu ni kwamba Mhe. Spika, naomba kukuarifu kuwa mashirikiano ya Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma na wizara yetu, imekubaliwa kuwaajiri jumla ya wafanyakazi 96 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Uajiri huo utapunguza tatizo letu la upungufu wa wataalamu katika nyanja mbali mbali.

Mhe. Spika, wizara yetu kama unavyojua ni wizara ambayo iliundwa kwa kumegwa kutoka katika wizara nyengine, tulikuwa tuna upungufu wetu mkubwa, lakini tunashukuru sana serikali kwa kutukubalia kuwaajiri watu 99, wataalamu wakiwemo hao. Wataalamu hawa tunataka kuwachukua katika Chuo chetu cha Kilimo au kwengineko ikiwa hali itaruhusu.

Hoja nyengine ilikuwa wizara inafanya nini ili kuwasaidia wafugaji. Wizara ina malengo ya kuwasaidia wafugaji taaluma zote za ufugaji, ikiwemo usarifu wa mazao ya mifugo na ujasiriamali. Pia wizara inaunganishwa na wafugaji wa taasisi za mikopo nafuu ili kupata mitaji ya biashara kuendeleza ile azma ya ufugaji wao.

Mhe. Spika, nimjibu dada yangu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa wa Viti Maalum, hoja yake aliyouliza kwamba vipi wataalamu wazoefu wameshirikishwa katika utekelezaji wa wizara kupatiwa maslahi yao. Hivi karibuni serikali iliwapatia ongezeko la mishahara wafanyakazi wazoefu, hasa wale waliokwishafanya kazi kwa muda wa miaka 15 na hasa wale wenye kiwango cha chini cha elimu, na hivyo kuwa na mishahara mizuri, kwa vile *scheme of service* yetu inatoa kipaumbele kwa wale wenye elimu ya juu zaidi.

Hii inaonesha kuwa serikali haikuwadharau, lakini tulikuwa tunaangalia ni njia gani za kuwasaidia wale waliokaa na elimu za muda mrefu na sasa serikali imewaongezea kipato hicho. Kwa hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi muiamini serikali kujua kitu ambacho tunakifanya.

Mhe. Spika, nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub...

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri jipangeni vizuri pamoja na waziri wako, ili hatimaye na yeye apate muda mzuri wa kukamilisha majumuisho, na hatimaye tuweze kumalizia kazi hiyo kabla ya kwenda Ijumaa. Muda ambao umeshachukua sasa ni karibu dakika 40, kwa hiyo punguza kidogo ili na Mhe. Waziri aje kumalizia kazi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumalizia suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliloleta kwa maandishi, alisema kuhusu boti ya wananchi wa kijiji chake cha Muyuni, kama nilivyomjibu kwa kupitia maelezo ya jana ya swali lake, kuwa tunajua habari ya boti hii, lakini hali itakaporuhusu basi yeye atakuwa ni wa mwanzo kuweza kumpa boti hiyo.

Kuhusu ni lini wananchi wa Jambiani na wao watafaidika na boti ya uvuvi. Nataka kumwambia tu kuwa hali itakaporuhusu, basi tutakaa pamoja ili kuweza kumsaidia kupata njia hiyo. Suala jengine Mhe. Waziri wangu atakuja kueleza jinsi hali yetu itakavyoruhusu, lakini namwambia asitie wasi wasi.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nataka kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wote, watuunge mkono katika bajeti hii ndogo, ili kuweza kutekeleza majukumu yetu kwa mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa mchango wako huo, ikiwa ni sehemu ya majumuisho ya hoja hii. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, karibu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na kutupa nguvu za kuendeleza dhamana zetu kwa nchi yetu.

Pili nikushukuru wewe mwenyewe binafsi na Wajumbe wako wote wa Baraza hili Tukufu, kwa michango yao yenye lengo la kunisaidia mimi binafsi pamoja na watendaji wa wizara hii katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi ili iwaletee maendeleo Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, Makamu Mwenyekiti wake Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Amina Iddi Mabrouk ambaye alisimama kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati kwa ajili ya kuwasilisha maoni ya kamati na kutoa maelezo yanayohusu wizara yangu pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii. *(Makofi)*

Kwa kweli kutokana na nasaha, ushauri pamoja na maelezo waliyoyatoa katika kunielekeza wizara yangu, ili kufikia malengo yetu ya kuwahudumia ipasavyo wafugaji, wavuvi na wakulima wa mwani pamoja na wadau wengine wa Sekta za Uvuvi na Ufugaji.

Mhe. Spika, naomba nilihakikishie Baraza hili kwamba michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tunaithamini na tutaitekeleza kwa kadri ya uwezo wetu.

Maoni yaliyotolewa na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi ni pamoja na wizara kuongeza fungu, ili iweze kuwahudumia vyema na ipasavyo wavuvi na wafugaji, kwa ajili ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana. Pia wizara iimarishe vyanzo vyake vya mapato, ili makusanyo yaongezeke na hatimaye yaweze kusaidia uendeshaji wa taasisi za wizara na taifa kwa jumla.

Vile vile kuajiri wataalamu wengi zaidi katika fani zilizo na upungufu ikiwemo wataalamu katika nyanja za utafiti, takwimu na elimu ya kuendesha uvuvi pamoja na madaktari wa mifugo.

Wizara ifanye juhudi za makusudi, ili kuongeza fursa zaidi na mafunzo kwa wafugaji na wavuvi, pia kufurahishwa na azma ya wizara ya kuongeza fursa za ajira kwa vijana katika mradi wa kuendeleza wafugaji wadogo wadogo.

Wafugaji waliopata mafunzo wanajitahidi kuendeleza ufugaji. Hata hivyo, wafugaji wa kuku wanapata vifaranga vingi, lakini vifaranga hivyo hushambuliwa na maradhi ya ndui na mahepe.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, samahani tunao utamaduni wa kuwatambua waliokusaidia kuchangia hoja hii, leo unafanya vipi au utafanya mwisho.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nitawatambua.

Kwa muhtasari ili tuokoe muda, niseme kwamba hotuba ya Wizara yangu ilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 26. Waliochangia kwa kuzungumza ni 23 na kwa maandishi ni watatu (3).
1. Mhe. Ali Salum Haji
2. Mhe. Asaa Othman Hamad
3. Mhe. Hassan Hamad Omar
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Kazija Khamis Kona
6. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
7. Mhe. Wavu Hafidh Ameir
8. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
9. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
10. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
11. Mhe. Mussa Ali Hassan
12. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa;
13. Mhe. Mohammed Haji Khalid
14. Mhe. Salma Mohammed Ali

15. Mhe. Salim Abdalla Hamad
16. Mhe. Salma Mussa Bilali
17. Mhe. Subeit Khamis Faki
18. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
19. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
20. Mhe. Saleh Nassor Juma
21. Mhe. Fatma Mbarouk Said
22. Mhe. Rufai Said Rufai; na
23. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwamba michango, maelekezo, maoni, ushauri pamoja na mapendekezo waliyotupa tutayafanyia kazi ipasavyo, kwani yatatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, ili kukidhi matakwa ya wadau wote wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi hapa nchini.

Baada ya kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, sasa naomba niainishe maeneo yaliyochangiwa kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Kwanza ni migogoro ya wavuvi katika maeneo ya hifadhi, ambayo tayari nafikiri imeshajibiwa, uvuvi haramu, ukatili wa wanyama, Sheria ya Uvuvi namba 7 mwaka 2010, machinjio ya mifugo likiwemo Chinjio la Kisakasaka, bei ndogo ya mwani na uvuvi wa Bahari Kuu kwa kuwezesha wananchi kuvua katika maeneo ya bahari kuu. Taaluma kwa wafanyakazi, wafugaji, wavuvi na wazalishaji wa mazao ya baharini, majosho ya mifugo ikiwemo ujenzi wa josho la Mjimbini; Pemba.

Mambo mengine ni Sera ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, uimarishaji takwimu, wizi wa mifugo, uanzishwaji wa Chuo cha Uvuvi, ubora wa mifugo na wanyama wanaopewa wafugaji, upandishaji ng'ombe kwa sindano, uwekezaji katika ufugaji wa kuku, masoko ya samaki Malindi na Tumbe, miradi ya mifugo na uvuvi, taaluma na usarifu wa bidhaa za mifugo na mazao ya baharini na kadhalika.

Mhe. Spika, sasa naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kuwasilisha majibu kwa hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Amina Iddi Mabrouk, yeye alikuwa na hoja kwamba idadi ya wafugaji 20 waliofundishwa uhifadhi wa malisho, idadi hii ni ndogo pamoja na ziara za kutembelea pia ni kidogo.

Mhe. Spika, jawabu ni kwamba wizara inakubaliana na maoni ya kamati, isipokuwa imetekeleza hayo kutokana na uwezo wa kifedha. Kwa mwaka ujao wa fedha wizara inategemea kutoa mafunzo zaidi ya uhifadhi wa malisho na ziara za kuwatembelea wafugaji katika uendelezaji wa Mradi wa *SSP* na *SDPL*.

Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa nadhani wameshajibiwa, kwa hiyo sina haja ya kupoteza muda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad, yeye alikuwa na hoja kwamba *pumps* tano za kuingiza maji katika mabwawa ya kufugia samaki zimetolewa Pemba, je kwa Unguja kuna mpango gani na kuna hasara gani kwa mradi wa ufugaji wa samaki kwa kukosa fedha.

Mhe. Spika, jawabu ni kwamba wizara hivi sasa iko katika kununua *pumps* tatu ambazo zitatolewa kwa wafugaji wa samaki kwa upande wa Unguja. Vile vile kuhusu mradi wa ufugaji wa samaki katika robo ya nne umepatiwa fedha shilingi milioni 20, na matumizi yake yameanza pamoja na kununua *pump* moja ya maji na ujenzi wa bwawa la mfano kisiwani Pemba.

Hoja yake ya pili wizara ina lengo la kushauri kufuga ng'ombe wangapi nchini, utafiti wa kuku wa kishingo umefikia wapi, tatizo la usafi kwa wafanyakazi na kutoa huduma za ugani.

Mhe. Spika, jawabu ni kwamba Sera yetu ya Mifugo imeelekeza katika kupunguza idadi ya ng'ombe wa asili kwa asilimia 40, ili kupunguza wingi wa ng'ombe hao na hapo hapo kuongeza idadi ya ng'ombe chotara na upandishaji wa ng'ombe kwa sindano.

Utafiti wa kuku kishingo uko katika hatua ya majaribio ya utunzaji, kuangalia wanavyoweza kustahamili maradhi na mazingira. Matokeo ya awali yameonesha kuwa kuku hao wanao uwezo wa kuzalisha mayai 200 kwa mwaka tofauti na mayai 60 ya kuku wa asili.

Wizara inakiri kuwepo upungufu wa usafiri kwa watoa huduma za ugani. Mhe. Spika, tunamuahidi Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako Tukufu, kwamba wizara itajitahidi kutatua tatizo hilo kwa kila hali ya kifedha itakavyoruhusu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, yeye alikuwa na hoja kwamba ng'ombe wa *PADEP* kutoweka tatizo nini? Taaluma itolewe kabla ya wafugaji kupatiwa ng'ombe hao.

Mhe. Spika, jawabu ni kwamba baada ya kumaliza mradi wowote umiliki wa mifugo unakuwa wa wafugaji wenyewe, utowekaji wa mifugo hiyo hutokana na aidha kwa mfugaji kutochukua juhudi za utunzaji, kufa au kuamua kuwauza.

Hata hivyo, zipo shehia mbali mbali za Pemba mifugo hiyo ipo na inafanya vizuri sana na shehia hizo ni kama Chokocho, Ukutini, Kuukuu, Mjimbini, Kisiwani, Wingwi, Kiuyu na Shumba. Wizara inao utaratibu wa kutoa taaluma kabla ya wafugaji kupatiwa mifugo, tumefanya hivyo kwa kupitia miradi ya kutoa mifugo chini ya ufadhili wa *IAA, HPI, IFAD, PADEP, MACEMP* na *TASAF*.

Mhe. Mjumbe, hoja yake ya pili ni kwamba watu wasio wafanyakazi wanaishi katika nyumba za wizara, wakati wafanyakazi wanapata shida za makaazi. Mhe. Spika, ni kweli wizara yangu inaendelea na kuchukua hatua ya kuwahamisha watu ambao hivi sasa sio tena watumishi wa serikali au wizara, ili kuwapatia wafanyakazi wa wizara yetu nyumba hizo.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, yeye pia alikuja na hoja kuhusu tatizo linalowakabili wavuvi wengi wadogo wadogo ni mitaji, kwa ajili ya kupata vifaa bora vya uvuvi.

Mhe. Spika, wizara yangu inafahamu tatizo hilo la mitaji kwa wavuvi wadogo wadogo, kwani taasisi nyingi za kifedha yakiwemo mabenki yana masharti magumu kwa wavuvi wengi kuweza kuyatimiza.

Hata hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Mradi wa *Sea Fish* itaangalia uwezekano wa kuwezesha Sekta Binafsi na vikundi vya wavuvi, kupata mitaji kwa utaratibu maalum wa ruzuku kwa kupitia vikundi vyao, ambayo itawezesha kununua vifaa vya uvuvi wanavyohitaji.

Mhe. Saleh Nassor Juma, yeye alikuwa na hoja kuhusu uhaba wa vifaranga vya kaa, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) *Campus* ya Nkrumah kimeanzisha Kituo cha Kuanzisha Vifaranga vya Kaa huko Beit-el-Raas.

Hoja yake ya pili ni kwamba hakuna madaktari wa mifugo wa kutosha. Mhe. Spika, ni kweli kuna upungufu mkubwa wa madaktari wa mifugo. Wizara yangu hivi sasa inashirikiana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuwalipia gharama za masomo wanafunzi watakaokwenda kusomea udaktari wa mifugo katika vyuo vyetu vya nchini au nje ya nchi, utaratibu huu utapunguza uhaba wa madaktari hapa nchini.

Vile vile hoja nyengine ni kuhusu wafugaji katika Jimbo la Wawi hawapati huduma za ugani. Mhe. Spika, kwa sasa wapo maafisa wawili ambao wanatoa huduma hizo za uzalishaji na utabibu wa mifugo katika Jimbo la Wawi. Kutokana na uchache wa wataalamu, wizara imetoa elimu kwa vijana wawili wengine ambao wanasaidia kutoa huduma za msingi za ushauri na utabibu wa mifugo katika ngazi ya shehia. Vijana hawa wapo katika kijiji cha Ng'ambwa na Vitongoji. Hata hivyo, wataalamu hawa ni wachache kulinganisha na mahitaji, kwa hiyo, tunawashauri wafugaji kuwaita wataalamu wa pale wakati wanapopata matatizo ya mifugo yao.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, yeye alikuja na hoja kuhusu fedha za mradi wa miundombinu ya mifugo zimeweza kupatikana zote na mradi huu umefikia wapi, hoja hii pia imechangiwa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa pamoja na ujenzi wa josho la Mjimbini; Pemba.

Mhe. Spika, jawabu ni kwamba mradi wa miundombinu ya mifugo unatekelezwa kwa fedha za SMZ pekee na fedha za mradi hazikupatikana zote. Makisio ya awali ya mradi mzima ilikuwa ni shilingi bilioni 7.2 kwa miaka minne, ambapo kwa miaka mitatu fedha zilizopatikana ni jumla ya shilingi milioni 234,253,000/= sawa na asilimia 3.3 na utekelezaji wake halisi ni wa kipindi hicho.

Kupatikana kwa michoro ya Chinjio la Kisakasaka, kukarabatiwa kwa vituo vya utabibu na uzalishaji wa mifugo Potoa, Matemwe, Dunga pamoja na nyumba za wizara za mtaalamu wa mifugo iliopo Mtoni ng'ombe, kuanza kwa ujenzi wa kituo kipya cha utabibu na uzalishaji mifugo cha Unguja Ukuu, ambao umefikia hatua ya kuezekwa hivi sasa.

Mhe. Spika, kuhusu ujenzi wa josho la Mjimbini kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi wa miundombinu wa mifugo ulipanga pamoja na malengo mengine kujenga josho la Mjimbini Pemba. Kwa hiyo, hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kukamilika kwa taratibu za zabuni na kupatikana kwa mkandarasi, ambaye ni *Exact Line Engineering Limited,* ambaye tayari ameshafunga mkataba na wizara yangu wa kujenga josho hilo.

Mkandarasi huyu yuko katika *mobilization stage*, ambapo kulingana na mkataba ujenzi unatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa hatua hii na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha na kukamilika mwakani. Shughuli nyengine zilizofanyika ni pamoja na uchoraji wa ramani, kutayarisha *BQ*, usafishaji wa eneo na uwekaji wa *beacon*.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, pia alikuja na hoja kwamba lini serikali itaanzisha Chuo cha Uvuvi Zanzibar. Mhe. Spika, jawabu ni kwamba wizara itafanya upembuzi yakinifu wa kuanzisha Chuo cha Uvuvi kwa kupitia mradi wa *Sea Fish* kwa mwaka ujao wa fedha.

Hoja yake nyengine aliitoa kwenye vifungu ambapo kifungu 220101 kuhusu gharama za simu kwa mwaka 2013/2014 iliidhinishiwa shilingi 480,000/= na mwaka wa fedha 2014/2015 kinaombewa shilingi milioni 1,440,000/=, kwa nini zimeongezeka kiasi hicho. Mhe. Spika, jawabu ni kwamba fedha hizi zinalipiwa *Internet* na *Cable Television*, matumizi ambayo mwaka jana hayakuwepo, kwa hiyo mwaka huu tumeyaingiza.

Mhe. Mjumbe, hoja yake ya tatu ni kuhusu kifungu 220201 chakula na vinywaji kwa mwaka 2013/2014 iliidhinishiwa shilingi milioni 2,626,000/= na mwaka wa fedha 2014/2015 kimeombewa shilingi milioni 1,890,000/= kwa nini zimepungua. Mhe. Spika, jawabu ni kwamba zilikuwa zikitumika kwa ajili ya mafunzo, lakini mwaka huu mafunzo hayo yamepunguzwa.

Mhe. Spika, hoja ya nne ya Mhe. Mjumbe kuhusu kifungu cha 22021 chakula na vinywaji kwa mwaka 2013/2014 iliidhinishiwa shilingi 600,000/= na mwaka wa fedha 2014/2015 kinaombewa shilingi 3, 210,000/= na kwa nini kimeongezeka.

Jawabu ni kwamba kifungu hichi kwa mwaka ujao wa fedha kimeongezewa kwa sababu kutafanyika mafunzo kwa wafugaji 200 juu ya uhifadhi wa malisho na wajasiriamali.

Mhe. Salma Mohammed Ali, yeye alikuja na hoja kwa nini asilimia 32 ya ng'ombe waliopandishwa hawakushika mimba. Mhe. Spika, jawabu kutokushika mimba kunasababishwa na mambo mengi yakiwemo hali ya ng'ombe mwenyewe, lishe ya wanyama wakati wa shurufu, mbegu zenyewe pamoja na mpandishaji mwenyewe.

Sasa inapotokea ng'ombe aliyepandishwa hakushika mimba, wataalamu wetu hufanya uchunguzi, kwa ajili ya kuweza kutambua tatizo ni lipi na kulipatia ufumbuzi. Nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba upandishaji una gharama, lakini gharama hizi ni ndogo kwa sababu serikali inatoa mchango mkubwa.

Mhe. Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu, kwamba hakuna kumbukumbu yoyote ya asilimia mia ya ushikaji mimba katika shamba lolote la mifugo duniani na hiyo ni kawaida.

Hoja nyengine ni kwa nini ndama waliowekewa kumbukumbu ni 409 tu. Mhe. Spika, jawabu ni kwamba kazi za kuweka kumbukumbu ndama wanaozaliwa ni zoezi endelevu, ambalo tumelianzisha na idadi ya ng'ombe 409 ni wachache, lakini lengo letu ni kuanzisha *database* ya ndama wote watakaozaliwa na kuanzisha kumbukumbu kwa ng'ombe wote kadri ya hali itavyoruhusu. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Subeit Khamis Faki, yeye alikuwa na hoja kuhusu kwa nini wafugaji wa mbuzi na kuku katika Wilaya ya Micheweni hawakusaidiwa tena au mradi ulikufa.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba wizara ina lengo la kuwasaidia wafugaji kadri hali itavyoruhusu. Katika mwaka wa 2013/2014 wizara ilipanga kusaidia vikundi vinne vya wafugaji mbuzi kutoka shehia ya Majenzi, Wingwi

Mapofu, Maziwang'ombe na Micheweni, lakini kutokana na kukosa fedha ni shehia mbili tu za Majenzi na Wingwi Mapofu ndio waliopata kusaidiwa mbuzi 24 wa maziwa.

Wafugaji kuku wa kijiji cha Kiuyu Mbuyuni walipata msaada kutoka Mradi wa *Millenium Village*. Aidha wafugaji 15 wa Makangale walisaidiwa ng'ombe 17 kupitia mradi wa *ITP* wa *Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe*.

Mhe. Salma Mussa Bilali, yeye alikuwa na hoja mbali mbali kwamba Mhe. Mwakilishi ameishukuru serikali kwa kuijengea Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu jengo zuri tena la kisasa, lakini masikitiko yake ni kwamba hadi hii leo wizara bado haijawapatia mamlaka wafanyakazi wa kutosha, jambo ambalo linazorotesha ufanisi mzuri wa utendaji kazi.

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi SMT imepeleka wafanyakazi katika Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kama muongozo, kuendeleza mamlaka kama anavyoshauri Mhe. Mjumbe.

Wafanyakazi hao tayari wanaendeleza majukumu yao katika vitengo vya uhasibu, udhibiti rasilimali watu na hivi karibuni tunategemea kupeleka wanasheria.

Hoja yake ya pili Mhe. Mwakilishi pia ameishukuru wizara kwa kuweza kuwasomesha vijana 13 kuhusiana na Uvuvi wa Bahari Kuu na ametaka kujua hatima ya vijana hao.
Mhe. Spika, miongoni mwa hatua ambazo wizara yangu inaendelea kuzichukua ni pamoja na kuwashajihisha wawekezaji kuleta meli za uvuvi zitakazoshiriki katika uvuvi wa bahari kuu. Hivyo, meli hizo zitakapokuja zinahitaji kuwa na wavuvi wenye ujuzi wa kuvua katika bahari kuu.

Kwa kweli ni kusudio la wizara yangu kuwa vijana watakaohitimu masomo ya uvuvi wa bahari kuu wataweza kuomba kazi na kuajiriwa katika meli hiyo. Elimu wanayohitaji vijana hawa inaweza kuwasaidia katika kujiajiri kwenye uvuvi wa kina kirefu kwa kuunda vikundi na kutumia vyanzo vya fedha mbali mbali kwa ajili ya kuomba mikopo nafuu itakayowezesha kushiriki katika uvuvi huo.

Mhe. Spika, hoja yake ya tatu Mhe. Mjumbe ni kwamba serikali bado haijawa tayari kusimamia sekta hii ya uvuvi, kwa sababu vijana wetu wa Kikojani bado wanavua kwa nyavu ndogo kama vile chandarua, ili samaki wakubwa waje kwenye maji madogo, kuwe na dagaa na maafisa uvuvi wapo wanaowaona, lakini wanaridhishwa na vidoo vya dagaa. Sasa je, samaki wakubwa watapatikana au watakuja juu.

Mhe. Spika, jawabu ni kwamba nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba wavuvi wetu wa Kikojani bado wanaendelea na uvuvi haramu wa samaki wachanga. Hali hii inasababishwa na ukaidi wakati mwengine wa kutofuata sheria za uhifadhi wa mazingira ya baharini na kutokubaliana na maelekezo ya wataalamu wetu na sio vidoo vya dagaa kwa vijana wetu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, yeye alikuwa na hoja kwamba miongoni mwa wananchi walioitikia wito wa ufugaji wa mazao ya baharini (ufugaji wa samaki) ni wananchi wa Chambani, lakini serikali haiwasaidii wananchi hao.

Mhe. Spika, jawabu ni kweli kwamba miongoni mwa wananchi walioitikia wito kwa shughuli za ufugaji wa mazao ya baharini ni wananchi wa Chambani, na wizara iko karibu sana na wafugaji hao kwa kuwatembelea na kuwapa ushauri wa kitaalamu.

Vile vile Kikundi cha Kwadawa Kichimba Chambani ambacho kinafuga samaki na uzalishaji wa chumvi kilisaidiwa fedha, kwa ajili ya mradi wa chumvi pia walisaidiwa fedha taslimu shilingi 300,000/=. *(Makofi)*

Aidha, katika kuendeleza shughuli za ufugaji, mwanakikundi mmoja alipelekwa China, wizara itaendelea kuwasaidia wafugaji wengine kadri ya fedha zitavyopatikana, nadhani ni vyema tuwe na subira. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan, yeye alikuwa na hoja kuhusu ukatili wa wanyama hasa kupigwa na kubebeshwa mizigo mizito, na hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na Mhe. Saleh Nassor Juma, wizara imefanya mambo yafuatayo kudhibiti ukatili wa wanyama.

Kutoa mafunzo kwa wafugaji juu ya utunzaji wa wanyama hawa hiyo ni hatua ya kwanza, vile vile kutoa vipeperushi kwa mafunzo na mafunzo kwa watoto maskulini, kushajihisha taasisi zisizo za kiserikali kushiriki katika kampeni ya kuzuia unyanyasaji wa wanyama, kuwashirikisha viongozi wa dini na wafugaji wengine

katika kutoa taaluma juu ya kuwatunza wanyama, kumuajiri askari mstaafu kukamata wahalifu wanaonyanyasa wanyama.

Jitihada za pamoja za kushirikisha jamii na vyombo vya ulinzi zinahitajika kuendelezwa kwa kuchukuliwa hatua wanaofanya vitendo hivyo kwani vitendo hivyo vinafanywa katika maeneo ya mjini ambako mifugo hiyo hairuhusiwi kuwepo; kazi ambayo Baraza la Manispaa inafanya jitihada kubwa na kwa kiasi kikubwa vitendo hivyo vimepungua. Hata hivyo Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuwaelimisha wafugaji ili waweze kuwatumia wanyama wao vizuri kwa miaka mingi bila ya kuwaletea athari.

Mhe. Salma Mohammed Ali vile vile alikuwa na hoja ya idadi ya majosho yaliyopo Unguja na Pemba ni mangapi na yanafanya kazi? Jawabu ni kwamba yapo majosho 13; Unguja 10 na Pemba 3, majosho yanayofanya kazi ni manne ambayo ni Kisakasaka, Makangale, Kizimbani na Pangeni na yasiyofanya kazi ni tisa ambayo ni Kipange, Mwera, Bambi, Hanyegwamchana, Binguni, Bweleo Makunduchi, Konde na Ole.
Majosho haya hayahitaji matengenezo makubwa, kwa kweli Wizara imo katika jitihada za kutafuta fedha ili kuyaboresha, hata hivyo wafugaji wanashauriwa watumie mabomba au watumie dawa za kupe za mafuta za kunyunyizia hasa kwenye maeneo ya mbali au yenye vipando ili kuepusha migogoro na wakulima.

Hoja yake ya pili Zanzibar kuna wafugaji wangapi? Kuna wafugaji ishirini (20) waliopatiwa mafunzo ya uhifadhi wa malisho na asilimia ngapi? Jawabu napenda kumuarifu Mhe. Salma kwamba Zanzibar tuna wafugaji wa ng'ombe na maziwa wafikao 20200, kutokana na idadi hiyo inafanya wafugaji waliopatiwa mafunzo ya uhifadhi wa malisho kuwa asilimia moja tu, nakubaliana naye kuwa ni mdogo lakini kama nilivyosema awali kwamba kutoa mafunzo kutokana na bajeti ambayo tumepitishiwa katika Baraza lako Tukufu.

Vile vile Mhe. Mohammed Haji Khalid alikuwa na hoja katika uzalishaji wa nyama ya mbuzi na kondoo haikutajwa je uzalishaji wake ni upi. Jawabu uzalishaji wa nyama ya mbuzi ni tani 50 kwa mwaka 2012 na tani 52 kwa mwaka 2013. Aidha uzalishaji wa nyama ya kuku ni tani 498 kwa mwaka 2012 na tani 704 kwa mwaka 2013.

Mhe. Panya Ali Abdalla naye alikuja na hoja ya uimarishaji wa huduma za ufugaji ni muhimu na kufurahishwa wazo la kutoa mwamko wa matumizi mazuri ya sanaa na nishati mbadala. Jawabu, tunashukuru Mhe. Panya kwa ushauri wake na tutatekeleza pongezi nazipokea na tutaendelea kuwa pamoja nao na ushauri wa kitalo, pia nitafanya ziara kwa vikundi ambavyo bado sijabahatika kuvitembelea.

Mhe. Rufai Said Rufai naye alikuja na hoja zake vipi wafugaji watanusurika na wizi wa ng'ombe. Wizi wa mifugo ni sawa na wizi wa mazao mengine yoyote, unapaswa kushughulikiwa na mfugaji mwenyewe na vyombo vya sheria. Hata hivyo Wizara inawashauri wafugaji kuweka mifugo yao karibu na majumba yao ili kuimarisha ulinzi, aidha Wizara yangu inawashauri wanajamii kuwa na utaratibu wa ulinzi shirikishi, vile vile sheria ya kumiliki rasilimali za mifugo inalazimisha kuongeza uwezekano wa kuzuia wizi wakati wa kusafirisha mifugo kwa kutoa vibali ambavyo mnyama anatambuliwa na Sheha na Shehiya anakotoka.

Mhe. Spika, nashukuru na hapo ndio mwisho wa majawabu yangu kwa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Nina imani kwamba wengi tumewajibu na nahisi kwamba wameridhika, na kama kuna kasoro basi buti ruksa, lakini hata hivyo Mhe. Mgeni Hassan naye alichangia kwa maandishi kwa hivyo kwenye *hansard* naye alisema kwamba mimi Mgeni Hassan Juma nimechangia hotuba yake, kwa hivyo tunakushukuru sana Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Toa hoja Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Samahani Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Wale wanaounga mkono hoja ya Mifugo na Uvuvi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolea uamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya Matumizi vya Wizara yangu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujakaa kwenye Kamati ya Matumizi nimearifiwa kwamba wapo vijana wetu ambao wamekuja kuona shughuli zetu, nao ni ni Wanafunzi kutoka *Zanzibar Vision Academy* Jumla yao ni wanafunzi 10 pamoja na walimu wao 3, nawaomba wasimame, wale pale, nakushukuruni sana na karibuni sana.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 22 WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0012	Idara ya Mazao Baharini; Pemba	21,000,000
Kifungu 0013	Idara ya Uzalishaji wa Nyama; Pemba	6,000,000
Kifungu 0014	Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo; Pemba	

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Waziri wake, na akatwambia kuwa aliyekuwa hakumjibu ruhsa kupiga buti, kwa hivyo tunamshukuru kwa kauli yake hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jana niliuliza swali asubuhi la nyongeza ambalo kuwa lilikuwa suala la mifugo na uvuvi, lakini nilipochangia pia nikalizungumza suala hili kuhusu kusaidiwa, kwa sababu Mhe. Waziri katika jibu lake alinambia atanijibu kwa maandishi lakini yale maandishi hakunipa.

Na mimi sikumuuliza vikundi vya kusaidiwa kwa mwani, alisema kuwa tangu 2007 wanasaidia wavuvi sio vikundi vya mwani. Sasa kwa hivyo naona Mhe. Naibu Waziri naona kanijibu kwa kejeli, mimi sikuuliza vikundi vya mwani kusaidiwa, niliuliza wavuvi, kuna tofauti ya wakulima wa mwani na wavuvi, mimi niliuliza wavuvi.

Kwa hivyo Mhe.Naibu Waziri alinambia atanijibu kwa maandishi lakini mpaka leo asubuhi hii hajanijibu, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri anijibu swali langu hilo ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Inahusiana na masuala ya mapato Mhe. Bikame, tusubiri katika eneo linalohusika.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Twende Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nilipokuwa nikichangia nilimwambia Mhe. Waziri, kutoridhishwa kwangu na mapato ambayo yalikuwa ni ya mwaka jana na mapato yale yale yamekuja kwa mwaka huu. Na nilimuomba Mhe. Waziri anisaidie sababu zilizosababisha hata ikabidi waridhike na mapato yale yale ya Shilingi 613 milioni kwa mwaka 2013/14 na mapato hayo hayo yawe yanakisiwa kukusanywa tena kwa mwaka 2014/15, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ni kweli makisio ni yale yale lakini kwa sababu mwaka jana hatujafikia kiwango kile, kwa hivyo ndio maana tukaweka makisio yale yale, kwa hivyo hatuwezi kuweka zaidi wakati huku hatujafika, jawabu ilikuwa ni hivyo tu kwa kweli. Hatujafikia wakati ule, kwa hivyo tumeyaweka yale yale ili kuona kwamba je tutayafikia au laa, ni hivyo tu ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli majibu hayajaniridhisha hususan tukizingatia kwamba bahari yetu Zanzibar na visiwa vya Unguja na Pemba vyote vimezungukwa na bahari, na tuna kila sababu na kila uwezo wa kuweza kutumia rasilimali hii na kuweza kupata mapato mazuri zaidi yatakayoweza kusaidia maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

Kuridhika na utaratibu wa makusanyo ambayo yalikuwa yamepangwa mwaka jana na mwaka huu tukasema tunataka kuendelea na mapato yale yale si jambo ambalo linaweza kuleta faraja katika mustakbali wa kunyanyua uchumi wetu, pamoja na kwamba nitakubaliana na hoja kutokana na mipango yao, ningeliomba basi Mhe. Waziri pamoja na timu yake katika Wizara hii wajitayarishe na kuangalia mikakati mizuri zaidi ya kuweza kunyanyua kipato katika Wizara yao na kwa nchi kwa ujumla. Naomba tuendelee Mhe. Spika.

Kifungu 0014	Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo; Pemba	12,000,000

Kifungu 0015	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi; Pemba	6,000,000
Kifungu 0016	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi; Unguja	430,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo	56,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Mazao ya Baharini; Unguja	70,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Uzalishaji wa Wanyama; Unguja	9,000,000
	Jumla ya Fungu	**613,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo Juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 22 WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0010 Idara ya Mifugo, Sera na Utafiti 30,000,

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia niliainisha baadhi ya mafungu ambayo yalikuwa yamekua, na Mhe. Waziri amekuja kujibu baadhi tu ya vifungu ambavyo ilikuwa nilitaka kupata ufafanuzi wake, lakini kuna fungu hili 0010 ambapo mwaka jana lilikuwa na kasma ya shilingi 880,000/= lakini mwaka huu linaombewa fedha 3,040,000/= ufafanuzi wake sikuupata, naomba maelezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu fafanua vizuri hicho kifungu chenyewe.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba kwa ujumla wake fungu la mishahara ya fedha taslim ambapo katika eneo la mishahara hapana kitu, lakini katika malipo ya likizo, malipo baada ya saa za kazi pamoja na malipo ya kujikimu haya yameainishiwa fedha na ametiliwa fedha katika mafungu yake, lakini mwaka jana kulikuwa kuna 880,000/= mwaka huu wa fedha zimeombwa Shs. 3,040,000/= ongezeko ni kubwa, lakini alipokuwa akitoa ufafanuzi Mhe. Waziri hakutoa ufafanuzi wa hili naomba kupata jawabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mahmoud hakunipata vizuri. Wakati nawasilisha nilijibu mimi suala hili na nilimwambia kama ifuatavyo; ni kweli kwenye mishahara halikuwepo lakini bajeti ya mwaka jana haikutimia kupata, na tulikuwa tukidaiwa sana pesa zile za *over time* na mambo mengine ya kujikimu ndio maana safari hii limejitokeza kubwa kwa sababu pamoja na ya mara hii kutaongezeka, ya mwaka jana hatukupata lakini na mwaka huu pia yapo, ndio maana ukaona limeongezeka hili fungu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0010 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Nakushukuru Mwenyekiti kwa kunipa na mimi fursa hii ingawa mambo tunajifundisha lakini tuvumilie tu hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza suala langu la kwanza ambalo nataka nipate ufafanuzi zaidi kuhusu jengo lile la soko la Tumbe, jana nilipochangia nilimwambia Mhe. Waziri atakapokuja anipe takwimu ya matumizi ya gharama zilizotumika katika jengo lile na kufikia pahali jengo lile likajengwa halina ubora, jengo ni bovu, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti fedha nyingi zimetumika pale, pesa za kusaidiwa. Kwa hivyo Wizara hii haikuwa makini katika kushughulikia ujenzi ule. Kwa hivyo Mhe. Waziri kutwambia tu kuwa linakarabatiwa jengo hata halijatumika limekuwa linaanza kukarabatiwa hilo ina maana ni jengo halina uhakika.

Halafu nilimwambia kwamba kuna ripoti yakinifu ya Mkaguzi kwa mradi wa Taasisi za Serikali. Nilimwambia kiko kitabu hiki lakini kwa sababu hawana ufuatiliaji hawajui chochote kinachoendelea. Nikamwambia niletee hizo takwimu za hizo pesa zilizotumika kwa sababu kwa mujibu wa kitabu hiki anasema, ukaguzi uliofanyika haukuridhishwa na hali halisi ya ujenzi huo. Ukilinganisha fedha zilizotolewa na kutumika hadi kukamilisha ukaguzi ujenzi wa sehemu ya soko hilo haujakamilika naona hakujibu hasa hili suala, kajibu Naibu Waziri kasema kwa kuwa tunafanyia ukarabati na halijakabidhiwa kwa Wizara kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alete majibu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ninashukuru Mhe. Spika, nakumbuka hili alijibu Naibu Waziri, lakini kwa kuongezea na kwa faida ya Wajumbe ni kweli soko hili lilijengwa na kampuni ya ujenzi ya Ngogo kwa gharama ya shilingi 712,500,000 kwa fedha za mradi wa *MACEMP* kwa kuwezesha wavuvi wa Kaskazini Pemba kuuza samaki wao katika hali ya ubora na unadhifu.

Ujenzi huu umeanza mwaka 2012 na kumalizika 2013, lakini hadi leo bado hatujakabidhiwa. Soko hili lina sehemu ya kuwekea mambo kadhaa ikiwemo mitambo ya barafu na kadhalika.

Labda nimueleze kwamba Wizara inakubali kwamba kuna kasoro zilijitokeza katika lile soko na kasoro zile sio kama na sisi tumeridhika, na sisi wenyewe kama Wizara hatukuridhika na tukazuia baadhi ya fedha ambazo ni milioni hamsini (50,000,000) kwa mkandarasi yule tukamwambia mpaka uhakikishe kwamba unafanya marekebisho kwa mambo ambayo yamebakia.

Na kwa kweli tumezuia na tumekaa na watu wa Tumbe vile vile tukajadiliana ili kuona kitu tayari, kwa sababu tunahisi kwamba tukikaa sana lile soko litaendelea kuharibika na wakati tunaamini kwamba likianza kazi angalau kutakuwa na tija itapatikana pale, mapato fulani yatapatikana. Na tulikubaliana hivyo kwamba basi acha tuendelee kulitumia lile soko, wakati huo tumemzuia mkandarasi, tumezuia milioni hamsini kutoka benki ili tuone kwamba zile fedha tunazipata na tufanye yale marekebisho madogo madogo ambayo yalibakia.

Tumefanya *process* lakini mpaka sasa tumejaribu kutafuta ushauri kwa Mwanasheria Mkuu namna gani ya kuzidai pesa zile kutoka kwa *Eco Bank*, lakini Mwanasheria Mkuu na yeye alitwambia kwamba kwa kweli inabidi kwanza kwa sababu mkataba ilibidi tuanze nao tokea mapema kama makubaliano yetu yalivyotakiwa yawe.

Kwa hivyo tunasubiri ushauri zaidi na Mwanasheria Mkuu ili tuzipate 50,000,000 zilizobakia kwenye *Eco Bank* ili tushirikiane na wananchi wa Tumbe tuendeleze zile sehemu ndogo ndogo ambazo zilibakia, hivyo ndivyo tulivyokubaliana. Tulikuja pale tukafanya mkutano na watu wa Tumbe na akasema basi acha tuanza hii kazi huku tunapata mapato madogo na kasoro ndogo tunazirekebisha. Na tumerekebisha baadhi ya mambo, sasa labda tena Mhe. Bikame sijui kama umeridhika. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini narudia tena kusema kauli yangu kuwa hawana ufuatiliaji.

Ujenzi huu ulianza tarehe 27/1/2011 ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitiliana mkataba na Kampuni hii ya Ngogo, sasa leo ananambia ulianza 2012. Na Mhe. Waziri alipojibu alisema karibu milioni kumi na saba (17,000,000) sikusikia vizuri lakini naona hivyo. Katika kitabu hiki karibuni milioni mia mbili na sitini na tatu laki nane ishirini na nne, mia sita sitini na sita pointi nane saba (263,824,666.87) ambazo zimeshatumika.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri na aseme ule ukweli halisi ulivyo kama hana utaratibu au hana jawabu ya kunijibu basi Mhe. Mwenyekiti kwa hili ninakuomba tumechoka kupewa ufadhili na watu mbali mbali lakini hatima yake haionekani.

Kwa hivyo naomba muongozo wa kiti chako au Mhe. Waziri ataendelea kunijibu lakini naona jawabu zake na jawabu zilizomo kwenye kitabu hiki ni tofauti. Hiki kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kwa hivyo naomba anijibu niridhike. Hakuna maridhiano ya majibu haya Mhe. Mwenyekiti tuunde Kamati.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo kidogo kuhusiana na suala hili. Kwa kweli hoja za Mkaguzi zote zilijibiwa, na wakati Mkaguzi alipokwenda bado lile jengo linaendelea, kwa hivyo litakapomalizika ndipo tutaanza hayo marekebisho ambayo anayodai Mhe. Bikame.

Na mkataba ulitiwa saini 2011 lakini ulikuwa na tatizo la *bond* ambayo sehemu ilikatika au ilimeguka mwaka 2012 na ndio ujenzi ulianza, lakini kwa sababu hoja zote za Mkaguzi na wakati huo kwa sababu ujenzi bado ulikuwa unaendelea. Kwa hivyo utapomaliza ndipo zile kasoro tutazifanyia kazi. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi siridhiki tena na kuendelea na shughuli hii Wizara tu, kutokana na matatizo yaliyojitokeza katika jengo lile basi labda pawe na mawazo mengine, lakini kuendelea kuwakabidhi wao kwa sababu jamani kitabu hiki 2011/2012 kitabu hiki kinatolewa, na mpaka leo 2014 miaka 2 hakijulikani kinachoendelea halafu waachiwe Wizara tena watakuja kutwambia nini hapa? Utaratibu utumike!

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na naomba nisaidie kidogo suala hili ambalo ninalijua sana, na nafahamu hisia za Mhe. Bikame kwa niaba ya watu wa Tumbe ninalifahamu sana na nazielewa vizuri kwamba walitaka sasa iwe ni wakati soko limalize, na mimi ninakubaliana naye sana kwa hili, lakini naomba akubali kwamba serikali ilifanya jambo kwa nia njema kabisa na mimi nilishiriki katika mwanzo wa shughuli hii kuona kwamba eneo la Tumbe ambalo lina wavuvi wengi

sana na linapata samaki wengi sana kwa mwaka wanaekewa *facility* ambayo itawasaidia katika shughuli zao za kimaisha. Soko kubwa sana lenye mambo mengi ndani kama ulivyosema ghala za baridi na mambo mengine.

Sasa ujenzi wake ni kweli kwamba ulipata matatizo kidogo, lakini nimwambie kwamba katika ujenzi ule Idara ya Mazingira ilihusika, *Environmental Impact Assessment* ilifanywa na bahati mbaya kumetokea matatizo kidogo katika ujenzi, lakini ni kweli kwamba Wizara na Serikali soko halijakabidhiwa.

Kwa hivyo ni jambo la kawaida katika ujenzi kwamba kuna pesa maalum zinawekwa, zinazuiwa na serikali kuona kwamba hazilipwi mpaka kuhakikisha kwamba ujenzi umemaliza kwa kiwango ambacho kimetakiwa.

Kwa hivyo Mhe. Waziri amesema kwamba ile *portion* ya pesa ambazo zilitakiwa zizuiwe tayari ziko bado hajalipwa, kwa hivyo Mhe. Bikame aiachie serikali ili fedha hizi ambazo hazijalipwa na Mkandarasi yuko katika *site* hivi sasa basi aone, kwamba kwa nia njema kabisa na kwa usimamizi wa Wizara hii ambayo ninaiamini kabisa watendaji wake kwamba watalisimamia hili jambo baada ya muda fedha hizi ziko mikononi zitatumika kumaliza ujenzi kwa kiwango kile ambacho kimetakiwa.

Na ndio maana hizi pesa huwa zinawekwa makusudi katika mikataba ili kuzuia, *intention* hii kumalizia pale ambapo imefikia. Kwa hivyo, ninamuomba sana ndugu yangu Mhe. Bikame hili ninajua, hisia za wananchi wa Tumbe na Wilaya ya Micheweni wote na Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa jumla; kwamba wanataka soko lao limalizwe, kwa hivyo, serikali hasa Wizara hii naamini kwamba wako katika hatua za mwisho za kumalizia Mhe. Mwenyekiti. Naomba sana aiamini Wizara, itafanya hivyo!

Mhe. Mwenyekiti: Unajua *concern* ya Mhe. Bikame kwa yale maelezo. Kwanza anaona jambo lenyewe limechukua muda mkubwa sana halijamalizika. Pili kilichofanyika kimethibitishwa kwamba hakitoshelezi.

Sasa ili mumridhishe ninavyohisi najua namna ya kuwaridhisha watu, nafahamu hivyo, sasa angalau mwambieni kazi hii itafanyika mpaka lini? Lakini pili mumwambie hatua gani nyengine mtazochukua ili kuondoa haya mapungufu na huyo mkandarasi wenu. Hebu mwambieni ili aridhike huyu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kwamba Wizara imekubali kwamba kuna kasoro na ndio maana tukazuia zile milioni hamsini (50,000,000) baada ya kuona kwamba kuna kasoro, na sisi inatuudhi kwa kweli, tunataka lile soko lianze kazi na ndio maana nikafanya kikao mimi binafsi pamoja na watu wa Tumbe ili kubadilishana fikra nini cha kufanya. Na sote tukakubaliana pale basi acha hili soko lifanye kazi, kwa sababu kasoro si kwamba zinazuia kwamba kusiwe na shughuli zinafanyika pale, kwa sababu tukikaa lile soko litaendelea kuharibika, lakini acha tuendelee na shughuli zetu, kwa sababu lile soko tuna imani kwamba litatia fedha nyingi.

Na tukakubaliana hivyo na watu wa Tumbe wakasema basi sawa hamna tatizo, tutashirikiana na huku tunazidai hizi 50,000,000 ili zile kasoro ambazo zilibakia pale twende nazo pamoja na wao wenyewe ndio watasema wapi tufanye; tutawashirikisha kikamilifu ili tuone kwamba tunaenda sambamba. Kwa sababu si kwamba limetufurahisha, hapana. Kwa hivyo sasa tuko katika juhudi ya kuzitafuta zile milioni hamsini (50,000,000) kutoka *Eco Bank* ili tuziingize pale, hivyo ndivyo tulivyokubaliana.

Kwa hivyo, pamoja na yote ninajua *concern* ya Mhe. Bikame na ndio hamu ya kutaka jambo liwepo kule kila mtu anakuwa hivyo na sisi tunataka lifanye kazi hivyo kwa sababu likifanya kazi kwetu ni faraja.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Bikame hebu tupe subira kidogo, sisi huku tuko katika juhudi ya kuzipata milioni hamsini (50,000,000), lakini lile soko acha lianze kazi, kwa sababu kuna *fees* zile zitakuwa zinapatikana, zile zitakuwa zinafidia kukarabati sehemu nyengine. Kwa sababu zile 50,000,000 zile ni mali ya soko si zetu hazirudi Wizarani, zile zitabakia katika soko na ndivyo tulivyokubaliana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mashaka, mimi nataka tuwe na ukweli na uwazi na lazima tuthamini kile tunachosaidiwa na wenzetu tukithamini, kwa sababu wao wanatusaidia sio kuwa hawana watu wa kuwapa; kuna masikini tele wa kuwapa, lakini inasaidiwa serikali kwa maslahi ya nchi, ina maana lile soko likiwepo pale hata hiyo serikali nayo itapata mapato. Leo kinafanywa kitu hakishughulikiwi, wanakwenda kutafutwa watu waliokuwa hawana uwezo, wanakwenda watu waliokuwa shangazi na mjomba wanapewa kitu halafu kitu kile ndio basi.

Unaiona hiyo takwimu anayosema matumizi yanayotumika pale na hiki kitabu hiki hazilingani pesa haziko sawa sawa, na ndio maana jana sikumwambia hii takwimu nikataka aniletee hizo zake yeye, nijue kama kweli

pana ufuatiliaji, lakini pia wanakwenda kufanya mambo kule ya maajabu ajabu, sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakwambia tuunde kamati au tuipeleke Kamati ya *PAC* tena iende pale, kwa sababu kwanza wametuchikiza kuja pale wakawafanyisha watu wetu kazi wanyonge wa Mungu hata kuwalipa wasiwalipe, halafu aniambie Mhe. Waziri hizo milioni zao sitini (60,000,000) zilizobakia asiwalipe tena Kampuni awalipe wale wanaodai pale.

Mhe. Mwenyekiti hadi tufike pahali kama tunaisimamia kweli serikali tuisimamie na waridhike kusimamiwa, sio wakitaka kusimamiwa warushe vichwa, aa haiwezekani hilo. Ikifika pahali wa kusimamiwa ni kufanywa uchunguzi kitu kikajulikana ukweli nani mharibifu, ndio watakapofanya kazi zao vizuri hao, lakini wasikae maofisini tu wakawapeleka watu huko, nendeni kwa kuwa ni Kampuni ile ni Kampuni gani? Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubali.

Mhe. Mwenyekiti: Ninavyoelewa jambo hili Mkaguzi na Mdhibiti wa Matumizi ya Serikali alifanya kazi yake, Kamati ya *PAC* imekwenda ikaona na ikatoa mapendekezo yake mengine yametajwa hapa. Sasa ikisema utengeneze Kamati nyengine nayo itabidi ni jambo la kufikiria sana. Mhe. Waziri wa Fedha hebu tusaidie.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru mimi nimeyafahamu sana maelezo ya Mheshimiwa pale Mwakilishi na *concern* zake, lakini kama ulivyoeleza na mimi nilikuwa nataka nipite kwenye misingi hiyo hiyo kwamba Mdhibiti na Mkaguzi amekwenda ametoa ripoti yake, *PAC* imekwenda imetoa ripoti yake, sasa ni jukumu la serikali kuangalia yale mambo yote ambayo yamependekezwa kupitia ripoti hizi mbili ili tuweze kuyafanyia kazi.

Nataka nimuombe tu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba atuachie tutazame, na nataka nimuahidi kwamba yale yote mapungufu tutayarekebisha katika kipindi kifupi, si zaidi ya miezi sita inayokuja ili hili soko liweze kufanya kazi kwa ukamilifu. Tutashirikiana na Wizara ya Uvuvi ili kuona kwamba hili soko linafanya kazi kwa ukamilifu.

Vile vile tutajaribu kuangalia yale mapungufu yaliyojitokeza chanzo chake nini na wapi yameanzia, ili tuweze kurekebishana basi matatizo kama haya yasiweze kutokea katika miradi mengine na katika kipindi kingine.

Namuomba sana Mhe. Mwakilishi aturuhusu tuendelee, na ninamuahidi kwamba tukimaliza tu bajeti yetu mimi binafsi na Mhe. Waziri tutalitembelea soko, ili kwa pamoja tuweze kuona tunaanza na hatua gani.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Mhe. Waziri wa Fedha kama msimamizi wa shughuli za matumizi ya serikali.

Mimi nitakubaliana na mawazo yake lakini anambie kwanza kikao gani ataleta ripoti hapa isomwe tuisikie sote kama Baraza la Wawakilishi, tuone kasoro zilizojitokeza na hatua gani serikali itachukua na mpaka kulipa madeni ya wale watu wanaodai katika soko lile pale waliofanya kazi. Ikiwa tutakubaliana hayo Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi, tukimaliza tu bajeti hii kama itakuwa ni tarehe 30/06/2014 au tarehe 1/07/2014 nitamuomba Mhe. Waziri wa Uvuvi na wataalamu wake na mimi na wataalamu wangu twende Pemba pamoja na Mwakilishi.

Hilo tutalifanya kwa udhati, kwa nguvu zetu zote pamoja na Mwakilishi twende Pemba tutembelee *site* ile na nitaomba vile vile Mkandarasi na yeye awepo *on the site* tuweze kuona nini hasa tatizo.

Tutaangalia michoro yote, tutaangalia pesa zote zilizotolewa, tutasoma tatizo ni nini? Mafanikio yako wapi, na nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kikao chetu cha Baraza cha mwezi wa Oktoba, tutaleta ripoti hiyo na tutaisoma hapa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Umesema nadhani tuendelee, umesema tayari tuendelee…

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee lakini namuomba Mhe. Waziri hiyo siku tutakayokwenda pamoja na masheha wa shehia zote mbili wawepo.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipochangia nilionesha wasi wasi wangu juu ya chumvi, na mwaka jana nilichangia, wakati nachangia nilichangia katika Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikuwa ishapita, lakini katika majumuisho Naibu Waziri wa Kilimo alijibu kama chumvi haiko katika

wizara yao, na katika kuzuia fungu Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi alisema kama chumvi iko katika wizara yake.

Vile vile na hasa Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo alisema kama nadhani Mhe. Salma Mohammed Ali anafikiria kama bado Wizara ya Kilimo iko pamoja na mifugo na uvuvi. Kwa hiyo, chumvi iko uvuvi; mimi ninaloomba Mhe. Mwenyekiti najua kilimo haijafika lakini nina wasi wasi mchezo huu kujakuwa ule ule kama wa mwaka jana. Leo tunapitisha bajeti ya Wizara ya Mifugo wameshatoa kama chumvi si yao, na kesho tukija tukipitisha ya Kilimo atakuja kusema chumvi ni ya Mifugo.

Kwa hiyo, naomba nipate kauli hapa, kwanza Mhe. Waziri wa Mifugo ikiwa chumvi si yake afute ile kauli yake ya kuwa chumvi ni yake, na ikiwa Waziri wa Kilimo chumvi ni yake akubali hapa kama chumvi ni yake kabla hatujafika kesho akaja akanirusha kesho. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.
Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla Mhe. Waziri hajajibu nakumbuka mchango huu nafikiri Mhe. Salma Mohammed Ali alitoa mpaka shairi chumvi imekosa nini? Bahati nzuri mimi kumbukumbu nakuwa ninazo kama *hansard* vile, kwa hiyo bado kumbe makosa yale yapo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kidogo. Kwa kweli nakumbuka suala hili lilikuja mwaka jana kweli, na tulitoa kauli kwamba suala la chumvi haliko katika wizara yetu. Ingawaje Mhe. Naibu Waziri alizungumzia kwamba tutalichukua kwa sababu ni *collective responsibility*, kwa sababu hili suala lilileta utata toka wizara hii ilikuwa ni moja yaani Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Kwa hivyo, zilipogaiwa hizi wizara kwa kweli likawa lina-*hang* suala la chumvi, sasa ikaonekana madamu hii inatoka baharini basi hii lazima itakuwa ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini sio ukweli halisi; ukweli ni kwamba mazao ya baharini yenye uhai chumvi ni maliasili, unapozungumza mazao ya baharini ni vile viumbe ambavyo vyenye uhai, chumvi haina uhai, mwani una uhai, kaa na vyengine vyote vina uhai lakini chumvi haina uhai.

Kwa hivyo, hili ni suala ambalo liko chini ya wizara nyengine ama Wizara ya Kilimo au Wizara ya Biashara, lakini kwa Wizara ya Uvuvi haliko. Sisi tulilichukua kwa sababu ni *collective responsibility,* tukasema *okay* tutalichukua, tutazungumza na Wizara ya Kilimo, tutazungumza na Wizara ya Biashara ili tuone liko wapi hasa hili suala kwani limekuwa kama mtoto yatima kwa kweli, lakini kwa Wizara ya Uvuvi halipo kwa sababu sisi ni mazao ya baharini kwa viumbe vyenye uhai. Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, suala hili lilikuwepo tokea mwaka jana Waziri wa Mifugo ameshanijibu kama haiko kwake, Waziri wa Kilimo yupo, sikubali kuambiwa kama waende wakashauriane. Halafu anijibu ni tokea mwaka jana na leo tuna bajeti ya Wizara ya Kilimo, kwa hiyo nataka nipate jawabu leo ili nijue kuandaa mchango wangu niandae vipi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, chumvi ina bahati ya aina yake, mara nyingi haitajwitajwi lakini karamu hailiki bila ya chumvi wala haiongoki. Sasa Mhe. Salma anataka kujua chumvi kwao wapi? Kama ikiwa suala la kwenye mifugo chumvi haiko basi mimi nitamshauri Waziri wa Kilimo chumvi iingie kwenye wizara yake na Mhe. Salma Mohammed aje alete mchango wake kwenye Wizara ya Kilimo juu ya suala la chumvi, msaada gani unaohitajika kwa watu wanaotengeneza chumvi nitaupokea na utafika kwenye Wizara ya Kilimo bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki ning'ang'ane hapa lakini kitu cha kuambiwa mtu anakwenda kushauriwa asipokubali je mimi nifanye nini? Kwa sababu kumshauri mtu anaweza akakubali au anaweza akakataa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, asiwe na wasiwasi wa kukubali au kukataa, chumvi kama kwenye uvuvi siko itashughulikiwa kwenye Idara ya Maliasili kwenye hii Wizara ya Kilimo. Yeye alete mchango wake usikie msaada gani unaotakiwa kwa ajili ya watengeneza chumvi. Wizara ya Kilimo kwa niaba ya serikali itatoa msaada wowote unaotakiwa kwa ajili ya watengeneza chumvi, hakuna wasiwasi wowote.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru najua Mhe. Waziri katumia mbinu lakini kakubali kama iko katika wizara yake, kwa hiyo tuendelee.

Kifungu 0010 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Pemba	30,000,000
Kifungu 0011 Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Pemba	792,000,000
Kifungu 0012 Idara ya Mazao Baharini; Pemba	

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia jana katika sehemu hii nilisema aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Said Ali Mbarouk alitembelea katika Jimbo la Kojani siku ya tarehe 10/02/2012 na akawakuta watu wa kikundi wa Kidunda wanafanya shughuli zao za ufugaji, hayo mambo ya chumvi na aliwataka watu wale wafanye makisio kwani ile shughuli aliona kama inakwenda vizuri ili wapate kutengeneza bwawa jengine.

Kwa hivyo, wana kikundi hao walifanya makisio na gharama yake ni shilingi milioni 1,894,000 na wakapeleka pale walipoelekezwa, na mpaka leo hawajapata chochote. Naomba kwa sababu aliyeondoka ni Waziri tu lakini wizara iko pale pale, nipate majibu sahihi kutokana na kusaidia kikundi hiki ili iweze kufanya shughuli zake.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Mjumbe kuhusiana na suala la Kiungoni kwamba waliahidiwa kusaidiwa, kwa kweli walisaidiwa kwa sababu Waziri aliyepita Mhe. Said Ali Mbarouk alijenga bwawa la mfano pale; kubwa tu ambalo halipungui gharama ya shilingi milioni 15.

Hata hivyo na mimi mwenyewe binafsi niliwahi kutembelea ili kuona changamoto zilizopo na tukaahidi kwamba tutashirikiana na kuzitatua tukiangalia bajeti yetu na hali inaporuhusu tutawasaidia kama sehemu nyengine ambazo tumezisaidia. Kwa hivyo, mimi ninachomuomba Mhe. Mjumbe najua tunataka kuvisaidia vikundi vingi, tunataka kusaidia miradi mingi lakini hali ya bajeti ndio kama unavyoiona.

Kwa hivyo, mimi nakuomba tujenge subra, kwa sababu nimekusudia kwamba tukimaliza bajeti nitembelee miradi yote Unguja na Pemba, kwa sababu ni zamani kidogo ili kuona wapi tumekwama na nini kinahitajika kusaidiwa ili kusaidiana. Kwa hivyo, bado tuna nia ile ile ya kusaidia, kama tulivyojenga bwawa basi na mengine tutasaidia. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri bado sijaridhika nayo kwa sababu za msingi yeye anasema zaidi ya shilingi milioni kumi na tano (15,000,000) alisaidia lakini mimi hili jambo silisemi kwa utashi nalisema kwa uhakika, kama ile ahadi iliyowekwa bado haijatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri anapoahidi sehemu hiyo ni serikali, kwa sababu waziri anafanya mambo ya serikali. Sasa nataka kujua kiasi hiki cha fedha ni lini wana kikundi hawa watapata ili kuweza kufanya shughuli zao wakati mmetoa ahadi? Hapo ndio nilipokuwa nataka kujua, mimi ukishanambia hakuna matatizo tutaendelea, lakini kama ulitembelea ndio tukayajua haya yaliyopo sasa ukinambia utatembelea tena hii haiingii akilini, naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Mwakilishi ni sahihi lakini nadhani akumbuke vizuri, nilikwenda mimi, yeye, Mhe. Farida na baadhi ya masheha na Wawakilishi. Pale pana mabwawa mengi watu wanafuga samaki yanafika mabwawa manane, naamini sasa yameendelea zaidi.

Tulipokuwa tunazungumza ahadi niliyotoa kwamba katika eneo hili tutajenga bwawa moja kama iwe ni skuli ya mfano kwa mabwawa ya hapa. Kwa hiyo, serikali ilichofanya ahadi ile imetimizwa kweli, tuliahidi shilingi milioni moja na kidogo, lakini kwa uzito wa shughuli yenyewe tulizidisha mara kumi ya kile ambacho tuliahidi. Mhe. Mwenyekiti, yupo bwana mmoja pale ana bwawa anaitwa bwana Ali Omar nakumbuka jina lake mpaka leo.

Kwa hivyo ana eneo zuri wamejenga Waheshimiwa hawa bwawa zuri hata mimi siku moja katika wizara hii aliniita akaenda akanigaia samaki wakubwa sana. Sasa naomba Mwakilishi akubali kwamba ahadi ya serikali ilitekelezwa kajengewa bwawa, kapewa na *pump* ya kutolea maji ili aweze kufanya shughuli zake ili iwe kama ni mfano na watu wengine waige katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana kwamba serikali haiwezi kumjengea kila mtu bwawa isipokuwa katika eneo pakiwa na mfugaji wa samaki mmoja mzuri na mwenye bwawa zuri serikali inafanya hivyo, hata Donge kwa Mheshimiwa kumefanyika na maeneo mengine, lakini si kwa kila mtu, ni kwa eneo moja kuwa na bwawa la mfano ili wananchi wengine waige mfano ule. Kwa hivyo, naona akubali kwamba serikali imetimiza wajibu wake kuliko ule ambao uliahidiwa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Waziri nadhani umemtaja shahidi Mhe. Farida Amour Mohammed wakati tulipokuwa katika ziara hiyo uliyotualika sisi katika Jimbo la Kojani ambaye ndiye Mwakilishi wao. Mhe. Mwenyekiti, hiki kikundi nimekitaja hapa na mpaka jana bado hawajapatiwa huo msaada mliokuwa mnataka kusaidia, hawa ndio uliowaahidi, sasa kama ulitoa kwengine umekwenda kinyume na utaratibu, kwa sababu hawa umewapa ahadi na kama umewapa ahadi wajibu wako uwatekelezee ahadi yao, sasa kama umekwenda kufanya kwengine umefanya vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuomba kama kuna ukweli ushawasaidia tunawataka wanakikundi hapa mimi na wewe au Waziri anayehusika twende tukaangalie kama kweli wamesaidiwa hawa, usitake kunivunga itakuwa haipendezi kabisa na itakuwa nawadanganya wananchi. Naomba jawabu Mheshimiwa bado sijaridhika na hii jawabu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, acha nichukue ushauri wake na nitafanya hivyo kushirikiana pamoja na yeye mwenyewe binafsi, kwa hiyo sina pingamizi kwa kweli. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mheshimiwa nakubaliana na kauli ya Mhe. Waziri lakini nataka anipe ahadi lini mimi na yeye tutakutana ili tupate huo ushauri wa kwenda kulitekeleza hilo, akishaniambia hapo hakuna matatizo. Aniahidi lini mimi na yeye tukutane.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nafikiri itakuwa muafaka katika sikukuu ya sita.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Baada ya sikukuu ya sita, nitakutafuta. Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Spika: Unajua Mhe. Hassan baada ya sikukuu ya sita mkienda pale mnaweza hata mkakaanga samaki pale pale mkatafuna.

Kifungu 0012 Idara ya Mazao Baharini; Pemba	40,425,000
Kifungu 0013 Idara ya Uzalishaji Wanyama; Pemba	63,960,000
Kifungu 0014 Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo; Pemba	50,700,000
Kifungu 0015 Idara ya Maendeleo	

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, lile suala langu la mwanzo pahali pake ni hapa kutokana na suala liloulizwa jana lilikuwa la Mhe. Jaku Hashim Ayoub sasa naona Mhe. Naibu Waziri alilijibu lakini amelijibu kinyumenyume, kwa sababu liliulizwa suala la uvuvi na ni suala langu la nyongeza nikalipeleka kule kule kwenye uvuvi, lakini anaponijibu yeye kanambia kwamba wamesaidia vikundi vya mwani Tumbe vingi, sikatai suala hilo kuwa wamesaidia vikundi vya mwani, lakini nililolizungumza mimi ni kusaidiwa hawa wavuvi wa pale Tumbe, kama alivyosema Mhe. Said mtaalamu hapo kwamba pana wavuvi wengi, bahari yao ni nzuri na wao wanataka kusaidiwa tangu mwaka 2007 wanasema wanasaidia vikundi vingi.

Sasa naomba Mhe. Waziri aniambie kama wanawasaidia basi anitajie ni vikundi gani, kama hajawasaidia basi aniambie tu siku gani tutakwenda tukawaone wavuvi wa pale ili tuwahamasishe pengine na wao wana changamoto zao watatueleza. Naomba Mhe. Waziri anijibu hivyo tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mhe. Bikame kwa sababu suala la nyongeza au la maandishi lina taratibu zake basi asiwe na wasiwasi tutamjibu. Na vile vile kama nimetoa hii habari ya mazao ya baharini waliosaidia mwani, boti na kila kitu basi nimewaahidi kwamba tukimaliza Baraza hili twende tuwaone wavuvi wake wa Tumbe ili tuone kupitia mradi wetu wa *Sole Fish* tunaweza tukawasaidia vile vile.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Naibu Waziri naomba tuendelee.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru tena kwa mara nyengine. Nilipokuwa nikichangia sehemu hii huyo huyo aliyekuwa Waziri wa Uvuvi Mhe. Said Ali Mbarouk katika ziara hiyo hiyo ya Jimbo la Kojani kule Kisiwani Kojani hasa, alitoa ahadi kutokana na jinsi alivyoona vile ilivyo akasema nataka niwapatie vijana wawili wa *form IV* kwenda kusoma Chuo cha Mbegani cha Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, tulifanya hivyo na majina jana niliyataja na leo mkitaka tena nitawatajia Mhe. Waziri alitoa ahadi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nimuulize Mheshimiwa vile vile tulifanya kikao ndani ya Wizara ya Uvuvi wakatwambia vijana hawa kama watastahamili mwaka huu watakwenda wote wawili, lakini Mheshimiwa

alipokuwa akitoa jawabu lake pale ananiambia kwamba ni mtu mmoja tu atakayemchukua. Naomba maelezo zaidi ya ziada.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru ni kweli maneno aliyozungumza Mhe. Mjumbe tuliahidi hivyo, lakini kwa bajeti ya mwaka huu tumesema kwamba tutamchukua mtu mmoja, tunawachukua kwa awamu na bajeti nyengine tutamchukua mwengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe namuomba akubali hili na aridhike kwamba angalau tunamchukua huyu mmoja kwa awamu hii na awamu inayokuja *inshaallah* tutamchukua mwengine. Sasa watachagua wenyewe kama watamchukua mwanamke au mwanamme, hiyo ni kazi yao, na tutakaa tushirikiane ili tuone itakavyokuwa, lakini ajue kwamba mwanafunzi mmoja tunamchukua. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina matatizo kama kakubali, naomba mara nyengine na huyu mwengine baadae atamchukua akamsomeshe, basi sina matatizo, lakini kama atachagua wanawake roho zao ndogo achukuliwe mwanamke aende akasome yeye kwanza.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Sawa nimekubali.

Kifungu 0015 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba-	46,500,000
Kifungu 0016 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja-	504,984,000
Kifungu 0201	

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Mhe. Mweyekiti, jana nilipokuwa nikichangia, niliomba ufafanuzi katika eneo la muhtasari wa mapato na matuzi, na nikatoa maelekezo katika ukurasa wa 44, lakini nikajumuisha na jadweli katika ukurasa wa 49. Nilikuwa nataka Mhe. Waziri, anisaidie tu je, hii ni *typing error* au ndio uhalisia kwamba tafauti ya mahesabu baina ya ukurasa wa 44 na 49. Naomba majibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, umeipata hoja? Mhe. Mjumbe, hebu ifafanue vizuri hoja.

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa upande wa mishahara imetengewa shilingi 2,045,000,000; lakini ukiangalia katika jadweli kuna shilingi 2,326,000,000. Pia, katika eneo la *OC* katika hotuba yake Mhe. Waziri, alisema kuna shilingi 463,918,000; katika jadweli kuna shilingi 426,000,000. Sasa nilitaka kufahamu kwamba ni *typing error* au ndio hasa uhalisia.

Mhe Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri inaweza ikawa ni *typing error*, lakini hata hivyo tutaisahihisha vile vile. Hiyo ichukuliwe kama ni *typing error*.

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kama ni *typing error* wapi tutatakiwa ku-*base*, katika jadweli au katika hotuba yake. Naomba tuweke *Hansard* sawa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, tuende kwenye kitabu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, usahihi uko kwenye kitabu sawa?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ndio.

Kifungu 0201 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti-	162,728,000
Kifungu 0401 Idara ya Uendeshaji na Utumishi-	1,047,681,000
Kifungu 0601 Idara ya Huduma za Utibabu na Mifugo-	703,984,000
Kifungu 0701 Idara ya Mazao ya Baharini Unguja-	203,301,000
Kifungu 0801 Idara ya Uzalishaji wa Wanyama Unguja-	604,237,000
Jumla ya Fungu:	**4,250,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 22 WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0016 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja-	6,261,600,000
Kifungu 0201 Idara ya Mipango-	

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri, anisaidie ufafanuzi juu ya suala la mradi ambao ni wa Mjimbini. Mhe. Waziri, alipokuja ameendelea kutoa maelekezo yale ambayo mimi nilikuwa nimeyatoa, nilichotaka kukifahamu mimi. Je, fedha hizi za mradi zinapatikana wapi? Kwa sababu katika orodha ya fedha ambazo zimo humu kwa wahisani wa maendeleo, mimi sikuziona hizo pesa, sasa nilitaka anisaidie fedha hizi wanazo na ni kima gani? Ndio suala langu lilipokuwepo hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nimuombe radhi sana Mhe. Mwakilishi, kwa kuwa labda hakufahamu vizuri, lakini niseme tu kwamba pesa hizi tunazo tangu mwaka jana na ziko katika *pipeline*, sasa hivi tayari tumeshatia mkataba na huyu mtu na soko linaanza mara moja.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 0016 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja-	6,261,600,000
Kifungu 0201 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti-	80,000,000
Kifungu 0601 Idara ya Huduma za Utibabu-	347,873,000
Kifungu 0701 Idara ya Mazao ya Baharini-	561,080,000
Kifungu 0801 Idara ya Uzalishaji wa Wanyama-	90,000,000
Jumla ya Fungu:	**7,340,553,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha za wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri muda uliopo sina hakika kama unamaliza, unatosha. Kwa hiyo, tunaendelea. Mhe. Waziri, ameahidi muda unamtosha, naomba nimkaribishe Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha
2014/2015 - Wizara ya Kilimo na Maliasili

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu likae kama Kamati kwa ajili ya kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, napenda kutoa taarifa kwamba nitakachokiwasilisha hapa ni muhutasari wa hotuba ambapo napenda kuomba Baraza lako tukufu kwamba, kile kitabu chenyewe cha hotuba kiwekwe kwenye *Hansard* ili iende pamoja na uwasilishaji wangu.

Mhe. Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambao wengi wao ni wakulima.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu na kuiwezesha

kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambapo yalifana na kudhihirisha kwamba sekta ya kilimo imepiga hatua katika kuleta maendeleo katika nchi yetu kama ilivyokuwa kauli mbiu ya maadhimisho hayo, "Tudumishe Amani na Umoja, tulete maendeleo – Mapinduzi Daima".

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, katika kuendeleza kwa vitendo Mapinduzi ya Kilimo yenye dhamira ya kuwaendeleza wakulima na kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, nawapongeza viongozi wakuu wa Kitaifa Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad (Makamu wa Kwanza wa Rais) na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi (Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar) kwa juhudi zao za kuhamasisha na kutoa miongozo katika kuendeleza sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo sambamba na kumpongeza Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, kwa miongozo na ushauri waliyoipa Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya wizara ya mwaka 2013/2014. Pia, tunaishukuru Kamati kwa maelekezo yao waliyotupa katika maandalizi ya bajeti ya wizara ya mwaka 2014/2015. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii .

Mhe. Spika, naomba pia nikupongeze wewe binafsi kwa umahiri wako katika kuliongoza Baraza lako tukufu kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wakulima na wananchi wote kwa mashirikiano yao katika kuendeleza kilimo na hifadhi ya maliasili hapa Zanzibar. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Jang'ombe kwa kuendelea kumpa mashirikiano Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili na kuwa na imani naye katika kusimamia na kuleta maendeleo ya jimbo hilo. Anawaahidi kwamba ataendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote kadiri atakavyoweza.

UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA

Mhe. Spika, Sekta ya Kilimo bado inaendelea kuwa ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar, ambapo inatoa mchango mkubwa katika kujikimu kimaisha na kupatikana kwa chakula na lishe bora. Ukuaji wa sekta hii katika Pato la Taifa kwa mwaka 2013 umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 31.0 ikilinganishwa na asilimia 30.2 ya mwaka 2012. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa mchango wa sekta ndogo ya mazao kutoka asilimia 19.4 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 19.7 mwaka 2013. Aidha, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hii kwa kuwapatia ajira na mapato.

Mhe. Spika, mwaka 2013 ukuaji wa Sekta ya Kilimo umeongezeka kufikia wastani wa asilimia 3.6 kutoka wastani wa asilimia 2.0 ya mwaka 2012. Miongoni mwa sababu zilizochangia ongezeko hilo ni ukuaji wa sekta ndogo ya mazao iliyofikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.7 mwaka 2012. Sababu nyengine ni hali nzuri ya hewa na muamko ambao wameuonesha wakulima kuhusiana na matumizi ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea na madawa. Jambo jengine lililochangia ongezeko hili ni kuimarika kwa uzalishaji wa zao la karafuu.

HALI YA UZALISHAJI

Mhe. Spika, msimu wa kilimo wa mwaka 2013/2014 unaonesha kuwepo kwa ongezeko la mavuno kwa baadhi ya mazao yakiwemo ya karafuu kutoka tani 4,000 mwaka 2012/2013 hadi tani 5,280 mwaka 2013/2014 na viazi vitamu kutoka tani 31,767.3 mwaka 2012 hadi tani 53,656.6 mwaka 2013. Mavuno ya zao la mpunga yalikuwa tani 6,372.1 mwaka 2012, hali hii ilitokana na ukame katika kipindi kilichoainishwa, kwa mwaka 2013 mavuno yalikuwa tani 33,655. *(Kiambatanisho Nam. 1).*

Mhe. Spika, takwimu pia zinatuonesha kuwepo kwa ushukaji kwa baadhi ya mazao ya kilimo ikilinganishwa na mwaka 2012/2013. Zao la muhogo limeshuka kutoka tani 192,072.68 mwaka 2012 hadi tani 164,332.2, ndizi kutoka tani 97,934.5 mwaka 2012 hadi tani 68,620, viazi vikuu kutoka tani 3,081.7 hadi tani 2,351.5 na mahindi kutoka tani 1,496 hadi tani 1,419 mwaka 2013.

Mhe. Spika, ingawa sekta ya kilimo inaendelea kukua, hata hivyo ukuaji huo umekua ni mdogo kufikia kiwango kilichowekwa katika MKUZA II cha asilimia sita kwa mwaka. Miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta

hii ni pamoja na uwezo mdogo wa wizara wa kutoa huduma na pembejeo kwa wakulima kutokana na kuingiziwa fedha kwa mujibu wa bajeti na kwa wakwati. Changamoto nyengine ni pamoja na utegemezi mkubwa wa kilimo cha kutegemea mvua, mabadiliko ya hali ya hewa, miripuko ya maradhi, wadudu waharibifu wa mazao na upungufu wa rutuba katika maeneo ya kilimo na uwekezaji mdogo wa sekta binafsi.

KILIMO CHA MAWENI:

Mhe. Spika, pamoja na jitihada nyingi tunazozichukua bado kilimo cha maweni hakijapiga hatua ya kuridhisha. Wakulima wengi wa ukanda huu wanauzoefu mkubwa katika uzalishaji wa mazao ya mbaazi, mtama, uwele, viazi vikuu, ndimu na pilipili hoho, kama mazao ya chakula na biashara. Wizara itaendeleza utafiti wa kilimo cha maweni kwa kushajihisha kilimo mseto na kuhamasisha utunzaji wa mazingira. Aidha, juhudi za kuwaendeleza wakulima wa maweni kwa kuwapatia kazi mbadala za kiuchumi hasa ufugaji nyuki zitaendelea zaidi.

Mhe. Spika, kilimo cha mboga kina umuhimu mkubwa kwa wazalishaji wadogo wa Zanzibar hasa kutokana na tija ya haraka inayopatikana pamoja na ukuwaji wa soko la utalii. Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa kilimo hicho inaendeleza mashirikiano na sekta binafsi zikiwemo Taasisi ya Wazalishaji wa mazao ya mboga, matunda na maua - *Tanzania Horticultural Association* (*TAHA*) na Kampuni ya *Zanzibar Agricultural Investment and Development (ZAIDI*) ambayo inajihusisha na utoaji wa taaluma na vifaa vya umwagiliaji maji kwa njia ya matone.

Mhe. Spika, kwa upande wa Maliasili, wizara inaendelea kushajiisha jamii katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili katika maeneo ya hifadhi na ya wananchi. Pia, inathamini mchango mkubwa unaotolewa na jumuiya hizo kwa kuhifadhi maliasili na kubuni mbinu mbadala za kupunguza uharibifu wa rasilmali za misitu.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeweza kukamilisha sensa ya miti iliyojumuisha miti ya mikarafuu ambayo imetuwezesha kupata takwimu sahihi za miti iliyopo. Vile vile, tutaweza kupanga mipango sahihi ya maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali zilizomo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, serikali kupitia wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2010 – 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Malengo ya Milenia (*MDGs*), Mipango na Mikakati ya Kisekta, pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (*ATI*).

Mhe. Spika, muelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

- Kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji, matumizi ya zana za kisasa na teknolojia za uzalishaji na taaluma juu ya uhifadhi wa mpunga;

- Kuendelea kuhifadhi rasilmali za misitu na kuongeza uzalishaji wa matunda, karafuu, viungo na asali kwa kutoa elimu kwa wakulima na uoteshaji wa miche bora;

- Kufanya tafiti ili kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo na kutoa ushauri wa kitaalamu na usambazaji wa mizinga na vifaa bora vya uzalishaji asali;

- Kuimarisha utoaji wa huduma za matrekta na zana nyengine za kilimo, elimu kwa wakulima na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati zikiwemo, mbegu bora, mbolea, dawa za kuzuia magugu na wadudu waharibifu;

- Kushajihisha uibuaji wa miradi ya kuongeza kipato katika Sekta ya Misitu na Maliasili ikiwemo uzalishaji wa asali na utalii wa kimaumbile *(eco-tourism)* katika maeneo ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa;

- Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma wakulima na wafanyakazi katika ngazi tofauti;

- Kuanzisha na kuendeleza hifadhi ya chakula ya Zanzibar;

- Kuendelea na mapitio ya Sera, Sheria na Mpango ili uendane na mabadiliko ya kiuchumi na kimazingira;

- Kuhakiki na kusimamia upatikanaji wa hati miliki za mali za serikali zilizopo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2013/2014

MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 748,000,000. Hadi kufikia mwezi wa Mei 31, 2014 wizara imekusanya Shilingi 856,180,640 sawa na asilimia 114 ya makadirio ya lengo. *(Kiambatanisho Nam. 2).*

MATUMIZI YA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 31,394,697,558.Kwa kazi za kawaida iliidhinishiwa Shilingi 13,642,699,558 (Mishahara Shilingi 7,903,699,558, Matumizi mengineyo Shilingi 5,239,000,000 na Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani Shilingi 500,000,000). Hadi kufikia Mei 2014, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni Shilingi 9,554,053,008 zinazojumuisha Mishahara Shilingi 7,170,292,608 sawa na asilimia 91. Matumizi mengineyo Tsh. 2,094,360,400 sawa na asilimia 40, pamoja na Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani Tshs. 289,400,000 sawa na asilimia 58. *(Kiambatanisho Nam. 3a na 3b).*

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi za maendeleo, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 17,751,998,000. (SMZ Tsh. 1,560,000,000 na washirika wa maendeleo Tsh. 16,191,998,000). Hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Tsh. 447,809,815, sawa na asilimia 29 ya fedha zilizoidhinishwa na jumla ya Tsh. 1,529,959,074 sawa na asilimia 9.4 ya lengo kutoka kwa washirika wa maendeleo. *(Kiambatanisho Nam. 4a na 4b).*

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inakadiriwa kukusanya mapato ya Tsh. 845,000,000 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 *(Kiambatanisho Nam. 2).* Aidha, Wizara pia inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 23,369,002,000. Kati ya fedha hizo, Tsh. 13,758,000,000 ni matumizi ya kazi za kawaida zinazojumuisha Tsh. 9,034,000,000 za mishahara, Tsh. 4,297,000,000 kwa matumizi mengineyo na Tsh.427,000,000 kwa ajili ya ruzuku ya Chuo cha Kilimo Kizimbani. Aidha, Wizara imetengewa Tsh. 9,611,002,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi 10 ya maendeleo (kati ya hizo Tsh. 1,500,000,000 ni mchango wa SMZ na Tsh. 8,111,002,000 ni mchango wa washirika wa maendeleo *(Kiambatanisho Nam. 3a, 4a na 4b).*

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepata mafanikio yafuatayo:-

- Jumla ya miche 941,176 ya mikarafuu (Unguja 309,640 na Pemba 631,536) sawa na asilimia 94 ya lengo imeoteshwa na kuisambaza kwa wakulima bila ya malipo, pamoja na kuwapatia wakulima mafunzo ya mbinu bora za uoteshaji wa miche ya mikarafuu, utunzaji na uoteshaji kwa wakulima 300 (Unguja 100 na Pemba 200). Aidha, skuli 21 za wakulima wa karafuu (Unguja 8 na Pemba 13) zilianzishwa na zimepatiwa mafunzo;

- Wizara imekamilisha sensa ya miti ambayo imetusaidia katika kukamilisha Sera, Sheria ya Misitu na Mpango wa Muda Mrefu wa Usimamizi wa Rasilmali za Misitu. Aidha, matokeo ya sensa hii yatasaidia taasisi nyengine katika kupanga mipango ya maendeleo;

- Wizara ya Kilimo na Maliasili imeongeza zana za kisasa kwa lengo la kuimarisha ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua. Jumla ya matrekta 20 mapya yamenunuliwa na kuweza kusaidia kazi za uzalishaji wa mpunga;

- Wizara kwa kushirikiana na wajasiriamali imeweza kuwasaidia wakulima katika bidhaa

wanazozalisha kwa kuziweka kwenye vifungashio na hivyo kuimarisha ubora wa bidhaa hizo na kujiongezea kipato;

- Wizara imeongeza kipato cha wanajamii kwa kuwashirikisha katika miradi ya utalii wa kimaumbile. Mfano wanajamii wa hifadhi ya msitu wa Mtende wameweza kuuza paa nunga mmoja dume aliyezeeka kwa shilingi 7,840,000. Vile vile, wanajamii hao wameweza kuuza wanyama wengine wanane wadogo wakiwemo kigombo na kima mweusi kwa thamani ya shilingi 480,000 kila mmoja;

- Kutokana na matokeo ya tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, imegundulika kwamba uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua unaweza kuongezeka kutoka tani moja hadi tani tano kwa hekta, viazi vitamu kutoka tani sita hadi 15 kwa hekta, iwapo kama mkulima atafuata teknolojia zilizotumika katika tafiti hizo;

- Wizara ya Kilimo na Maliasili imeongeza idadi ya mabibi na mabwana shamba kwa kuajiri vijana 45 na kusomesha wanafunzi 197 kati ya hao, wanafunzi 24 wa Diploma wa awamu ya kwanza wamemaliza katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Spika, utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara na taasisi zake kwa mwaka 2013/2014, pamoja na malengo ya mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, majukumu ya Idara hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti. Idara pia inaratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa 2013/2014 ililenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuzipitia Sera za Misitu, Kilimo, Sheria ya Uhifadhi wa Mimea pamoja na kutayarisha Sheria mpya ya mbegu;

- Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya kisekta na Wizara (*M & E*); ikiwemo mawasiliano na utoaji taarifa kwa njia ya tovuti (*www.kilimoznz.or.tz*);

- Kutoa nakala 2,000 za Jarida la Mkulima na kuzisambaza kwa wadau wote wanaohusika; wakulima matayarisho ya vipindi 10 vya *TV.* na Redio juu ya elimu kwa wakulima (mpunga, matunda, karafuu na mbogamboga) na kuvirusha hewani;

- Kutayarisha makala 15 na vipeperushi 1,000 kwa ajili ya wakulima ili kupata taarifa muhimu za kilimo cha kisasa, taarifa za masoko na pembejeo;

- Kukusanya taarifa na takwimu muhimu za kijamii na kiuchumi katika sekta ya kilimo, ikiwemo uzalishaji na masoko ya mazao ya chakula biashara, pamoja na kukamilisha mfumo wa ufuatiliaji, tathmini;

- Kuimarisha mashirikiano kati ya Wizara, taasisi za ndani, za kikanda na nje ya nchi;

- Kuratibu mfumo wa pamoja wa kitaasisi katika Sekta ya Kilimo *(ASP-Z)* pamoja na kushiriki katika vikundi Kazi vya Kitaifa, mikutano na makongamano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

- Kuimarisha tafiti za kijamii, kiuchumi na kisayansi ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo kwa kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya maeneo ya kipaumbele ya utafiti;

- Kuandaa warsha na kutoa Toleo la Nne la Utafiti wa Kilimo *(4th Annual Agricultural Research Meeting);* na

- Kuratibu na kusimamia miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Sheria ya Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea imejadiliwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi. Rasimu ya Sera ya Misitu imekamilika na hivi sasa inajadiliwa na wadau. Mapitio ya Sheria ya Hifadhi na Utibabu wa Mimea imekamilika na hivi sasa inasubiri maoni kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;

- Utayarishaji wa Programu ya Kuendeleza zao la karafuu imekamilika na imeanza kutekelezwa. Pia, Programu ya Mazao ya Matunda na Viungo imekamilika;

- Uingizwaji wa taarifa katika Tovuti *(Website)* ya Wizara ulifanyika kwa lengo la kuelimisha wadau mbali mbali. Aidha, vipindi viwili vya *TV.* na vitano vya redio vimetayarishwa na kurushwa hewani;

- Jumla ya nakala 1000 za Jarida la Mkulima zimechapishwa na kusambazwa kwa wakulima na wadau wengine;

- Wizara imeshiriki katika vikao vya mashirikiano na hivi sasa kuna muelekeo wa utekelezaji miradi ikiwemo ya mboga, *sunflower,* miundombinu ya umwagiliaji maji na mradi wa uzalishaji wa asali;

- Makala kumi zimekusanywa kwa ajili ya utayarishaji wa toleo la tatu la *Agriculture Research Proceedings;*

- Utafiti wa uingizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo umefanyika na kuonesha kwamba ipo haja ya kurekebisha mfumo wa uingizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo; na

- Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa sekta ya kilimo umekamilika na unatarajiwa kuwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo kama ifuatavyo:-

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo–*ASSP. (Kiambatanisho Nam. 5).*

- Programu ya Kutoa Huduma za Mifugo *ASDP-L. (Kiambatanisho Nam. 6).*

- Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Kilimo na kuongeza Thamani ya Mazao *(MIVARF). (Kiambatanisho Nam. 7).*

- Mradi wa Usarifu wa Mazao. *(Kiambatanisho Nam. 8).*

MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuipitia Sera ya Kilimo, kukamilisha Sheria ya Uhifadhi na Utibabu wa Mimea;
- Kutoa nakala 2,000 za Jarida la Mkulima na kuzisambaza kwa wadau wote;
- Kufanya utafiti wa mboga mboga na matunda juu ya mtazamo wa soko la Utalii nchini;
- Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu muhimu za kijamii na kiuchumi katika sekta ya kilimo ikiwemo uzalishaji na masoko ya mazao ya chakula na biashara, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya sekta/Wizara;
- Kuimarisha mashirikiano kati ya Wizara, taasisi za ndani, za kikanda na nje ya nchi pamoja na kushiriki katika vikundi kazi vya Kitaifa, mikutano na makongamano ya Kitaifa, Kikanda na

Kimataifa;

- Kukamilisha mapitio ya tafiti zilizowasilishwa pamoja na uchapishaji wa Toleo la Tatu la Utafiti wa Kilimo *(3rd Annual Agricultural Research Proceeding);* na

- Kuratibu na kusimamia miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara iliombewa Tsh. 470,545,700 hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 338,993,537 sawa na asilimia 72 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya Tsh. 377,129,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, Idara inasimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea na uhakiki wa mali za Serikali zilizo katika Wizara na kuzipatia hati miliki;

- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 15 wapya na 106 wanaoendelea;

- Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;

- Kuratibu utaratibu wa manunuzi ya Wizara;

- Kuratibu ukusanyaji wa mapato ambayo yanakadiriwa kuwa ni Tsh. 748,000,000.

- Kuratibu maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa upande wa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Kupimwa na kupatiwa hatimiliki kwa majengo ya Ofisi Kuu za Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, Ofisi za Utibabu wa Mimea zilizopo Mwanakwerekwe, Nyumba iliyopo *Beit-el-Ras* na bonde la mpunga la Kibonde Mzungu. Aidha, bonde la mpunga la Cheju limo katika hatua za mwisho za upimaji;

- Jumla ya wafanyakazi 62 wa Wizara ya Kilimo na Maliasili wanaendelea na masomo katika fani tofauti. Aidha, wafanyakazi 67 (wanaume 30 wanawake 37) wameanza masomo kwa mwaka 2013/2014;

- Jumla ya wafanyakazi 22 wamestaafu (15 kwa kutimiza umri, 5 kwa hiari na 2 kwa maradhi);

- Wafanyakazi 15 (wanaume 12 na wanawake 3) wamepatiwa likizo bila malipo;

- Wafanyakazi 485 (wanaume 262 na wanawake 223) wamepatiwa likizo ya kawaida;

- Wizara ilishiriki kikamilifu katika maadhimisho ya kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar;

- Wizara imetayarisha mfumo mpya wa uhakiki wa wafanyakazi *(Database)* kwa Unguja na kupata taarifa sahihi za watumishi;

- Mafunzo ya Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011 ya Utumishi wa Umma kwa wafanyakazi 893 wa Wizara ya Kilimo na Maliasili yametolewa;

- Mafunzo kwa Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manunuzi hayakufanyika;

- Jumla ya mapato Tsh. 802,385,890 yamekusanywa sawa na asilimia 107 kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato ya Kilimo na Maliasili; na

- Jumla ya wafanyakazi 60 wakiwemo mabwana/mabibishamba 45 na 15 kada nyenginezo wameajiriwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 20 Unguja na Pemba;

- Kuhakiki mali za serikali zilizo chini ya Wizara ya Kilimo na kuzipatia hatimiliki;

- Kuhakiki wafanyakazi wa Wizara Pemba kwa kutumia mfumo mpya *Database*;

- Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri;

- Kuratibu ukusanyaji wa mapato yanayokadiriwa Tsh. 845,000,000; na

- Kutayarisha na kutekeleza mpango wa manunuzi wa Wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara iliombewa Tsh. 1,261,892,700 hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh 904,7158,308 sawa na asilimia 72 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya Tsh. 1,543,027,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA KILIMO

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima, uhifadhi na ukaguzi wa mazao na kutoa mafunzo kwa wazalishaji.

MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kusimamia ukulima wa mpunga ekari 35,000 kwa msimu 2013/2014 (Unguja ekari 15,000 na Pemba 20,000);

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabibi/mabwana shamba 140 (90 Unguja na 50 Pemba) juu ya mbinu shirikishi za elimu kwa wakulima;

- Kununua seti mbili (seti moja Pemba na seti moja Unguja) za ng'ombe wa kulimia kwa ajili ya mafunzo ya ukulima kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe pamoja na kutoa mafunzo kwa wakulima 40 (20 Pemba na 20 Unguja);

- Kuzalisha tani 5 za mbegu ya mahindi, tani 2 za mbegu ya mtama katika vituo vya Idara vya kuzalisha mbegu na tani 300 za mbegu ya mpunga kupitia kwa wakulima wa mikataba;

- Kununua na kusambaza tani 1,300 za mbolea (*TSP* tani 300 na *UREA* tani 1000), lita 30,000 za dawa ya magugu na tani 300 za mbegu ya mpunga kutoka Tanzania Bara;

- Kuzalisha mbegu ya mpunga aina ya *NERICA* tani 20 katika vituo vya uzalishaji mbegu Bambi na kupitia mikataba na wakulima;

- Kutengeneza matrekta 37 (13 Pemba 24 Unguja), kutoa mafunzo kwa mafundi na madereva 60 wa matrekta na kutoa huduma za matrekta kwa wakulima kwa msimu wa mpunga wa mwaka

2013/2014;

- Kuendelea na kazi za ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima juu ya mbinu bora za kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea na uhifadhi wa mazao; na

- Kuendelea na kazi ya kusambaza na kubadilisha dawa katika mitego ya kunasia nzi waharibifu wa matunda;

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:-

- Jumla ya ekari 30,444 za mpunga zililimwa Unguja 12,548 na Pemba 17,896 kwa msimu wa 2013/2014;

- Tani 40 za mbegu ya mpunga aina ya *NERICA* zimevunwa;

- Tani 376 za mbegu ya mpunga zimesambazwa kwa wakulima, kati ya mbegu hizo tani 150 zilinunuliwa kutoka Tanzania Bara na tani 226 zimenunuliwa na Wizara kutoka kwa wakulima wa mikataba;

- Tani 2 za mbegu ya mahindi na mtama kilo 450 zimezalishwa na kuuzwa kwa wakulima;

- Tani 199 za mbolea aina ya *UREA* na tani 150 za *TSP* zilisambazwa kwa wakulima wa mpunga msimu 2013/2014;

- Jumla ya matrekta 37 makongwe (Pemba 13 na 24 Unguja) yalitengenezwa kwa msimu wa 2013/2014. Aidha, matrekta mapya 20 *(NEWHOLLAND 75HP 4WD)*, pamoja na zana zake yalinunuliwa na kugaiwa 10 Unguja na 10 Pemba;

- Mafunzo juu ya udhibiti wa wadudu waharibifu katika mazao ya mboga yalitolewa kwa wakulima 51 (kutoka Kivunge 15, Nyamanzi 15 na 21 kutoka Bambi);

- Mitego 3,400 (Unguja 1,650 na Pemba 1,750) ya kunasia nzi waharibifu wa matunda ilisambazwa katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Wataalamu wawili walipelekwa nchini Kenya kwa mafunzo ya miezi 6 juu ya udhibiti wa nzi waharibifu wa matunda;

- Udhibiti wa viwavijeshi ulifanyika kwa kusambaza lita 100 za dawa katika mashamba ya mpunga yaliyoshambuliwa na wadudu hao Wilaya za Kati na Kaskazini ”B”;

- Mafunzo yalitolewa kwa mabibi na mabwana shamba 79 juu ya mbinu bora za kilimo katika Wilaya za Kaskazini "A" na "B" na Wilaya ya Magharibi Unguja;

- Jumla ya mabibi na mabwanashamba 22 kutoka Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja walipatiwa mafunzo juu ya udhibiti wa maradhi ya mpunga; na

- Jumla ya tani 1,424 za karafuu zilikaguliwa na kupasishwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi. Aidha, mazao mengine ya biashara yakiwemo mwani, pumba na makome yalikaguliwa.

MALENGO KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi juu ya mbinu shirikishi za kilimo bora kwa mabibi na mabwana shamba 140 (90 Unguja na 50 Pemba);

- Kuendeleza kazi ya usambazaji wa dawa katika mitego 21,615 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda pamoja na kununua mitego mipya 500 na kutoa mafunzo kwa kutumia mbinu mchanganyiko Unguja na Pemba;

- Kuendeleza kazi za karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo karafuu kwa ajili ya usafirishaji na kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima;

- Kuzalisha tani 350 kutoka kwa wakulima wa mikataba na kununua tani 150 za mbegu ya mpunga kutoka Tanzania Bara na kuzalisha tani 5 za mahindi, 2 za mtama na tani 8 za jamii ya kunde katika kituo cha uzalishaji mbegu Bambi na mashamba ya JKU;

- Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kutengeneza matrekta 29 na zana zake (10 Pemba na Unguja 19);

- Kuwaelimisha wakulima 150 juu ya mbinu za kilimo bora kupitia mabwana/mabibishamba, skuli za wakulima na jumuia zao; na

- Kununua na kusambaza tani 750 za mbolea (*TSP* tani 150, *UREA* tani 600) na lita 20,000 za dawa ya kuulia gugu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara iliombewa Tsh. 5,841,254,438 hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh 3,351,146,996 sawa na asilimia 57 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya Tsh. 4,802,444,000 kutoka Serikalini.

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO

Mhe. Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za utafiti katika sekta za Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi hii inajumuisha vituo vyote vya utafiti vilivyo ndani ya sekta ya Kilimo na Maliasili.

MALENGO YA TAASISI YA UTAFITI KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuanzisha na kuendeleza tafiti 17 za mbegu na mbinu mpya za uzalishaji wa mazao makuu ya chakula;

- Kufanya utafiti wa mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya biashara yakiwemo mikarafuu, minazi na matumizi bora ya udongo;

- Kujenga miundombinu ya maji na uzio katika maabara mpya ya mpunga pamoja na kukarabati jengo la uchunguzi wa mimea *(screen house)* liliopo Kizimbani na ukarabati wa maabara ya mazao iliyoko Matangatuani Pemba na ununuzi wa vifaa;

- Kuendelea na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano na utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ili kuweka mazingira mazuri katika utekelezaji wa kazi za utafiti; na

- Kuotesha miche 10,000 ya minazi katika vitalu vya Selemu na Kidichi.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Taasisi imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Tafiti sita mpya za mpunga zimeanzishwa na tafiti nyengine saba zimeendelezwa;

- Vishamba 40 vya majaribio juu ya matumizi ya mbinu bora za uzalishaji wa zao la mpunga wa kutegemea mvua zimeanzishwa na tathmini ya majaribio hayo imeonesha kwamba upo uwezekano wa kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka tani 1 hadi tani 5 kwa hekta endapo mkulima atazingatia matumizi ya teknolojia iliyofanyiwa majaribio;

- Utafiti wa awali wa mbegu 13 za muhogo zenye kustahamili maradhi ya michirizi ya kahawia *(Cassava brown streak disease)* na zenye uzazi mkubwa zimefanyika katika vituo vya utafiti vya Kizimbani na Matangatuani na kwa wakulima wa maeneo ya Potoa, Kilombero, Chaani, Bungi na

Bumbwini kwa Unguja na Vijileni, Konde, Pembeni na Matangatuani kwa Pemba;

- Tafiti 3 zinazojumuisha mbegu 30 za viazi vitamu vyenye viini lishe zimefanyika. Matokeo ya awali yameonesha kwamba mbegu 10 zina uwezo mkubwa wa uzalishaji, ustahamilivu, ladha nzuri na zimechaguliwa na wakulima kwa kuziendeleza;

- Ukusanyaji na utunzaji wa viasilia vya mimea *(germplasm conservation)* 50 vya muhogo, 33 vya viazi vitamu, 50 vya mpunga na 36 vya migomba umefanyika katika vituo vya Kizimbani na Matangatuani;

- Uchunguzi wa awali wa ukuaji wa miche ya mikarafuu kwa kutumia udongo tofauti kwenye vitalu umefanyika katika kituo cha Matangatuani. Utafiti wa viwango vya mbolea ya samadi katika kilimo cha migomba unaendelea na takwimu za awali zimekusanywa;

- Utayarishaji wa ramani ya aina za udongo wa Unguja na Pemba kwa kutumia *digital* unaendelea;

- Ujenzi wa maabara mpya ya utafiti wa mpunga na ukarabati wa maabara za udongo, *tissue culture* na usarifu wa mazao umekamilika na zimeanza kutumika; na

- Miche 6,350 ya minazi imeoteshwa.

MALENGO YA TAASISI KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuanzisha na kuendeleza tafiti za mbegu na mbinu mpya za uzalishaji wa mazao makuu ya chakula na biashara yakiwemo nazi, mpunga, mazao ya mizizi, migomba, mboga na matunda;

- Kukarabati maabara ya Matangatuani, majengo ya uchunguzi wa mimea (*Screen house*) na kujenga uzio katika maabara mpya ya mpunga Kizimbani; na

- Kukamilisha Mpango Mkakati wa miaka mitano na utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ili kuweka mazingira mazuri katika utekelezaji wa kazi za utafiti.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14, Taasisi iliombewa jumla ya Tsh. 1,115,298,710 kwa kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 140,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Mei, mwaka 2014 jumla ya Tsh. 965,099,310 sawa na asilimia 87 kwa kazi za kawaida na Tsh. 10,000,000 sawa na asilimia 7 kwa kazi za maendeleo zimepatikana. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/15, Taasisi imepangiwa kupata Tsh. 1,221,269,000 kwa kazi za kawaida na Tsh. 300,000,000 kwa kazi za maendeleo.

CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kina jukumu la kutoa utaalamu/mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kimelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 184, ngazi ya Cheti 135 na Diploma 49;

- Kuendelea na kazi za ujenzi wa Dakhalia moja yenye ghorofa 4 yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 wa kike kwa wakati mmoja;

- Kufanya ukarabati wa Dakhalia mbili; na

- Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji katika bonde moja kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II*.

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2013/2014

Mhe. Spika, mwaka wa fedha wa 2013/2014, Chuo kimetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Jumla ya wanafunzi 197 walipatiwa mafunzo ya kilimo na mifugo katika ngazi ya Diploma na Cheti. Aidha, wanafunzi 24 wa Diploma wa awamu ya kwanza wamemaliza;

- Kazi ya kutayarisha michoro na makadirio ya ujenzi wa Dakhalia moja yenye ghorofa 4 yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 wa kike kwa wakati mmoja imeshakamilika;

- Kazi za kukarabati Dakhalia mbili (ya wanafunzi wa kike na wa kiume) umekamilika; na

- Mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji na wa kutegemea mvua yametolewa kwa mabwana na mabibishamba 40 na wakulima 80 kutoka katika mabonde 24 ya mpunga wa kutegemea mvua na skimu 16 za mpunga wa umwagiliaji maji Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mwaka huu wa fedha 2013/2014, kwa kushirikiana na mradi wa *EPINAV*, Chuo kimetekeleza kazi zifuatazo:-

- Kutayarisha Mpango Mkakati wa miaka mitano;

- Maktaba imeimarishwa kwa kuwekewa huduma za mtandao, vifaa vya kisasa vya kuhifadhia taarifa na kumbukumbu. Pia, kompyuta 45 kwa ajili ya kufundishia zimenunuliwa;

- Ziara za kimasomo kwa wafanyakazi zimefanyika baina ya Chuo cha Kilimo Kizimbani na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Vyuo vya Kilimo na Mifugo vya Tanzania Bara, Chuo cha *University of Life Sciences* Norway na Tasisisi ya Utafiti ya Norway; na

- Walimu 11 wanaendelea na masomo, Shahada ya pili 9, Shahada ya kwanza mmoja na Shahada ya tatu mmoja katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine.

Mhe. Spika, Chuo kimeweza kuanzisha ushirikiano na Chuo cha *SJH* cha Norway kupitia Shirika la Kujitolea la Norway. Katika ushirikiano huu kila Chuo kimeweza kubadilishana walimu wawili ambao watafanya kazi za kujitolea kwa muda wa mwaka mmoja. Mradi huu wa ushirikiano utakuwa wa miaka mitatu ambapo jumla ya walimu sita kutoka katika kila Chuo watapata fursa ya kushiriki.

Mhe. Spika, mradi huu utakiwezesha Chuo kuimarisha mashamba ya maonesho ambayo yanatumika kwa ajili ya utoaji mafunzo kwa wanafunzi wa kawaida, wakulima na wafugaji. Walimu sita wa Chuo watapata kujifunza mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya mifugo wakiwemo mbuzi wa maziwa, uzalishaji wa mboga na uuzaji wa mazao.

MALENGO KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuendelea kutoa mafunzo ya kilimo na mifugo kwa wanafunzi 150 wa ngazi ya cheti na Diploma;

- Kuendelea na kazi za ujenzi wa Dakhalia moja itakayotumiwa na wanafunzi wa kike;

- Kutayarisha mpango wa matumizi ya shamba la RAZABA; na

- Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji katika bonde la Makombeni na Bumbwisudi kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II.*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kiliombewa Tshs. 500,000,000 ikiwa ni ruzuku na TSh.90,000,000 kwa kazi za maendeleo, ambapo hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Chuo kimepatiwa jumla ya Tsh. 289,400,000 sawa na asilimia 58 ya makadirio na Tsh. 10,000,000 ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 11 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kinaombewa jumla ya Tsh. 427,00,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 100,000,000 fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa bweni jipya.

IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Spika, Idara ina jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu na wanyama pori, kusimamia mashamba ya misitu na mbegu, upatikanaji wa miche bora, kuhamasisha kilimo cha biashara na kuratibu uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuotesha miche 1,500,000 katika Vitalu vya Serikali, kati ya miche hiyo 1,000,000 ya misitu na 500,000 ya matunda;
- Kuotesha miche 1,000,000 ya mikarafuu;
- Kupanda miti ya misitu hekta 300 katika misitu ya Serikali, hekta 30 za eneo la mikoko na kilomita 50 maeneo ya barabarani;
- Kutayarisha na kutekeleza mipango shirikishi ambayo itawezesha matumizi endelevu ya Maliasili Zizisorejesheka katika Wilaya za Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Kati kwa Unguja na Wilaya za Mkoani na Wete kwa Pemba;
- Kutayarisha na kutekeleza mpango wa kujikinga na matukio ya moto kwenye misitu ya jamii na Serikali;
- Kuimarisha na kuendeleza ufugaji nyuki wa kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa asali, kuongeza kipato kwa jamii na utunzaji wa misitu katika maeneo yanayozunguka misitu ya hifadhi;
- Kupitia Kanuni ya msumeno wa moto kwa lengo la kutokutumika tena; na
- Kukamilisha Sensa ya Miti *(Woody Biomass Survey).*

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Jumla ya miche 2,098,072 imeoteshwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 140 ya lengo (1,778,810 ya misitu, na 319,262 ya matunda na viungo);
- Jumla ya miche ya mikarafuu 941,176 imeoteshwa, (309,640 Unguja na 631,536 Pemba) sawa na asilimia 94 ya lengo;
- Jumla ya hekta 302 (12 Pemba na 290 Unguja) zimepandwa miti katika msimu wa vuli na masika 2013/2014. Hekta 30 zimepandwa miti ya mikoko (hekta 10 Pemba na 20 Unguja), Pia, kilomita 50 zimepandwa miti ya aina mbali mbali katika maeneo ya barabarani za Wilaya zote 10 za Unguja na Pemba chini ya usimamizi wa Wakuu wa Wilaya husika;
- Matayarisho ya awali ya mipango shirikishi ya matumizi endelevu ya maliasili zisizorejesheka katika Wilaya ya Kaskazini "A", "B" na Kati kwa Unguja na (Wilaya za Mkoani na Wete kwa Pemba) imeanza kutekelezwa;
- Rasimu ya kwanza ya mpango wa kujikinga na moto imetayarishwa sambamba na utoaji wa mafunzo ya kujikinga na matukio ya moto kwa wafanyakazi 21 na wanajamii 20 wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani na wanajamii wanaozunguka hifadhi hiyo yametolewa kwa kushirikiana na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Aidha, visima 10 vimechimbwa ndani ya Hifadhi ya Taifa kwa ajili ya kupata maji ya kuzimia moto;
- Jumla ya mizinga 350 (175 Unguja na 175 Pemba) ya kisasa ya kufugia nyuki imetengenezwa na kugaiwa kwa vikundi vya uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki. Aidha, uzalishaji wa asali kwa mwaka huu umefikiwa tani 6.5 kutoka tani 5;

- Kanuni ya kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto imefanyiwa mapitio ili kudhibiti uingizaji na matumizi yake; na

- Sensa ya miti ambayo imejuimisha idadi ya miti ya misitu, matunda na mikarafuu imekamilika.

MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuotesha miche 2,500,000 (1,000,000 ya misitu, 500,000 ya matunda na viungo katika vitalu vya Serikali na miche 1,000,000 ya mikarafuu);

- Kupanda miti ya misitu eneo la hekta 300 katika mashamba ya Serikali, hekta 40 za mikoko na kilomita 60 maeneo ya hifadhi ya barabara;

- Kukamilisha mipango shirikishi ya matumizi endelevu miwili (1 Unguja na 1 Pemba) ya maliasili zisizorejesheka;

- Kukamilisha na kutekeleza mpango wa kujikinga na matukio ya moto kwenye misitu ya serikali na jamii;

- Kuimarisha na kuendeleza ufugaji nyuki kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa asali, kuongeza kipato kwa jamii na utunzaji wa misitu katika maeneo yanayozunguka misitu ya hifadhi;

- Kufanya tathmini ya akiba ya mchanga uliopo na kujua mahitaji kwa mwaka;

- Kuendeleza uhifadhi na kuimarisha utalii endelevu katika hifadhi za misitu;

- Kukamilisha Sera ya Misitu na kufanya mapitio ya Sheria na Mpango wa muda mrefu wa kuendeleza misitu;

- Kufanya tathmini ili kujua hali halisi ya uzalishaji na kiuchumi ya mashamba ya mipira yanayomilikiwa na serikali na hatimae kuishauri serikali kupitia upya matumizi ya mashamba hayo; na

- Kutayarisha mpango wa usimamizi wa mashamba ya serikali ya mikarafuu na minazi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itasimamia miradi mikuu miwili kama ifuatavyo:-

- Mradi wa Taifa wa Uimarishaji Mikarafuu; *(Kiambatanisho Nam. 9).*

- Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili (HIMA); *(Kiambatanisho Nam. 10).*

- Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani. *(Kiambatanisho Nam. 11).* na

- Mradi wa kuangamiza Adui Kunguru. *(Kiambatanisho Nam.12).*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014,Idara iliombewa Tsh. 1,465,089,500 hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 1,243,722,930 sawa na asilimia 85 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya Tsh. 1,605,448,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kuratibu kazi za uhakika wa chakula na lishe ikiwa ni pamoja na kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe na tahadhari ya mapema juu ya matukio yanayohusiana na hali ya uhakika wa chakula na lishe hapa nchini. Idara pia ina jukumu la kusimamia na kuendesha Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar *(Zanzibar Food Reserve).*

MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kukarabati ghala moja la Hifadhi ya Chakula liliopo Unguja;
- Kutayarisha miongozo ya uendeshaji wa Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar;
- Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na utoaji wa tahadhari ya mapema juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe kwa kujenga uwezo katika ukusanyaji wa takwimu. Kazi zilizopangwa ni;
- Utayarishaji wa taratibu za ukusanyaji wa taarifa na takwimu; na
- Mafunzo kwa wafanyakazi wanane juu ya ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na uandishi wa ripoti za uhakika wa chakula na lishe.
- Kutoa taarifa za Hali ya Uhakika wa Chakula. Kazi zilizopangwa ni:
- Kukusanya takwimu na taarifa juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe;
- Uchambuzi na takwimu na taarifa za uhakika wa chakula na lishe;
- Uandishi na uchapishaji wa ripoti za hali ya uhakika wa chakula na lishe (*Food Balance Sheet Reports, Policy Briefs; Food Insecurity Reports*); na
- Kuratibu ushiriki wa Sekta na wadau husika katika kutekeleza masuala ya uhakika wa chakula na lishe.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Kazi ya ukarabati wa ghala haikufanyika kutokana na ukosefu wa fedha;
- Taratibu za ukusanyaji wa taarifa za takwimu za uhakika wa chakula zimekamilika sambamba na *database* ya *Food Security* na taarifa zimeanza kuingizwa katika *database*;
- Mafunzo yametolewa kwa wafanyakazi wanne juu ya ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na uandishi wa ripoti za uhakika wa chakula na lishe;
- Ripoti juu ya masuala ya uhakika wa chakula na lishe *(Food Balance Sheet 2012/2013)* imekamilika na ipo katika hatua za uchapishaji; na
- Miongozo ya uendeshaji wa Hifadhi ya Chakula *(Operational Procedure Manual)* imekamilika kwa hatua ya mwanzo.

Mhe. Spika, miongozo ya uendeshaji wa Hifadhi ya Chakula itasaidia katika kuhakikisha kwamba Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar inaendeshwa katika hali ya uwazi, kwa kufuata taratibu ambazo zinakubalika kisheria na Kimataifa na kuhakikisha kuwa inaendeshwa kwa mujibu wa malengo ya uanzishwaji wake. Kutokana na miongozo hii, Baraza la Taifa la Uhakika wa Chakula na Lishe ndio chombo kikuu cha kufanya maamuzi juu ya matumizi ya chakula cha akiba.Chakula hiki kitatumika kwa kuuzwa katika soko la ndani pale itakapobainika kuwa kuna upungufu wa chakula nchini. Chakula hiki pia kitatumika kwa kutolewa kama chakula cha msaada kwa kaya ambazo zitathibitika kuwa zipo katika hali mbaya iliyokithiri ya ukosefu wa chakula. Mfumo maalumu na vigezo vya kuweza kuwatambua wananchi walio katika hali hiyo umetayarishwa.

Mhe. Spika, kwa vile mchele unaotarajiwa kuwekwa katika maghala haya, ni kwa kipindi cha miezi sita, Wizara tayari imeandaa utaratibu kwa kushirikiana na wafanyabiashara katika kuuza mchele uliowekwa na kununua mchele mpya kwa ajili ya kuwekwa akiba.

MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015, Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuchapisha na kusambaza matokeo ya ufuatiliaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe ikiwemo *(FSN Policy Briefs, Food Balance Sheet Report);*

- Kuandaa vipindi vya radio na kuchapisha jarida la masuala ya uhakika wa chakula na lishe;

- Kuandaa mkutano na wadau wa sekta mbali mbali pamoja na kushajihisha uhusiano wa kisekta katika kusimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe;

- Kuendeleza *database* ya uhakika wa chakula na lishe;

- Kuanzisha timu ya wataalamu wa ufuatiliaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe katika taasisi husika; na

- Kukarabati ghala la Hifadhi yaTaifa ya Chakula la Unguja.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itaendelea kusimamia Programu ya Lishe ya Mwanzo Bora. *(Kiambatanisho Nam. 13).*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14, iliombewa jumla ya Tsh. 190,739,700 kutoka Serikalini kwa kutekeleza kazi za kawaida na jumla ya Tsh. 160,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 134,240,300 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 70 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya Tsh.194,500,000 kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida na Tsh.160,000,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini, pamoja na kutoa taaluma za kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Idara pia ina jukumu la kushajihisha na kusimamia Jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji sambamba na kutoa elimu ya utaalamu juu ya teknolojia za kilimo cha umwagiliaji maji.

MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuchimba visima vinane katika vituo vya Kibondemzungu, Ole, Kisimamchanga, Kibojemkwajuni, Cheju, Kibokwa na Bumbwisudi;

- Kujenga mtaro wa saruji mita 500 na kununua pampu mbili kwa ajili ya mabonde ya Bumbwisudi na Kibokwa kupitia mradi wa *KOICA*;

- Ujenzi wa vibanda vinne vya kuendeshea pampu katika kituo cha Kibokwa (1), Bumbwisudi (1) na Mtwango (2);

- Kuunga umeme katika bonde la Machigini Pemba;

- Kupima, kuchora ramani na kusanifu miundombinu ya umwagiliaji maji katika eneo la hekta 2,105 kwenye vituo vya Cheju, Kilombero, Chaani, Mlemele na Makwararani kupitia Mradi wa *EXIM BANK* – Korea;

- Kutayarisha zabuni na kutafuta mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu katika eneo la hekta 2,105;

- Ujenzi wa njia ya kutolea maji ya ziada *(spillway)* katika tuta lilioko bonde la Chamawe Pemba;

- Kukarabati visima viwili na pampu nne za vituo vya Bumbwisudi, Cheju, Saninga na Kibokwa; na

- Utayarishaji wa ardhi Makombeni hekta 7 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji.

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Matengenezo ya pampu tano katika mabonde ya Cheju, Uzini, Kibokwa na Bumbwisudi yamefanyika;
- Ujenzi wa vibanda vitatu vya pampu, viwili kituo cha Mtwango na kimoja Bumbwisudi umefanyika.;
- Vifaa vya ujenzi wa bwawa la Kinyakuzi vimenunuliwa na matengenezo yameanza;
- Kazi ya kumpata mkandarasi kwa mradi wa miundombinu ya umwagiliaji maji kupitia mkopo wa *EXIM BANK* ya Korea imekamilika;
- Uchimbaji wa kisima kimoja Bumbwisudi umekamilika; na
- Ujenzi wa msingi wa kumwagilia maji mita 500 kwa kiwango cha saruji katika kituo cha Bumbwisudi umekamilika.

MALENGO YA IDARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji kwa kufanya kazi zifuatazo:-
    - Kukarabati njia za mashambani mita 400 katika vituo vya Bumbwisudi na Mtwango;
    - Uchimbaji wa visima viwili pamoja na ujenzi wa vibanda viwili vya kuendeshea pampu katika vituo vya Kibonde mzungu na Ole;
    - Kuunga umeme katika kituo cha Machigini, Mtwango na Bumbwisudi;
    - Utayarishaji wa eneo la hekta 7 kwa upimaji na ukataji wa ploti katika kituo cha Makombeni;
    - Ukarabati wa pampu sita na visima vitatu katika vituo vya Makombeni, Bumbwisudi, Cheju, Kibokwa, Mtwango na Uzini; na
    - Ujenzi wa banio katika tuta la kuzuia maji ya bahari bonde la Chamawe.
2. Kukarabati majengo ya vituo vya umwagiliaji, pamoja na kujenga kituo kipya cha Kianga kwa kufanya kazi zifuatazo:-
    - Ukarabati wa majengo manne ya Idara (Mtwango, Bumbwisudi, Weni na Mbweni; na
    - Ujenzi wa Kituo cha Umwagiliaji Maji Kianga.
3. Kuwajengea uwezo kiuzalishaji na kiutendaji wakulima wa umwagiliaji maji kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-
    - Kutoa mafunzo ya mbinu bora za umwagiliaji maji kwa wakulima na skuli za wakulima 10 (Koani, Kianga, Bumbwisudi *Field* 1 na 3, Kibokwa na Uzini kwa Unguja, Kinyakuzi, Mangwena, Tibirinzi na Ole kwa Pemba);
    - Ziara za mafunzo kwa wakulima 20 wa Makombeni Pemba kwenda Moshi Tanzania Bara; na
    - Kutayarisha vishamba vinne (Ole na Weni kwa Pemba na Koani na Banda maji kwa Unguja) vya majaribio ya uvunaji wa maji ya mvua.
4. Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji hekta 10 jimbo la Muyuni kwa msaada wa fedha za

Food Aid Counterpart Fund.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara iliombewa Tsh. 671,053,360 kwa kazi za kawaida hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 564,688,677 sawa na asilimia 84 ya makadirio. Kwa upande wa fedha za maendeleo mchango wa SMZ Idara ilitengewa Tsh. 450,000,000 hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 69,000,000 sawa na asilimia 15. Aidha, Idara imepata jumla ya TSh. 250,000,000 kutoka *Food Aid Counterpart Fund* mnamo mwezi wa Mei, 2014, kwa ajili ya mradi wa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji Muyuni. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaombewa jumla ya Tsh. 725,370,000 kutoka SMZ. Kwa upande wa fedha za maendeleo mchango wa SMZ inaombewa Tsh. 400,000,000. Kutoka kwa washirika wa maendeleo *(KOREA EXIM BANK),* Idara inaombewa jumla ya Tsh. 3,858,000,000.

OFISI KUU PEMBA:

Mhe. Spika, utekelezaji wa kazi za Wizara kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba mwaka wa fedha 2013/2014, unaendana na maelezo ya kila Idara ambayo yamehusisha na kazi za Ofisi Kuu Pemba. Ofisi hii ya Pemba ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na kazi zote za Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa Pemba zinatekelezwa kama zilivyoainishwa katika Idara na Taasisi za Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza lako tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya Tsh. 2,126,825,450 kwa kazi za kawaida na hadi kufika tarehe 30, Mei, 2014, Ofisi Kuu Pemba imepatiwa Tsh. 1,762,045,950 sawa na asilimia 83. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi Kuu Pemba inaombewa jumla ya Tsh. 2,861,813,000 kwa kazi za kawaida.

CHANGAMOTO ZA WIZARA

Mhe. Spika**,** pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, bado Wizara ya Kilimo na Maliasili inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Mabadiliko ya hali ya hewa ni moja ya changamoto kubwa zinazoathiri kilimo hasa cha mpunga wa kutegemea mvua kutokana na kutokuwa na miongo isiyotabirika;
- Ushiriki mdogo wa Sekta binafsi katika kutoa huduma za kilimo;
- Ongezeko la mahitaji na matumizi makubwa ya pembejeo linaathiri utekelezaji wa mpango wa ruzuku;
- Uvamizi wa maeneo ya kilimo kwa kazi za maendeleo ya jamii; na
- Ufinyu wa bajeti na miundombinu ya kusaidia sekta ya Kilimo.

Mhe. Spika, changamoto kubwa inayoathiri ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Wizara, ni upatikanaji mdogo wa fedha zilizotengwa katika bajeti na kutoingizwa fedha kwa wakati. Hali hii inaathiri utekelezaji wa kazi hasa katika suala zima la upatikanaji wa pembejeo za kutosha na kwa wakati, uzalishaji wa miche na kazi za utafiti.

NJIA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili, inachukuwa hatua za makusudi kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa kama ifuatavyo:-

- Mabadiliko ya hali ya hewa.

  Ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, Wizara inatoa msisitizo juu ya kilimo cha umwagiliaji wa mpunga na mazao mengine ya juu pamoja na kuendelea kuhamasisha wakulima kuvuna maji ya mvua. Aidha, hatua za uibuaji wa teknolojia za kilimo na misitu zitaendelea kuelekezwa katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa;

- Ushiriki mdogo wa Sekta binafsi katika kutoa huduma za kilimo,

  Kwa kuthamini mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya kiuchumi, Wizara imeanza

mashirikiano na sekta binafsi katika kuendeleza kilimo;

- Ongezeko la mahitaji na matumizi makubwa ya pembejeo linaathiri utekelezaji wa mpango wa ruzuku.

  Kutokana na ongezekeo la mahitaji, pamoja na matumizi makubwa ya pembejeo ikiwemo mbolea, mbegu bora na madawa ya magugu, Wizara imefanya tafiti juu ya tathmini ya upatikanaji na usambazaji wa pembejeo. Ripoti ya tathmini hiyo itaiwezesha Wizara kufanya mapitio ya utaratibu wa ruzuku na kuweka mfumo maalum kwa ajili ya utoaji wa pembejeo kwa njia ya ruzuku kulingana na hali halisi;

- Uvamizi wa maeneo ya kilimo kwa matumizi ya jamii.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la uvamizi wa ardhi ya kilimo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, itaendelea kuyapima na kuyapatia hati miliki maeneo ya serikali yaliyotengwa kwa kilimo.

Aidha, Wizara inatoa wito kwa viongozi wa Mikoa, Wilaya na Shehia kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kusimamia sheria na Kanuni zilizowekwa ili kuepuka uvamizi na kuhifadhi maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo.

MFUMO WA BAJETI UNAOZINGATIA PROGRAMU

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na utekelezaji wa mfumo wa bajeti ambayo inazingatia utekelezaji wa Programu na Miradi husika (*Program Based Budget)*. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, utekelezaji wa Programu na Miradi utawasilishwa katika kitabu cha muhutasari wa bajeti inayotumia mfumo huu utakaowasilishwa na Wizara ya Fedha.

SHUKRANI

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa muongozo na ushauri wao uliopelekea kukamilika kwa hotuba hii. Aidha, tunazishukuru nchi na Mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo, zikiwemo nchi za Japan, Finland, Norway, Ireland, China, India, Israel, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ujerumani, Vietnam na Uholanzi. Aidha, tunaomba kutoa shukurani za pekee kwa Mashirika na Taasisi za Kikanda na za Kimataifa zifuatazo; *AfricaRice*, *COSTECH, SUMA JKT, TASAF, ZSTC, SIDO,* Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Tanzania, *SUA, IAEA, INGER-Africa*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika - AfDB, IFAD, *UNDP, FAO, JICA, UNICEF, UPOV, USAID, KOICA, IITA, iAGRI, IRRI, CFC, GEF, Exim Bank of Korea, AVRDC* na *AGRA*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Aidha, nawapongeza wakulima wote waliotumia ubunifu wao katika kufanya tafiti mbali mbali, pamoja na waliohamasika kwa kutumia pembejeo za kilimo zikiwemo mbolea, mbegu bora na zana za kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija.

Mhe. Spika, pia, naomba kuwashukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Manaibu wa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi, watumishi wote wa Wizara pamoja na wadau wa Sekta ya Kilimo na Maliasili kwa juhudi, ushirikiano, ushauri na utendaji wao wa kazi uliowezesha kutekelezwa kwa malengo na kazi za Wizara kwa mwaka 2013/2014 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2014/2015 ili kufikia malengo yaliyopangwa.

MAKADIRIO YA MAOMBI YA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Baraza lako tukufu liidhinishe Tsh. 23,369,002,000 kati ya hizo Tsh. 13,758,000,000 ni kwa matumizi ya kazi za kawaida ambapo (Mishahara Tsh.

9,034,000,000, Matumizi mengineyo Tsh. 4,297,000,000 na Tsh. 427,000,000 ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani) na Tsh. 9,611,002,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 10 ya maendeleo ambapo Tsh. 1,500,000,000 ikiwa ni mchango wa serikali na kwa upande wa washirika wa maendeleo ni Tsh. 8,111,002,000.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ninataka nikushukuru sana Mhe. Kaimu Waziri kwa kuwasilisha hotuba yako kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Maliasili kwa muda wa dakika 35 tu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, ninafikiri muda uliobaki hautotasha kumwita Mwenyekiti wa Kamati ili kuja kutoa mchango wao wa Kamati, lakini kuna jambo moja muhimu ambalo inabidi tuliwekee utaratibu.

Waheshimiwa Wajumbe, kunako mwanzoni mwa wiki hii au wiki iliyopita, nilimuelekeza Mwenyekiti wa Baraza atoe taarifa kwenu Waheshimiwa Wajumbe, kwamba tunakusudia kumaliza shughuli zetu na nilifikiri baada ya kushauriana na baadhi ya wenzangu kwamba ingekuwa ni vyema tukamaliza shughuli zetu hizi za mkutano huu wa bajeti mapema kidogo kabla ya kwenda kuingia mwezi wa Ramadhani. Hii itasaidia WaheshimiwaWajumbe, kuingia katika mwezi wa Ramadhani, kufunga na kufutari na familia zenu.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa kufanikiwa kufanya hivyo, inabidi tukubaliane kwa kuweka utaratibu ili shughuli zetu ziwe zinaendelea kwa Jumamosi mbili; ikiwe ni Jumamosi ya kesho ya tarehe 21/06/2014 na Jumamosi ya tarehe 28/06/2014 ambapo siku hiyo tunategemea tumalize kabisa shughuli zetu.

Waheshimiwa Wajumbe, utaratibu wa kawaida kama ninavyoelewa upo. Hakuna matata katika hilo, lakini katika kufanya shughuli hiyo tulichokubaliana tunaweza tukaamua vile vile, unajua kazi yetu mara hii imekuwa ni kubwa. Imechukua muda mrefu kidogo na tumeingia shughuli hii tukiwa tunatokea kwenye Bunge Maalum, kiasi cha kwamba tumeingia humu ndani tukiwa tayari tumefanya kazi kubwa, lakini pia, na kazi hii nayo si ndogo.

Waheshimiwa Wajumbe, isitoshe kwa Wajumbe wengi wenu mara baada ya kurudi kwenye Bunge Maalum, muliingia kwanza kwenye Kamati tukisimamia mambo mbali mbali kama utaratibu ulivyo na baadae mukaingia katika Kamati ili kupitia makadirio ya bajeti ya serikali na hatimaye bajeti kwa wizara mbali mbali. Kwa hivyo, hapana shaka kama ilivyo kawaida pengine Jumamosi na Jumapili ni vyema tukawa tunapumzika kama tulivyofanya mwanzo, lakini kwa hizi mbili na kwa sababu ya mnasaba huo, Wajumbe, ilikuwa tunataka tuwaombe kwa utaratibu ambao utawekwa baadae na Mhe. Waziri, siku mbili hizi ya Jumamosi hii ya tarehe 21/06/2014 na tarehe 28/06/2014, basi tuzifanyie kazi.

Waheshimiwa Wajumbe, lakini tunaweza tukaamua kwamba kazi yetu iendelee na tena hiyo niliwahi kupata ushauri kwa baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba basi tufanye kikao kimoja tu, pengine twende mpaka kunako saa tisa tumalize shughuli ili jioni tusije tupate tumpumzike. Sasa nikasema kwamba basi haya yote tumuachie Mhe. Waziri, aseme maneno ili hatimaye Waheshimiwa Wajumbe, mukipenda hivyo, muidhinishe tufanye hivyo. Hii itakwenda pamoja na utaratibu wa kawaida kwa siku ambazo si rasmi za utaratibu wa kazi zetu humu ndani ya Baraza. Nimuombe basi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ili aweke utaratibu na Waheshimiwa Wajumbe, muombe muridhie jambo hilo. Mhe.Waziri karibu.

HOJA YA KUWEKA KANDO KANUNI ILI BARAZA KUENDELEA KWA SIKU ZA JUMAMOSI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Kanuni ya 23 (1) na (4) za Kanuni za Baraza la Wawakilishi, limeweka nyakati za vikao vya Baraza kuwa katika siku za kazi pekee na kwa kuwa siku zilizobaki ni chache kabla ya kuingia katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kwa kuwa kwa mujibu wa taratibu za vikao vya Baraza vinavyoendelea Mkutano huu wa bajeti unaweza kumalizika tukiwa ndani ya kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, na kwa kuwa ni vyema shughuli za Baraza zikamalizika mapema ili Wajumbe waweze kufunga mwezi huu wa Ramadhani kwa utulivu wakiwa pamoja na familia zao. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 156 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, naomba kutoa hoja ya kutenga kando Kanuni ya 23 (4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ili Baraza hili liweze kuendelea na vikao vyake siku ya Jumamosi ya tarehe 21/06/2014 na Jumamosi ya tarehe 28/06/2014, kuanzia saa tatu asubuhi hadi kumaliza shughuli

zitakazopangwa kwa siku hizo za Jumamosi mapema iwezekanavyo ili tukamilishe shughuli zetu kabla ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuanza.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja ya maelezo yake imetolewa. Niwahoji sasa. Wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa mashirikiano hayo makubwa na sasa tusitishe shughuli zetu hadi saa kumi na moja jioni ya leo ambapo tutaanza mchango wa hoja hii iliyowasilisha hivi punde.Tukutane saa kumi na moja leo jioni. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5:52 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

Kiambatanisho. Na.1. Takwimu za Uzalishaji wa Mazao ya kilimo kwa Tani Mwaka 2012/2013

Mazao/Mwaka	2008	2009	2010	2011	2012	2013
Mahindi	1,920	2,011.75	3,112	3,281	856.67	1,419.07
Mtama	610	457	572	512	484.31	225.53
Mpunga	20,857	26,980	21,014	23,702	6,372.15	33,655.06
Muhogo	153,050	195,674	229,284	273,342	192,072.68	164,332.29
Ndizi	100,873	100,873	102,258	110,250	97,934.53	68,357.60
Viazi Vitamu	55,294	53,596	58,953	92,715	31,767.75	53,656.6
Viazi Vikuu	3,516	11,373	7,488	4,212	3,563.80	2,351.5
Njugu Nyasa	465	320.43	432	401	407.26	642.84

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali (2014)

Kiambatanisho Na. 2: TAARIFA YA MAPATO KWA MWAKA 2013/2014 NA MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2014/2015

KASMA	MAELEZO	MAPATO YALIYOIDHINISHWA 2013/2014	MAPATO HALISI JULAI – MAY 2013/2014	%	MAKADIRIO YA MAPATO 2014/2015
0301 OFISI KUU PEMBA.					
142224	MAZAO YA MISITU	20,000,000	15,907,400	80	20,000,000
142299	MAPATO YA UKODISHAJI WA MASHAMBA YA MIKARAFUU	345,000,000	158,179,900	46	200,000,000
142225	ADA YA UUZAJI MAWE, MICHANGA NA KOKOTO	28,000,000	75,294,050	269	71,500,000
	JUMLA NDOGO	**393,000,000**	**249,381,350**	**63**	**291,500,000**
142254	UKAGUZI A MAZAO	4,000,000	4,816,000	120	5,000,000
142257	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	500,000	-	0	500,000
145001	MAPATO MENGINEO	1,500,000	362,000	24	1,000,000
142101	MAUZAJI YA MICHE	1,000,000	1,004,000	100	2,000,000
	JUMLA NDOGO	**7,000,000**	**6,182,000**	88	8,500,000
	JUMLA PEMBA	**400,000,000**	**255563350**	**64**	**300,000,000**
0401 IDARA YA SERA, MIPANGO NA UENDESHAJI.					
145001	MAPATO MANGINEO	2,000,000	5,950,000	298	10,000,000
	JUMLA NDOGO	**2,000,000**	**5,950,000**	**298**	**10,000,000**
1501 IDARA YA KILIMO					
142254	UKAGUZI WA MAZAO	15,000,000	14,556,900	97	15,000,000
	JUMLA NDOGO	**15,000,000**	**14,556,900**	**97**	**15,000,000**
1701 TAASISIS YA UTAFITI.					
142257	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE.	15,000,000	23,340,700	156	25,000,000
142281	ADA YA UINGIZAJI WATALII	6,000,000	7,428,700	124	10,000,000
	JUMLA NDOGO	**21,000,000**	**30,769,400**	**147**	**35,000,000**
0701 IDARA YA MISITU.					
142101	MAUZO YA MICHE	25,000,000	15,290,800	61	15,000,000
142224	MAZAO YA MISITU	100,000,000	118,991,720	119	110,000,000
142299	MAPATO YA UKODISHAJI WA MASHAMBA YA MIKARAFUU	5,000,000	-	0	
142225	ADA YA UUZAJI WA MAWE NA MICHANGA	180,000,000	415,058,470	231	360,000,000
	JUMLA NDOGO	**310,000,000**	**549,340,990**	**177**	**485,000,000**
	JUMLA UNGUJA	**348,000,000**	**600,617,290**	**173**	**545,000,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA	**748,000,000**	**856,180,640**	**114**	**845,000,000**

Kiambatanisho Na. 3(a): MUHTASARI WA HESABU KWA KAZI ZA KAWAIDA: JULY 2013 - MEI, 2014

UNGUJA:

	JINA LA IDARA/TAASISI	JUMLA YA BAJETI JULAI,13/JUNI,14	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI- MEI, 2014	%	MAKISIO YA BAJETI 2014/2015
1	IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	470,545,700	338,993,537	**72**	377,129,000
2	IDARA YA MISITU NA MALI ZISIZOREJESHEKA	1,465,089,500	1,243,722,930	**85**	1,605,448,000
3	IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	671,053,360	564,688,677	**84**	725,370,000
4	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	1,261,892,700	904,715,308	**72**	1,543,027,000
5	IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	190,739,700	134,240,300	**70**	194,500,000
6	IDARA YA KILIMO	5,841,254,438	3,351,146,996	**57**	4,802,444,000
7	TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	1,115,298,710	965,099,310	**87**	1,221,269,000
	JUMLA	**11,015,874,108**	**7,502,607,058**	**68**	**10,469,187,000**
8	RUZUKU CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	500,000,000	289,400,000.00	**58**	427,000,000
	JUMLA	**11,515,874,108**	**7,792,007,058**	**68**	**10,896,187,000**

PEMBA:
MUHTASARI WA HESABU KWA KAZI ZA KAWAIDA: JULY 2013 - MEI, 2014

	JINA LA IDARA/TAASISI	JUMLA YA BAJETI JULAI,13/JUNI,14	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI- MEI, 2014	%	MAKISIO YA BAJETI 2014/2015
1	IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	25,080,000	11,581,985	46	60,000,000
2	IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA	88,760,000	15,836,475	18	94,960,000
3	IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	36,480,000	15,493,010	42	90,000,000
4	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	1,889,865,450	1,683,527,905	89	2,409,853,000
5	IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	18,240,000	7,552,753	41	42,000,000
6	IDARA YA KILIMO	41,040,000	16,264,043	40	99,000,000
7	TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	27,360,000	11,789,779	43	66,000,000
	JUMLA	**2,126,825,450**	**1,762,045,950**	**83**	**2,861,813,000**
	JUMLA KUU	**13,642,699,558**	**9,554,053,008**	**70**	**13,758,000,000**

Kiambatanisho. Na. 3(b): MCHANGANUO WA HESABU KWA KAZI ZA KAWAIDA: JULY 2013 - MEI,2014

UNGUJA

	JINA LA IDARA/TAASISI	MISHAHARA			MATUMIZI MENGINEYO		
		BAJETI YA JULAI,13/ JUNI,14	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MEI,2014	%	BAJETI YA JULAI,13/JUNI,14	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MEI,2014	%
1	IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	170,545,700	153,825,300	90	300,000,000	185,168,237	62
2	IDARA YA MISITU NA MALI ZISIZOREJESHEKA	1,305,089,500	1,187,987,650	91	160,000,000	55,735,280	35
3	IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	592,053,360	538,008,360	91	79,000,000	26,680,317	34
4	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	791,892,700	719,348,500	91	470,000,000	185,366,808	39
5	IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	120,739,700	109,340,300	91	70,000,000	24,900,000	36
6	IDARA YA KILIMO	2,091,254,438	1,895,067,238	91	3,750,000,000	1,456,079,758	39
7	TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	1,035,298,710	939,669,310	91	80,000,000	25,430,000	32
	JUMLA	6,106,874,108	5,543,246,658	91	4,909,000,000	1,959,360,400	40
8	RUZUKU CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	-	-		500,000,000	289,400,000	58
	JUMLA	**6,106,874,108**	**5,543,246,658**	**91**	**5,409,000,000**	**2,248,760,400**	**42**

PEMBA

	JINA LA IDARA/TAASISI	MISHAHARA			MATUMIZI MENGINEYO		
		BAJETI YA JULAI,13/JUNI,14	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MEI, 14	%	BAJETI YA JULAI,13/JUN,14	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MEI, 14	%
1	IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI				25,080,000	11,581,985	46
2	IDARA YA MISITU NA MALI ZISIZOREJESHEKA				88,760,000	15,836,475	18
3	IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI				36,480,000	15,493,010	42
4	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	1,796,825,450	1,627,045,950	91	93,040,000	56,481,955	61
5	IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE				18,240,000	7,552,753	41
6	IDARA YA KILIMO				41,040,000	16,264,043	40
7	TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	-			27,360,000	11,789,779	43
	JUMLA	**1,796,825,450**	**1,627,045,950**	**91**	**330,000,000**	**135,000,000**	**41**
	JUMLA KUU	**7,903,699,558**	**7,170,292,608**	**91**	**5,739,000,000**	**2,383,760,400**	**42**

Kiambatanisho Na.4(a): TAARIFA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA KWA KAZI ZA MAENDELEO KUANZIA JULAI, 2013 HADI MEI, 2014 PAMOJA NA MAKISIO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 KWA FEDHA ZA SMZ

KASMA	JINA LA MRADI	MAKISIO SMZ 2013/2014	FEDHA ZILIZOPATIKANA SMZ JULAI / MEI, 2014	%	MAKISO MWAKA 2014/15
610002	UHIFADHI WA MISITU YA PWANI	35,000,000	22,000,000	63	
610003	HIFADHI YA MISITU YA ASILI	35,000,000	25,000,000	71	
610004	MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA KILIMO CHA U/MAJI	450,000,000	69,000,000	15	400,000,000
610005	MRADI WA KUIMARISHA MIKARAFUU	390,000,000	175,619,815	45	300,000,000
610007	MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	160,000,000	-	-	160,000,000
610008	MRADI WA KUKUZA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO	50,000,000	50,000,000	100	100,000,000
610014	PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO(ASDP-L)	35,000,000	24,190,000	69	30,000,000
610015	PROGRAMU YA KUIMARISHA HUDUMA YA KILIMO(*ASSP*)	55,000,000	43,000,000	78	-
610016	PROGRAMU YA UTAFITI WA KILIMO NA MALIASILI	140,000,000	10,000,000	7	300,000,000
710001	KUANGAMIZA ADUI KUNGURU	20,000,000	10,000,000	50	-
660004	THAMANI NA MISAADA VIJIJINI (*MIVARF*)	60,000,000	9,000,000	15	60,000,000
610020	KATI INFRASTRUCTURE	90,000,000	10,000,000	11	100,000,000
610019	PROGRAM YA MWANZO BORA		-		
610021	MPANGO WA ULIMWENGU WA KUSAIDIA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA (*GAFSIP*)	40,000,000	-	-	50,000,000
	JUMLA	**1,560,000,000**	**447,809,815**	**29**	**1,500,000,000**

Kiambatanisho Na. 4(b): TAARIFA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA KWA KAZI ZA MAENDELEO KUANZIA JULAI, 2013 HADI MEI, 2014 PAMOJA NA MAKISIO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 FEDHA KUTOKA KWA WAHISANI

KASMA	JINA LA MRADI	MAKISIO 2013/2014	FEDHA ZILIZOPATIKA NA JULAI / MEI, 2014	%	MAKISO MWAKA 2014/15
610002	UHIFADHI WA MISITU YA PWANI	350,000,000	170,000,000	49	-
610003	HIFADHI YA MISITU YA ASILI	250,000,000	215,991,000	86	84,000,000
610004	MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA KILIMO CHA U/MAJI	3,328,000,000	192,000,000	6	3,858,000,000
610007	MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE				64,800,000
610008	MRADI WA KUKUZA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO	160,000,000	161,183,880	101	-
610014	PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO (*ASDP-L*)	828,155,000	197,615,670	24	346,886,000
610015	PROGRAMU YA KUIMARISHA HUDUMA YA KILIMO(*ASSP*)	518,881,000	138,452,200	27	-
660004	THAMANI NA MISAADA VIJIJINI (*MIVARF*)	9,348,560,000	245,064,800	3	3,008,416,000
610020	KATI INFRASTRUCTURE	178,402,000	178,400,000	100	178,400,000
610019	PROGRAM YA MWANZO BORA	30,000,000	31,251,524	104	-
610021	MPANGO WA ULIMWENGU WA KUSAIDIA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA (GAFSIP)	1,200,000,000		-	570,500,000
	JUMLA	**16,191,998,000**	**1,529,959,074**	**9.4**	**8,111,002,000**

Kiambatanisho Na. 5: PROGRAMU YA KUENDELEZA HUDUMA ZA KILIMO (*ASSP*)

MWAKA ILIOANZA: Programu ilianza mwezi Januari mwaka 2007.

Gharama Mwaka 2013/2014: Programu iliombewa Tsh. 55,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 518,881,000 kutoka *IFAD*. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Tsh. 43,000,000. Na. Tsh. 138,452,200 kutoka *IFAD*.	
Malengo 2013/2014	**Utekelezaji**
Kuendelea kuimarisha kazi za utafiti, tathmini na ufuatiliaji katika maeneo ya wakulima.	Programu imeweza kusaidia kufanya utafiti juu ya kusambaa kwa magonjwa ya kiwele kwa ng'ombe wa maziwa. Kazi za ufuatiliaji na tathmini katika maeneo ya wakulima zilifanyika kwa kushirikiana na maafisa wa programu wa wilaya.
Kutoa mafunzo ya uzalishaji mbegu bora kwa vikundi vya uzalishaji mbegu.	Programu imetoa mafunzo kwa wakulima 40 juu ya njia bora za uzalishaji wa mbegu bora ya mpunga.
Kutayarisha ripoti ya kumalizika kwa programu.	Ripoti ya kumaliza programu haikuandikwa kutokana na ushauri wa *IFAD* kwamba ripoti za programu zote mbili ziandikwe kwa pamoja baada ya kumalizika kwa programu za *ASDP-L*.
Ununuzi wa mashine ya usarifu wa zao la muhogo.	Mashine mbili zimenunuliwa.
Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya wakulima.	Tathmini imefanyika.
Kutoa elimu kwa wakulima.	Elimu imetolewa kwa mizunguko 20 Unguja na 10 Pemba kwa mshamba darasa 168 Unguja na 132 Pemba.
Programu hii imemalizika mwezi wa Machi 2014	

Kiambatanisho Na. 6: PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA MIFUGO (*ASDP-L*)

MWAKA ULIOANZA: Programu ilianza mwezi Januari mwaka 2007.

Gharama Mwaka 2013/2014: Programu iliombewa Tsh. 35,000,000 kutoka SMZ na Tshs 828,155,000 Kutoka *IFAD*. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana kutoka serikalini ni Tsh. 24,190,000 na Tsh. 197,615,670 kutoka *IFAD*.	
Malengo 2013/2014	**Utekelezaji**
Kununua mashine 3 za kutotolea vifaranga na mashine 5 za kusarifu maziwa kwa ajili ya wafugaji.	Mashine hizo hazikununuliwa kutokana na uhaba wa fedha.
Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo na ufugaji bora kwa vikundi 300 vya awamu ya nne	Programu imewezesha skuli 300 za Wakulima na wafugaji za awamu ya nne kwa kuendelea na mafunzo ambayo yamewezesha skuli hizo kuongeza uzalishaji wa mazao maradufu.
Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo na mifugo kwa vikundi 180 vya awamu ya tatu.	Mafunzo kwa vikundi 180 vya awamu ya tatu vya Unguja na Pemba. yametolewa. Taaluma hiyo imewezesha kuongeza uzalishaji kwa asilimia 53 ya wanavikundi, asilimia 24 wameongeza kipato na asilimia 16 ya wanavikundi wamekuwa na uhakika wa chakula.
Kuwapatia mafunzo msasa ya siku kumi watoa huduma za msingi za mifugo 40.	Mafunzo msasa kwa watoa huduma za msingi za mifugo 43 yalitolewa. Watoa huduma hao wamepunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa madaktari wa mifugo vijijini. Asilimia 59 (Unguja) na 17 (Pemba) ya wafugaji wamekiri kunufaika na watoa huduma hao.
Kuwapa mafunzo wawezeshaji kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, kilimo mseto na uhifadhi wa malisho ya n'gombe.	Mafunzo hayo hayakufanyika kutokana na uhaba wa fedha.
Kufanya utafiti,ufuatiliaji na tathmini wa athari za utekelezaji wa programu (*Impact ssessment*)	Hududi rejea za kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu zimetayarishwa na kuwasilishwa kwa maelekezo na kupata ridhaa ya *IFAD*.
Kutayarisha vipindi kwa njia ya video kuhusu utekelezaji na mafanikio ya skuli za wakulima.	Jumla ya vipindi vinne kuhusu utekelezaji na mafanikio ya skuli za wakulima vimetayarishwa.
Kuandaa mapendekezo ya kuendelea na kazi za programu kwa awamu ya pili.	Rasimu imeandaliwa na imo katika hatua ya kuipeleka kwa mashirika ya Kimataifa kwa kupata ufadhili.
Ununuzi wa chanjo ya maradhi ya vibuma (*ECF*).	Dozi 900 zimenunuliwa na kukabidhiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.
Kusaidia uwekaji wa mitambo 10 ya Biogas Unguja na Pemba.	Mitambo 10 (6 Unguja na 4 Pemba) imefungwa kwa wakulima/wafugaji.
Ununuzi wa mirija ya mbegu za majimaji za kupandishia ng'ombe.	Mirija 1000 ya mbegu za majimaji imenunuliwa.
Gharama mwaka 2014/2015: Programu inatarajia kupata Tsh. 30,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 346,886,000 kutoka *IFAD*.	
Malengo Kwa Mwaka 2014/2015 • Kuendelea kuvipa taaluma za ufugaji bora kwa vikundi 300 za skuli za wafugaji; • Kununua dozi 900 za chanjo ya maradhi ya vibuma (*ECF);* • Kununua mashine tatu za kutotolea vifaranga; na • Kuendelea kutayarisha vipindi kwa njia ya video kuhusu utekelezaji na mafanikio ya skuli za wakulima.	

Kiambatanisho Na. 7. Programu ya Miundombinu ya Masoko - *MIVARF*.

MWAKA Ilioanza: 2011/2012

Kwa mwaka 2013/2014 Programu iliombewa Tsh. 60,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 9,348,560,000 kutoka *IFAD/AfDB*. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Tsh. 9,000,000 na Tsh. 245,064,800 kutoka *IFAD/AfDB*	
MALENGO 2013/2014	**UTEKELEZAJI**
Kukarabati kilomita 100 za barabara za mashambani (*feeder roads*) kwa kiwango cha kifusi,	Ukarabati wa barabara haukufanyika kutokana na mabadiliko ya mpango wa manunuzi wa *AfDB* kwa mara ya pili kutoka "*Shopping"* kwenda "*National Competitive Bidding".* Mchakato wa mpango huo kwa sasa umefika pazuri kwa kupewa ruhusa (*No Objection*) katika mwezi wa Machi 2014 ya kutafuta wakandarasi kwa kazi hio;
Kujenga masoko matatu yenye vyumba vya baridi,	Ujenzi wa masoko haukufanyika kutokana na kutokamilika kwa hatua za kumpata mshauri muelekezi (*Consultant*) wa kutayarisha michoro ya masoko.
Ununuzi wa mitambo miwili ya kuzalisha barafu;	Ununuzi wa mitambo umeaghirishwa kabisa hadi majengo yanayotarajiwa kufungwa mitambo hio yakamilike. Majengo hayo ni soko jipya la samaki la Malindi linalotarajiwa kujengwa na Serikali ya Japan na Soko la Chake Chake linalotarajiwa kujengwa na Programu ya *MIVARF*;
Kuwawezesha watoa huduma na kuwaunganisha na masoko wazalishaji wadogo wadogo 2,500;	Utoaji wa mafunzo na kuwawezesha watoa huduma, kazi hizi zilitegemea watoa huduma kutoka sekta binafsi ambapo mchakato wa awali ulifikia hatua ya kufungiana mkataba na mtoa huduma (*GEODATA CONSULTANTS Ltd*), lakini ukatakiwa kurudiwa mchakato huo. Marudio ya mchakato huo yamefikia hatua ya kufungiana mkataba na mtoa huduma mwengine (*DELIGENT CONSULTING Ltd*) na inatarajiwa kuanza nae kazi katika robo ya April/Juni 2014;
Kuchangia kwa asilimi 75 ununuzi wa vifaa vya usarifu wa mazao;	Taasisi tatu tayari zimeshapitishwa kuweza kunufaika na utaratibu wa kuchangia kwa asilimi 75 ya ununuzi wa vifaa vya usarifu wa mazao (*JUWAFU* na *JUWAMIJICHWA* za Unguja na *WEMA Cooperative* ya Pemba) baada ya kukidhi vigezo vilivyotakiwa;
Kuwawezesha watoa huduma kuzijengea uwezo asasi ndogo ndogo za kifedha vijijini kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa mahitaji ya mafunzo;	Matokeo ya utafiti wa mahitaji ya mafunzo umekamilika na mchakato unaoendelea ni kuwapata watoa huduma kupitia mabenki ya kibiashara na kufanya kazi kwa majaribio (*Pilot*) katika zoni nne za Tanzania ikiwemo moja ya hapa Zanzibar;
Kuimarisha kitengo cha Microfinance cha Wizara ya Fedha na kuisaidia Idara ya Ushirika;	Afisa mmoja wa kitengo cha Microfinance amepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini Swaziland na pia kupelekwa ziara ya mafunzo nchini India. Idara ya Ushirika imeendelea kusaidiwa kulipia mafunzo ya maafisa wake watano katika ngazi ya Cheti na Diploma fani ya huduma za kifedha vijijini na uhasibu unaotumia teknohama. Pia, Idara ilipatiwa jumla Tsh. 50,000,000 ili kutekeleza mpango kazi wake uliopitishwa na Programu.
Gharama Mwaka 2014/2015**:** Programu inatarajiwa kupata Tsh. 60,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 3,008,416,000 kutoka *IFAD.*	

MALENGO KWA MWAKA 2014/2015

- Kujenga soko moja lenye chumba cha baridi;
- Kukarabati kilomita 148 za barabara za mashambani (*feeder roads*) kwa kiwango cha kifusi,
- Kutoa mafunzo ya utunzaji wa miundombinu ya masoko vijijini kwa wanajamii 100 na madiwani 20;
- Ununuzi wa vifaa vidogo vidogo vya usarifu wa mazao;
- Kutoa mafunzo ya uhifadhi na usarifu wa mazao;
- Kuwawezesha watoa huduma watakao toa huduma katika Wilaya za Zanzibar ili kuwajengea uwezo wazalishaji wadogo na kuwaunganisha na masoko;
- Kufanya warsha mbili kwa wadau za mapitio ya huduma za kifedha vijijini;
- Kusaidia Idara ya Ushirika pamoja na mpango kazi wake uliopitishwa na Programu;
- Kusaidia Wizara ya Fedha kukiimarisha kitengo cha Microfinance;
- Kununua vitendea kazi (Kompyuta) kufanikisha utendaji kazi wa Kamati za Programu za Wilaya; na
- Kuratibu Kazi za wadau wanaotekeleza Programu.

Kiambatanisho Na. 8: Mradi wa Usarifu wa Mazao ya Kilimo (*Agro-processing*)

Maelezo ya Mradi: Mradi huu ulitarajiwa kuwa ni wa miaka mitatu kuanzia Julai 2010/Juni 2013**.** **Gharama/Wachangiaji.** *KOICA*: *US $* 2.300 milioni (ambazo ni msaada) SMZ TSh 600 milioni. Hata hivyo, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu, wahisani wameshindwa kumalizia ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa Mazao huko Kizimbani ikiwa ni hatua za mwisho za utekelezaji wa Mradi huo. Hivyo, hivi sasa Wizara inaendelea na ujenzi wa Kituo hicho kwa kutumia fedha za msaada ***(budget support)*** zilizotolewa na *KOICA* pamoja na Bajeti ya Serikali. Vile vile, Wizara inaendelea kutafuta wafadhili wengine ili kukamilisha ujenzi huo.
Lengo kuu: Kujenga uwezo wa wakulima juu ya usarifu wa mazao na ujasiriamali pamoja na kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wazalishaji.
Gharama kwa mwaka 2013/2014: SMZ Tsh. 50,000,000 na kutoka kwa washirika wa maendeleo *KOICA* Tsh. 160,000,000. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Tsh. 50,000,000 na kutoka washirika wa maendeleo Tsh. 161,183,880
MALENGO YA MWAKA 2013/2014 i. Kumalizia ujenzi wa jengo pamoja na Ufungaji wa mitambo; na ii. Kutoa mafunzo ya usarifu wa mazao kwa wafanyakazi wanne (Unguja wawili na Pemba wawili) na wajasiriamali wanaosarifu mazao 100 (10 kwa kila Wilaya Unguja na Pemba).
Utekelezaji 2013/2014: • Kazi ya utiaji umeme, milango 14 ya ndani katika vyoo, ofisi na sehemu zote za jengo imekamilika; • Kazi ya ujenzi wa mfumo wa maji machafu (*sewage system*) imekamilika; • Kazi ya ujenzi wa mfumo wa maji masafi imekamilika; • Ukarabati wa paa la jengo na upakaji rangi magrills ya paa imekamilika; na • Jumla ya wajasiriamali 60 wamepatiwa mafunzo ya usarifu wa mazao na kuzuiya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa (*reduction of Post harvest losses*). Wajasiriamali hao hapo wanatoka katika wilaya sita za Unguja.
Gharama Mwaka 2014/2015: Programu inatarajia kupata Tsh. 100, 000,000 kutoka SMZ.
Malengo ya mwaka 2014/2015: • Kukamilisha ujenzi wa jengo la kituo cha usarifu wa mazao

Kiambatanisho. Na. 9: Mradi wa Uimarishaji Mikarafuu

Lengo kuu: Kuongeza pato la mkulima na Taifa kwa ujumla.

Malengo 2013/2014	**Utekelezaji**
Kwa mwaka 2013/2014 Mradi uliombewa Tsh.390,000,000 kutoka SMZ Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana ni Tsh. 175,619,815.	
Kuzalisha miche 1,000,000 ya mikarafuu na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo.	Jumla ya miche ya mikarafuu 941,176 imeoteshwa, sawa na asilimia 94.1, kati ya hiyo miche 309,640 imeoteshwa Unguja na miche 631,536 imeoteshwa kisiwani Pemba.
Ujengaji na ukarabati wa mabanda ya kuoteshea miche katika vitalu vya Selem, Machui, Mwanakombo kwa Unguja na Weni, Mkatamaini na Chanjaani kwa Pemba.	Ujenzi wa mabanda mawili ya kudumu katika vitalu vya Ole – Pemba, na Machui – Unguja umekamilika na kazi za ukarabati wa mabanda ya kuoteshea miche katika vitalu vya Selem, Machui, Mwanakombo kwa Unguja na Weni, Mkatamaini na Chanjaani kwa Pemba zimefanyika.
Kufanya tathmini ya miche ya mikarafuu iliopandwa na kumea katika msimu uliopita.	Tathmini ya uotaji wa mikarafuu iliopandwa katika msimu wa 2012/13 imefanyika Unguja na Pemba. Wastani wa uotaji kwa nchi nzima ni asilimia 52.85. Kwa upande wa Unguja ni asilimia 54.20 na kwa Pemba ni asilimia 51.49.
Kutoa Elimu ya utunzaji wa mikarafuu kwa wakulima 350 katika Wilaya 7 za Unguja na Pemba na kuanzisha mashamba darasa.	Mafunzo kwa wakulima mikarafuu 100 wa Unguja na Pemba 200 yametolewa. Mashamba darasa 21 yameanzishwa (8 Unguja na 13 Pemba). Jumla ya Kilo 50 za polythene zimegawiwa kwa wakulima wa karafuu ikiwa ni jitihada za kuimarisha uzalishaji.
Kuhamasisha upandaji wa mikarafuu katika Wilaya 7 za Unguja na Pemba (Upandaji wa Mikarafuu Kitaifa.	Upandaji wa mikarafuu kitaifa umefanyika katika Wilaya ya Wete ambapo Mikarafuu 1,200.
Kupima na kuchora ramani za mashamba 100 ya mikarafuu pamoja na kuyasafisha.	Kazi hii haikuweza kutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha.

Gharama Mwaka 2014/2015: Mradi unatarajiwa kupata Tsh. 300,000,000 kutoka SMZ

Malengo ya mwaka 2014/2015

- Kuzalisha miche 1,000,000 ya mikarafuu na kuigawa kwa wakulima bila ya malipo;
- Kujenga na kukarabati mabanda ya kuoteshea miche katika vitalu vya Selem, Mwanakombo kwa Unguja na Weni, Mkatamaini na Chanjaani kwa Pemba;
- Kufanya tathmini ya miche ya mikarafuu iliopandwa na kumea katika msimu uliopita;
- Kutoa elimu ya utunzaji wa mikarafuu kwa wakulima 350 katika Wilaya 7 za Unguja na Pemba na kuanzisha mashamba darasa;
- Kuhamasisha upandaji wa mikarafuu katika Wilaya 7 za Unguja na Pemba (Upandaji wa Mikarafuu Kitaifa, Vipindi vinane vya redio na *TV*, Mikutano 8 ya wadau); na
- Kupima na kuchora ramani za mashamba 100 ya mikarafuu pamoja na kuyasafisha.

Kiambatanisho. Na. 10: Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili (*HIMA*)

Lengo kuu: Kupunguza Hewa ukaa kutokana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu.

Malengo 2014/2015	**Utekelezaji**
Kwa mwaka 2013/2014 Mradi uliombewa Tsh. 35,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 250,000,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana ni Tsh. 25,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 215,991,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo.	
Kutayarisha mpango wa kuongeza maeneo ya uhifadhi misitu ya wanajamii.	Maeneo 12 ya uhifadhi wa Misitu ya Jamii ya wanajamii yalitayarishiwa mipango ya uhifadhi na kufanya idadi ya maeneo yote ya uhifadhi ya wanajamii kufikia 5, ikiwa Unguja 33 na Pemba 24.
Kutoa gesi ya kupikia bila ya malipo kwa kaya 4,000 za Unguja (2000) na Pemba (2000) pamoja na kuelimisha matumizi salama ya gesi.	Jumla ya kaya1,242 zimepatiwa gesi ya kupikia bila malipo (Unguja 492 na Pemba 750). Gesi hiyo hugawiwa katika mitungi yenye ujazo wa kilo 6 na 15. Lengo la kugawa gesi ni kupunguza uharibifu wa misitu asili hapa nchini.
Kutengeneza Tovuti itakayohusiana na Masuala ya *MKUHUMI*.	Tovuti ya *MKUHUMI* inayosomeka (*www.forestryznz.or.tz*) imetengenezwa na kurushwa kwenye mtandao na kazi ya uwekaji taarifa katika tovuti hiyo inaendelea.
Gharama Mwaka 2014/2015: Programu inatarajia kupata Tsh. 84,000,000 kutoka NORWAY.	
MALENGO 2014/2015 • Kuzijengea uwezo kamati 57 za uhifadhi ili waweze kutekekeleza mipango ya matumizi ya rasilimali za misitu kwa ufanisi; • Kuzitathmini kamati 45 za uhifadhi jinsi wanavyo tekeleza mipango ya matumizi ya rasilimali za misitu kwa ufanisi; • Kutayarisha mipango 16 ya maeneo ya uhifadhi ya matumizi ya rasilimali za misitu; • Kuhamasisha jamii kupanda miti ya misitu ya asili katika wilaya 7 zinazo fanyiwa kazi na mradi; • Kutoa taaluma ya uanzishaji vitalu na upandaji wa miti ya misitu kwa wakulima wenye vitalu binafsi 100; • Kutoa taaluma za mbinu mbadala kama vile ufugaji nyuki katika wilaya 7 zinazafanyiwa kazi na mradi; na • Kuhamasisha kilimo mseto (*Agroforestry*) katika maeneo ya maweni.	

Kiambatanisho. Na. 11: Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani

Malengo 2013/2014	**Utekelezaji**
Kwa mwaka 2013/2014 Mradi uliombewa Tsh. 35,000,000/- kutoka SMZ na Tsh. 350,000,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana ni Tsh. 22,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 170,000,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo.	
Kukamilisha taratibu za kupandisha hadhi hifadhi mpya ya Muyuni – Jambiani yenye ukubwa wa eneo la hekta 4,214.	Kazi hii imetekelezwa na imefikia hatua ya kutayarisha hati ya mwisho ya kulitangaza eneo la msitu wa Jambiani-Muyuni (*Final Reserve Order*) kuwa eneo la Hifadhi rasmi. Aidha mipaka ya hifadhi hiyo imewekwa vigingi vya kudumu, kazi ambazo imefanywa kwa mashirikiano na wananchi wanaoishi karibu na msitu huo.
Kuanza taratibu za kupandisha hadhi msitu wa Ufufuma Pongwe – Unguja na Kangagani – Pemba.	Rasimu ya tangazo la azma ya kulitangaza eneo la msitu wa Ufufuma -Pongwe kuwa eneo la Hifadhi (*Notice of Intent*) imekamilika. Aidha kazi ya upimaji na uchoraji wa ramani imekamilika. Eneo lote la msitu wa Ufufuma-Pongwe lenye ukubwa wa hekta 1,988.38 limewekewa mipaka.
Kuweka mipaka ya kudumu (*beacons*) katika Msitu wa Muyuni Jambiani.	Jumla ya hekta 4,200 za Hifadhi ya Msitu wa Jambiani-Muyuni zimewekewa mipaka ya kudumu kwa kutumia vigingi (*Beacons*) 420 kuzunguka eneo lote.
Kutayarisha Mipango ya Uendeshaji (*Management Plan*) kwa Misitu ya Jambiani - Muyuni, na Msitu wa Ufufuma Pongwe na Kangagani.	Matayarisho ya mipango ya uendeshaji wa maeneo ya hifadhi yameanza kwa kuwateuwa mameneja wa Hifadhi hizo. Aidha muundo wa usimamizi na uendeshaji kazi (*Management Organization charts*) umekamilika.
Kuunda Bodi ya Kitaifa ya usimamizi wa Maeneo ya Uhifadhi kwa kufanya mikutano ya uzinduzi na Wajumbe kutembelea maeneo ya Uhifadhi Unguja na Pemba.	Muundo wa Bodi ya Kitaifa ya Maeneo ya Uhifadhi umefikia hatua ya kuandaa kanuni za uendeshaji ambazo zimepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuzipitia na kupata muongozo.
Mradi huu umemalizika mwezi wa Machi 2014.	

Kambatanisho Na. 12: Mradi wa Kuangamiza Adui Kunguru:

Lengo mahsusi: Kuangamiza kuguru 400,000 kwa kutumia sumu na mitego.

MALENGO 2013/2014	**UTEKELEZAJI**
Kwa mwaka 2013/2014 Mradi uliombewa Tsh. 20,000,000 kutoka SMZ. Hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana ni Tsh. 10,000,000.	
Kununua sumu ya kuulia kunguru kilo 3.	Hakuna sumu iliyonunuliwa kwa kipindi cha mwaka 2013/14 na badala yake bado imeendelea kutumika sumu iliyonunuliwa mwaka 2012/2013.
Ununuzi wa chambo cha kutegea kunguru na vitendea kazi.	Jumla ya kilo 200 za nyama kwa ajili ya chambo zimenunuliwa na kuchanganywa na sumu kwa lengo la katika kazi ya kuuwa kunguru. Aidha,vitendea kazi vilinunuliwa vikiwemo (ndoo 100, miko 100 na glavu 100).
Kuelimisha jamii kwa njia ya vipindi 10 vya redio / *TV*, mikutano na vijarida.	Jumla ya wananchi 15,000?? Wame elimishwa na kuhamasishwa kushiriki katika kazi ya kuwauwa kunguru (Pemba 729 na Unguja 14,271). Mkutano mmoja wa kutoa elimu ya kuwahamisha kuwatokomeza kunguru ulifayika na kuwashirika wafanyakazi 27 wa Baraza la Mji wa Zanzibar. Aidha, matangazo kwa njia ya *Radio* yametolewa kupitia *ZBC* ambapo kipindi 1 cha radio cha dakika 15 kimerushwa hewani kwa njia ya redio. Idadi ya kunguru waliouliwa hadi mwezi Machi 2014 imefikia 38,878 (Unguja 23,000 na Pemba 15,878).
Ushirikishwaji wa wanajamii katika Shehia zote za Unguja na Pemba ili kufanikisha kazi ya uangamizaji kunguru.	Mkutano wa kuelimisha wananchi wa kisiwa cha Tumbatu kupitia viongozi wa Shehia zote tatu umefanyika. Aidha, mkutano na viongozi wa Visiwa vya Bawe na Changuu umefanyika pamoja na kuwapatia viongozi hao sumu ya kuulia kunguru katika visiwa hivyo. Pia, wananchi wa Bopwe, Micheweni, Mbuyuni, Tibirinzi, Uwandani, Selem na Vitongoji wameshirikishwa katika mpango wa kuwauwa kunguru kwa kuwapatia taaluma.
MALENGO 2014/2015. • Kununua sumu ya kuulia kunguru kilo tano (5); • Kununua kilo (800*kgs*) za nyama kwa ajili ya chambo cha kutegea kunguru. • Kuifanyia matengenezo mitego 20 ya kunasia kunguru; • Kuendelea kusambaza elimu ya kuwauwa kunguru kwa njia mikutano na vyomvo vya mawasiliano; na • Kushirikiana na wenye mahoteli pamoja na kambi za kijeshi kwa lengo la kumtokomeza adui kunguru.	

Kiambatanisho Na.13: Programu ya Lishe ya Mwanzo Bora.

Programu: hii ni ya miaka mitano na imeanza 2009 **Gharama :** *USD* 15 Milioni, Wachangiaji: SMZ, na *USAID.*
Lengo kuu la Programu ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umaskini wa chakula na kipato kukabiliana na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za Taifa, jamii na kaya na kushajiisha ushiriki wa jamii katika hatua za kujiongezea k ipato.
Gharama Mwaka 2013/2014: Programu iliombewa Tsh. 30,000,000 kutoka MWANZO BORA, hadi kufikia Mei, 2014 fedha zilizopatikana kutoka ni Tsh. 31,251,524.
Utekelezaji 2013/2014: • Vikundi vinane vya kina mama (*Mother to Mother Support Groups*) vimeanzishwa na kupatiwa mafunzo juu ya lishe bora. (Unguja – Shehia za Kijini, Kidoti, Tazari na Mchezashauri, Pemba-Shehia za Tumbe Magharibi na Mashariki, Pujini na Mbuzini) aidha uundaji mwengine wa vikundi katika shehia 37 umeanza kwa mikutano ya awali ya uundaji wa kamati za uhakika wa chakula na lishe zenye wajumbe 15, kazi hii inaendelea na hadi sasa shehia 16 (Unguja 8 na Pemba 8) zimeshapitiwa; • Makabrasha ya mawasiliano juu ya masuala ya lishe (*Social Behavioral Communication Change - Kit*) yametayarishwa kutoa muongozo juu ya utowaji wa taarifa za lishe kwa jamii. Kazi hii bado inaendelea; • Uanzishwaji wa siku ya afya katika shehia kwa shehia 8 za Unguja 4 na Pemba 4; na • Jumla ya bustani za mfano 6 za mbogamboga zilianzishwa (Unguja – shehia za Kijini, Kidoti, Tazari na Kilimani, Pemba-Shehia za Pujini na Mbuzini) zimetayarishwa kwa lengo la kutoa elim kwa jamii juu ya bustani ndogo ndogo na kushawishi wananchi kuanzishwa bustani kama hizo katika maeneo yao.
Gharama Mwaka 2014/2015: Programu inatarajiwa kupataTsh. 160,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 64,800,000 kutoka kwa *USAID.*
Malengo Mwaka 2014/2015: • Kukamlisha makabrasha ya mawasiliano juu ya masuala yalishe (*Social Behavioral Communication Change - Kit),* kuchapisha na kuanza matumizi ya makabrasha; • Kuanzisha vipindi vya radio na kutoa machapisho juu ya masuala ya lishe kwa jamii; • Kushajiisha na kusaidia uanzishwaji wa bustani za nyumbani katika shehia 37 za Wilaya za Kaskazini A, Chakechake na Micheweni; • Kuanzisha vikundi vya kina mama (*mother to mother/father to father support groups*) na kupatiwa mafunzo juu ya lishe bora katika shehia 45 za wilaya 3; • Kuanzisha kamati za uhakika wa chakula katika Shehia 37 za Wilaya za Kaskazini A, Chake chake na Micheweni; na • Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya, sita kutoka wodi ya wazazi na sita kutoka PHCUs kwa vituo vitatu Unguja na vitatu Pemba katika *IYCFP*

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhudu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba uniruhusu kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, Mwingi wa Rehema na mwenye kurehemu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu yetu mbali mbali ya kuwatumikia wananchi wetu, ambapo leo tunajadili Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, shukurani zangu za dhati pia zije kwako kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kutoa muhutasari wa maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu

makadirio ya mapato na matumzi kwa mwaka wa fedha 2014/15, ambayo punde hivi Mhe. Kaimu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, amewasilisha mbele yetu.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii pia kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Mhe. Waziri, Kaimu Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili, pamoja na watendaji wote wa wizara hii, kwa jitihada wanazozionesha katika kutekeleza majukumu yao na kushirikiana bega kwa bega na Kamati hii kila wanapohitajika kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Wajumbe na makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wa kuipitia bajeti ya wizara hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja kwa majina Wajumbe hao pamoja na makatibu wake kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hijja Hassan Hijja	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
5.	Mhe. Hamad Masoud Hamad	Mjumbe
6.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
7.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
8.	Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu
9.	Ndg. Haji Khatib Haji	Katibu

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha kwamba sekta ya kilimo bado inaendelea kuwa, ndio tegemeo kubwa kwa Uchumi wa Zanzibar. Ukuwaji wa sekta hii katika pato la Taifa kwa mwaka fedha 2013/2014, umeripotiwa kuongezeka na kufikia asilimia 31, ikilinganishwa na asilimia 30.2 ya mwaka 2012/2013. Aidha, takwimu pia zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hii kwa kujipatia ajira na kipato.

Mhe. Spika, pamoja na umuhimu mkubwa wa Sekta hii ya Kilimo kwa nchi yetu, bado uingizwaji wa fedha kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, kama ni msimamizi mkuu wa kuiendeleza sekta ya kilimo umekuwa si wa kuridhisha. Kamati imesikitishwa kuona kuwa hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014 mchango wa serikali kwa kazi za Maendeleo ni asilimia 29 tu na zile za Washirika wa Maendeleo zilizopatikana hadi kipindi hicho ni asilimia 9.4 tu ya lengo. Cha kusikitisha zaidi ni kuwa baadhi ya taasisi muhimu za wizara hii zimekosa kabisa fedha za Maendeleo, kwa kutoingiziwa fedha yoyote ya maendeleo kutoka serikalini.

Mhe. Spika, Kamati inaendelea kushangazwa sana na hali ya bajeti finyu ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, ambayo imepelekea utekelezaji wa kazi za wizara hii muhimu kuwa katika mazingira magumu. Hali hii imepelekea wananchi wengi ambao wanategemea huduma mbali mbali zinazotolewa na wizara hii kwa njia moja au nyengine, wakiwemo wakulima kukosa matumaini.

Mhe. Spika, pamoja na uingizwaji mdogo wa fedha kwa Wizara hii muhimu ya Kilimo na Maliasili, bado watendaji wa wizara hii wanaonekana kufanya kazi kwa bidii kubwa na maarifa. Jitihada za watendaji wa wizara hii zinaonekana wazi katika eneo la ukusanyaji wa mapato katika wizara hii. Taarifa zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi Tsh, 748,000,000, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2014, wizara ilikuwa imeshakusanya shillingi Tsh.856,180,640, sawa na asilimia 114 ya makadirio ya lengo.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huu, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inapenda kutoa pongezi za dhati kwa watendaji wa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili, kwa mafanakio hayo makubwa ya kuweza kuvuka lengo la makusanyo ya mapato. Kamati inawataka watendaji wa Wizara hii kuzidisha bidii ya kufanya kazi, ili mapato ya serikali kupitia wizara hii yaweze kukua zaidi kwa mwaka ujao wa fedha wa 2014/2015.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma katika wizara, ikiwa pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Kwa muktadha huu, Kamati

inaipongeza wizara kwa kufanikisha upatikanaji wa ajira 60, zikiwemo za mabwana na mabibishamba 45 na 15, hadi kada nyenginezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, pamoja na kufanikiwa kuajiri wafanya kazi hao 60, Kamati inaona bado wizara hii inaendelea kukabiliwa na tatizo la upungufu wa wafanyakazi wa kada mbali mbali, wakiwemo mafundi, walinzi, mabwana na mabibishamba pamoja na kada nyengine za kitaalamu. Kamati ilisikitishwa kupata taarifa kuwa kutokana na upungufu wa wafanyakazi, ilipelekea baadhi ya maafisa Kilimo kufanya kazi za ulinzi hususan kisiwani Pemba. Aidha, pamoja na kuwepo kwa upungufu wa mabwana na mabibi shamba, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wakulima, kuwa hata hao mabwana na mabibishamba wachache waliopo hawaonekani ipasavyo katika Shehia walizopangiwa.

Mhe. Spika, kutokana na hali zote hizo, Kamati inasisitiza wizara kuendelea kulivalia njunga, suala la upatikanaji wa ajira za wafanyakazi wa kada mbali mbali, ili kuweza kupunguza tatizo hili sugu la uhaba wa wafanayakzi katika wizara. Aidha, Kamati inaisihi Wizara kuendelea na mpango wake wa kuzitumia skuli za wakulima kutoa taaluma ya kilimo bora kwa wakulima, ili angalau kuweza kupunguza pengo lililopo la uhaba wa mabwana na mabibishamba, ambao wanahitajika sana katika kuwasaidia wakulima wetu.

IDARA YA KILIMO

Mhe. Spika, kama inavyofahamika kuwa Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za Kilimo kwa wakulima, pamoja na uhifadhi na ukaguzi wa mazao na utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa kuwa miongoni mwa malengo yaliyotekelezwa na Idara hii, pamoja na kuwezeshwa kuvuna kwa tani 40 za mbegu ya mpunga aina ya *NERICA.* Pamoja na nia nzuri ya serikali ya kuwaletea wakulima wake mbegu hiyo mpya ya mpunga aina ya *NERICA,* bado kiwango cha upatikanaji wa mchele unaotokana na mbegu hiyo kimekuwa ni tofauti na matarajio ya wananchi. Aidha, taarifa ambazo zimetolewa na wizara hazioneshi idadi ya wakulima wanaojitokeza kutumia mbegu hiyo, pamoja na tathmini ya kina juu ya ufanisi wa mbegu hiyo, iliyotangazwa kwa mapana kuwa ni mbegu ambayo ingewakomboa wakulima wa mpunga pamoja na wananchi wetu katika upatikanaji wa chakula kinachozalishwa hapa nchini.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri wizara kufanya utafiti wa kina, ili kujua sababu zilizopelekea wakulima wetu kutoitumia ipasavyo mbegu hii waliyoletewa na serikali kwa matumaini makubwa. Aidha, Kamati inaishauri wizara pamoja na serikali kwa ujumla kufanya utafiti wa kina juu ya faida na hasara wanazoweza kupata wakulima wetu kulingana na hali na mazingira yao, kutokana na matumizi ya aina mpya ya mbegu zinazoingizwa hapa nchini.

Mhe. Spika, moja kati ya malengo ya Idara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ilikuwa ni kudhibiti maradhi ya mimea na wadudu waharibifu wa mazao, ambapo imeelezwa kuwa mafunzo juu ya udhibiti wa wadudu waharibifu katika mazao ya mboga yalitolewa kwa wakulima 51. Aidha, iliarifiwa udhibiti wa viwavijeshi ulifanyika kwa kusambazwa lita 100 katika mashamba ya mpunga yalioshambuliwa na wadudu hao katika Wilaya ya Kati na Kaskazini 'B".

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo za wizara za kudhibiti maradhi ya mimea na wadudu waharibifu wa mazao, bado wakulima wamekuwa wakilalamika sana kuhusu tatizo hilo la kuharibika kwa mazao yao yakiwemo muhogo na machungwa. Hivyo, Kamati inaitaka wizara kuzidisha juhudi zake za kutoa elimu kwa wakulima wengi zaidi wa mazao mbali mbali, pamoja na kuwahamasisha wakulima kutumia dawa zinazopendekezwa na wataalamu wa kilimo, ili kuepusha kupata hasara inayotokana na maradhi ya mimea na wadudu waharibifu wa mazao.

Mhe. Spika, katika mkutano wa Kumi na Tano wa Baraza lako tukufu, uliofanyika mwezi wa Januari mwaka huu wa 2014, ambao ulijadili ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza, Kamati iliripoti kuwepo kwa deni kubwa la Tsh millioni 240, lililokuwa inadaiwa wizara na wakulima wa mikataba wanaozalisha mbegu za mpunga katika mabonde mbali mbali likiwemo Bonde la Mtwango. Kamati imefarajika kidogo baada ya kuelezwa kuwa baadhi ya wakulima hao wamelipwa fedha zao. Hata hivyo, wakati Kamati ilipokuwa katika kazi zake za kawaida mwanzoni mwa mwezi wa Mei 2014, iliarifiwa kuwa bado walikuwepo wakulima katika mabonde mbali mbali ambao hawajalipwa

fedha zao zipatazo Tsh millioni 106. Deni ambalo lilitarajiwa kulipwa ndani ya mwezi wa Mei 2014, baada ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kuingiziwa fedha kutoka Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, inahoji na kutaka kujua hatma ya deni hilo la wakulima wanaozalisha mbegu za mpunga iwapo limelipwa. Iwapo deni hilo halijamaliza kulipwa hadi hii leo, Kamati inaiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuhakikisha kuwa inaingizia fedha Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa ajili ya kulipa deni hilo kwa wakulima, na hivyo, kuwaondoshea dhiki wanayoendelea kuipata wakulima hao wanyonge wanaozalisha mpunga wa mbegu hapa nchini. Aidha, Kamati inaisihi sana serikali kutowaongezea dhiki na kutowavunja moyo wakulima wetu, kwa kutowalimbikizia madeni kwa muda mrefu, madeni wanayoidai serikali, kwani fedha hizo ndizo wanazozitegemea katika kujikimu kimaisha.

Mhe. Spika, Idara hii ya Kilimo ndio kiini cha wizara hii kwa kuwa imebeba majukumu makuwa ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima, uhifadhi na ukaguzi wa mazao na kutoa mafunzo kwa wazalishaji.

Mhe. Spika, pamoja na umuhimu mkubwa iliyonayo Idara hii, Kamati inaona bado baadhi ya vitengo vya Idara hii havifanyi kazi ipasavyo, kutokana na changamoto mbali mbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi. Moja kati ya vitengo muhimu vinavyokabiliwa na changamoto hizo ni kituo cha uzalishaji mbegu, Bambi ambapo Kamati ilishangazwa kuona kuwa kituo hicho kinakabiliwa na ukosefu wa bomba za kumwagilia dawa za mimea ambazo gharama yake ni ndogo. Hivyo, Kamati inaiomba wizara ipange vizuri vipaumbele vyake katika matumizi pindi inapoingiziwa fedha, kwa kufanya manunuzi ya nyenzo muhimu zilizo bei rahisi ili kuondoa usumbufu wa kiutendaji usio wa lazima.

Mhe. Spika, wazalishaji na wawekezaji katika sekta ya kilimo kutoka nje ya nchi wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya kilimo na viwanda katika nchi mbali mbali duniani, kwa mfano katika nchi ya Kenya wawekezaji kutoka nje ya nchi wamekuwa wakipewa ardhi na serikali ili kuanzisha miradi mbali mbali ya viwanda inayotumia mazao ya wakulima nchini humo. Miradi hii imekuwa ikiwasaidia sana wakulima wadogo wadogo wakiwemo wa mboga mboga na maua, kwa kuipatia soko la uhakika kwa bidhaa zao, wakulima ambao hushirikiana moja kwa moja na wawekezaji *Outgrowers,* kwa ajili ya kuzalisha mazao ya kilimo na kupatiwa utaalamu wa kuzalisha mazao yanayohitajika katika soko. Huu ni mfano bora wa kuigwa na serikali yetu ili kuwaendeleza wakulima wetu na kuimarisha sekta ya kilimo kwa ujumla.

Mhe. Spika, ni wazi kuwa wawekezaji hao wanapowekeza ndani ya nchi yetu, husaidia kwa kuinua kipato cha wakulima na kukuza pato la serikali kwa asilimia kubwa, pamoja na kutoa fursa za ajira kwa wananchi wetu. Pamoja na hayo, kuwepo kwa wawekezaji hao hupelekea bidhaa zetu kutambulika katika soko la ndani, la kikanda na la Kimataifa.

Mhe. Spika, kutokana na hali hii, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, inaiomba serikali kulipa uzito unaostahili suala hili, kwa kuwapatia sehemu ya ardhi wawekezaji wenye nia njema ya kuwekeza katika miradi hii ya kilimo, ili kuweza kuwanufaisha wakulima wetu wadogo wadogo na kutuletea maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe. Spika, Kamati imefarijika sana kuona kuwa katika bajeti ya 2013/2014, kazi ya kumpata mkandarasi kwa mradi wa miundombinu ya umwagiliaji maji kupitia mkopo wa *Exim Bank* ya Korea imekamilika. Huu ni mradi muhimu na mkubwa unaokadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani millioni 50. Kamati ina matumaini makubwa kuwa mradi huu utawakomboa wakulima na wananchi wetu kwa ujumla, kutokana na kilimo duni cha kutegemea mvua na kuingia katika kilimo cha kisasa cha umwagiliaji maji na hivyo kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mpunga hapa nchini.

Mhe. Spika, pamoja na matumaini hayo kwa mradi huu mpya wa umwagiliaji maji, Kamati inatoa indhari kuwa ni vyema kwa viongozi na watendaji wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, hususan katika Idara hii ya Umwagiliaji Maji kuwa waangalifu sana katika utekelezaji wa mradi huu, kwani uzoefu unaonesha kuwa utekelezaji wa miradi mikubwa na mipya kama hii hapa nchini huwa unakumbwa na mashaka na changamoto nyingi.

IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Mhe. Spika, moja kati ya malengo ya Idara hii kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, ni kukarabati ghala moja la Hifadhi ya Chakula lililopo Unguja. Kamati imesikitishwa sana kuona kuwa kazi hiyo ya kukarabati ghala hilo la Hifadhi ya Chakula imeshindwa kufanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Aidha, ni jambo la kusononesha kabisa kuona kuwa Idara hii haijaingiziwa fedha yoyote kwa ajili ya kazi za maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, iliidhinishiwa Tsh 160 millioni kwa jili ya kazi hizo. Kamati inahoji uko wapi uhakika wa chakula iwapo itatokea hali ya nchi isiyotarajiwa wakati ghala la Hifadhi Taifa ya Chakula linashindwa kutengenezwa na kufanyakazi.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imeliweka tena lengo hili la kukarabati ghala la Hifadhi ya Taifa ya Chakula lililopo Unguja. Kwa mnasaba huu, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaitaka serikali kufanya kila italoweza kuhakikisha kuwa Tsh 160 millioni ambazo zinazotengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo za Idara hii zinaingizwa kikamilifu, ili ukarabati wa ghala hilo uweze kufanyika, kwani ni aibu kwa serikali kushindwa kuingiza Tsh 160 millioni kwa ajili ya jambo hili muhimu la ukarabati wa ghala la Hifadhi ya Taifa ya Chakula.

IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Spika, jukumu kubwa la Idara hii ni kulinda na kuhifadhi misitu ya asili na wanyama pori, kusimamia mashamba ya misitu na mbegu, upatikanaji wa miche bora pamoja na kuratibu uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Spika, kwa kuwa sehemu kubwa ya utekelezaji wa majukumu ya Idara hii inahitaji ushirikishwaji mzuri wa wanajamii hasa walioko vijijini. Kamati inaomba wizara kuzidisha juhudi za kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi misitu ikiwa ni pamoja umuhimu wa kupanda miti na athari za kukatwa miti ovyo ikiwemo katika sehemu za ukanda wa pwani.

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO

Mhe. Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kupanga na kutekeleza kazi za utafiti katika Sekta za Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaipongeza wizara pamoja na Uongozi wa Taasisi hii ya Utafiti wa Kilimo kwa kukamilisha ujenzi wa maabara mpya ya utafiti wa mpunga na ukarabati wa maabara za udongo na usarifu wa mazao. Hata hivyo, pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa maabara hiyo mpya ya utafiti wa mpunga, Kamati imeona kuwa maabara hiyo inakabiliwa na ukosefu wa samani (*furniture*) ambazo upatikanaji wake bado haujawa wa uhakika kutokana na uhaba wa fedha. Hivyo, Kamati inaishauri wizara pamoja na taasisi hii kuliangalia kwa uzito unaostahili suala hilo la upatikanaji wa samani, ili kutozorotesha utendaji katika maabara hiyo mpya.

Mhe. Spika, nchi nyingi zilizoendelea katika Sekta ya Kilimo zimekuwa zikitoa kipaumbele katika masuala ya utafiti wa kilimo pamoja na kuzipatia vifaa na utaalamu wafanyakazi wa Taasisi za Utafiti wa Kilimo. Katika muktadha huu, Kamati imesikitishwa sana kuona kuwa hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, taasisi hii imeingiziwa Tsh millioni 10 tu sawa na asilimia 7 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kazi za maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ilitengewa jumla ya Tsh 140 millioni kutoka serikalini.

Mhe. Spika, Kamati inaona kuwa hakuna utafiti wowote wa maana unaoweza kufanyika kwa kuingizia taasisi hii muhimu asilimia finyu sana ya fedha kama hii. Aidha, Kamati inaona pia kuwa kwa utaratibu huu wa kuingizia bajeti finyu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Taasisi nyengine muhimu za wizara hii, ile kauli mbiu ya serikali ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini itakuwa ni ndoto tu kwani maendeleo katika sekta ya Kilimo huchangiwa sana na tafiti za kina katika sekta hii.Hivyo, Kamati inaisihi sana serikali kuwa iwapo inataka kuleta maendeleo ya Kilimo hapa nchini haina budi kuachana na kauli mbiu za maneno matupu na badala yake kutoa kipaumbele kwa vitendo katika masuala ya utafiti wa Kilimo kwa kuingiza fedha za kutosha katika taasisi hii ya utafiti pamoja na taasisi nyengine muhimu za wizara hii kwani maendeleo ni gharama.

Mhe. Spika, katika maabara ya Matangatuani, Pemba, Kamati imepata faraja kuona kuwa katika mwaka huu wa fedha wa 2014/2015, wizara ina mpango kabambe wa kutaka kuiimarisha kwa kuifanyia ukarabati, pamoja na mambo mengine maabara hiyo. Ukweli ulio wazi kuwa kwa muda mrefu, sasa maabara hiyo imekuwa katika hali

mbaya na kukosa hadhi ya kuitwa maabara kwa kukosa hata vifaa vidogo vidogo tu vinavyotakiwa kuwepo katika maabara.

CHUO CHA KILIMO, KIZIMBANI

Mhe. Spika, kama inavyofahamika kuwa Chuo cha Kilimo Kizimbani kina jukumu la kutoa utaalamu katika fani za Kilimo, Maliasili na Mifugo katika ngazi tofauti. Aidha, ni jambo la kutia moyo kidogo kuona kuwa uingizaji wa fedha za ruzuku kwa chuo hiki umefikia asilimia 58 ya makadirio hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014. Hata hivyo, fedha za kazi za maendeleo zimekuwa bado ni kitendawili kwani chuo hiki hadi kufikia mwezi huo wa Mei, 2014, kilikuwa kimeingiziwa Tsh millioni 10 tu kati ya Tsh milloni 90, ambazo ni sawa na asilimia 11 tu ya makadirio.

Mhe. Spika, pamoja na hali hiyo, Kamati inaisisitiza Wizara pamoja na Uongozi wa Chuo kuendelea na jitihada mbali mbali za kukiimarisha chuo hicho pekee cha serikali ikiwa ni pamoja na kutafuta wataalamu mbali mbali wakiwemo wa maabara ya mifugo na wale wa teknolojia ya habari na mawasiliano, ili Chuo hicho kiweze kukua zaidi kitaaluma. Aidha, Kamati inathamini sana mipango mizuri iliyowekwa na chuo kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015, ukiwemo ule wakuendeleza kazi ya ujenzi wa Dakhalia moja la ghorofa 4 yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 wa kike kwa wakati mmoja. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuongeza jitihada zitakazokifanya Chuo cha Kilimo Kizimbani kuwa na ulinzi wa uhakika wa masaa 24 kama vilivyo vyuo vyengine, ili kukiepusha chuo hicho na hatari ya matukio ya wizi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaombewa idhini ya matumizi ya Shilngi Ishirini na Tatu Billioni, Mia Tatu Sitini na Tisa Miliioni na Elfu Mbili (Tsh 23,369,002,000), kati ya hizo Shillingi Billioni Kumi na Tatu, Mia Saba Hamsini na Nane Millioni (Tsh 13,758,000,000) ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs Billioni Tisa, Mia Sita Kumi na Moja Millioni na Elfu Mbili (9,611,002,000), kwa ajili ya kazi za maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeyakubali mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na inawaomba Wajumbe wako waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Mchangiaji wa kwanza naona amedharurika, lakini anayefuata ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadae Mhe. Ali Salum Haji, afuatie Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nianze kuchangia kwenye ukurasa wa 50, ambapo Mhe. Waziri, ametuomba hapa tumuidhinishie shilingi bilioni 23,369,000,000/= kwa ajili ya kufanya maendeleo pamoja na mishahara.

Mhe. Spika, naamini kuwa fedha hizi ndio malengo ya wizara nzima ya kutaka kuendesha shughuli zake za kazi, lakini ninamasikitiko makubwa sana na mara hii bajeti yetu kubwa bilioni 700 na kidogo na tumeambiwa uchumi wetu umekua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa mimi huwa ninapata mashaka sana na kila hivi sasa nikiangalia kitabu jinsi malengo yao wizara ilivyojipangia ni kwamba tunadanganyana tu, kwa sababu fedha zenyewe tulizoambiwa zimekua ni shilingi bilioni 700 na wakati wizara hii inataka bilioni 23 utakuta na wizara nyengine, hali kadhalika tunakwenda kwenye mabilioni tu. Matokeo yake haikidhi haja na wala hawapati ile *percentage* ambayo waliyokusudia kwenye malengo yao.

Mhe. Spika, kwa kweli hatutendi haki kwa mujibu wa utaratibu na hatuzungumzi vizuri kwa wananchi wetu suala la kuwaambia ukweli, kwa sababu hatimaye tunakuwa tunawakaba mawaziri pamoja na watendaji wao na hata

ukiangalia bajeti ya nyuma pia kwa wizara hii haikufikia malengo kutokana na hali halisi ilivyo. Kutokana na hali hiyo, ndio maana utakuta kitabu chao hichi wameonesha jinsi gani wanavyokabiliwa na changamoto katika wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, kuna changamoto kubwa ambayo inayoathiri ufanisi katika utekelezaji wa kazi za wizara na upatikanaji mdogo wa fedha zinazotengwa katika bajeti kutoingiziwa fedha hizo. Hili ni sikitiko moja kubwa sana, kwa sababu hawawezi kulipa fedha za wakulima, kwani wao wenyewe wizara hawapewi fedha taslimu kwa mujibu wa utaratibu, kwa mfano jimboni kwangu wanadai fedha za mbegu ambazo waliwauzia, lakini nilitaka niwe mkali sana na kumbe ningewaonea bure, kwa sababu nilitaka nizuie fungu hapa, najiuliza nikizuia fungu, itakuwa nimembinya sana Mhe. Waziri, kwani yeye mwenyewe anadai fedha kama hizi aingiziwe.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, ingawa hayupo, lakini nataka niseme kwamba ninaisubiri Wizara ya Fedha, kwa sababu hivi sasa nimesomeshwa sana na jinsi gani nitakavyoichambua bajeti yao na jinsi gani itakavyoonesha dhahiri kuwa wanawadhulumu hizi wizara zilizopeleka malengo yao na hili ni moja. Kwa kweli wananchi wanapiga kelele kwa kutokujua, lakini sasa wapige kelele kuelekeza fedha ambapo ni Wizara ya Fedha, kwa sababu hizi wizara nyengine zinapewa fedha tu, kama ingekuwa zile fedha wanaingiziwa kwa mujibu utaratibu, mimi ningewakamata, kwani lengo lipo na linatakiwa kufanywa na hawakuweza kulifanya.

Mhe. Spika, niwaombe sana wananchi wangu kwamba wastahamili na wizara haina tatizo, kwa sababu Katibu hana sehemu ya kuzipata na hata afanye vipi, isipokuwa tutamsema asubuhi na jioni pamoja na Mhe. Waziri wake, lakini fedha hizi hawazipati. Vile vile, wanajitahidi kufanya kazi na wala tusifikiri kwamba wamelala usingizi kama vile wanakwenda na kurudi Wizara ya Fedha, watu wazima wanahangaika kwa ajili ya kudai haki yao, ambayo imepitishwa na Baraza hili tukufu. Kitu kinachonisikitisha kuwa hili Baraza tunakaa hapa na tunakula jasho au fedha za wananchi wetu kwa kuwapitishia mawaziri na tunaambiwa kwamba fedha zipo na tunatangaziwa kwenye bajeti kuwa fedha mara hii imepanda au uchumi umekua, umekua vipi? *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasikitika sana, kwa sababu hawa wanayo malengo mazuri sana ya kumuondoa mtu kwenye umasikini na kumpeleka kwenye utajiri katika masuala ya ukulima, kwa mfano kwenye ukurasa wa 6, wametuonesha mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na wameshatuwekea vizuri, lakini hakuna kitu. Kwa hivyo, hali hii haiendi kwani malengo yao bure yamo ndani ya *briefcase* tu, kwa sababu wanaendesha nini? Wanaweza kusema tunaleta matrekta 10, sio kweli hawana uwezo huo, lakini kusema binadamu hatoacha, kwa sababu ndio haki yao, si wanaambiwa maana ya kukaa bajeti, ikifika kipindi wanaambiwa leteni makisio yenu. Kwa kweli, masikini wa Mwenyezi Mungu wanakaa na wataalamu wao usiku na mchana kwa ajili ya kukaa na kutunga bajeti hizi na hatiyame imekuwa bure.

Mhe. Spika, tutafute sheria na naomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kwamba tuwatafute watalaamu na sasa tuunde sheria ambayo itawalinda mawaziri katika utendaji wao wa wizara. Naomba sana na mara nyengine nitaleta sheria, kwa sababu itakuwa huu ni mchezo wa foliti, yaani tunawachezesha foliti tu hawa mawaziri na tukiwa na sheria ya kuwa Wizara ya Fedha imeshindwa kuwalipa asilimia ile inabidi iwajibike itabidi iwe hivyo.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, nina wasiwasi sana na Mhe. Waziri wa Fedha, labda hawa wataalamu wake wanakuwa wanamdanganya kwa sababu *figures* hizi haziwi sawa na ninakataa, haiwezekani kuwa leo anakubalika Mhe. Waziri, katika kupanga bajeti na inapitishwa mpaka kwenye Kamati na watu wa fedha wanakuwemo kwenye Kamati kwamba hii safi. Kwa maana hiyo, iletwe na sisi hapa tunaomba idhini na sisi tunakubali kwa kupiga kura kusema tumeipitisha na leo wanashindwa kupewa fedha zile, kwa nini mumewakubalia mwanzo, ingekuwa mwanzo munawakatalia nafikiri isingefika leo Waheshimiwa Wawakilishi wetu hapa wakawa wakali sana kama vile Mhe. Saleh Nassor Juma na wala haiwezekani kukaa hapa na kupiga kelele tu, lakini anapiga kelele kutokana na hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba sana kwamba sheria hiyo tuitafute na tuweze kuletewa, ili tuweze kuwanusuru Waheshimiwa Mawaziri wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo au ni muokozi. Kwa kweli nafikiri kama tungejipanga vizuri sana katika kilimo, watu wote tungekuwa wanene na wala tusingekuwa wembamba na wembamba ni shida tu, kwa sababu mtu anafika mpaka jioni au usiku chakula cha mchana hajakijua.

Mhe. Spika, kilimo ni jambo kubwa sana katika nchi, lakini mpaka leo nikiuliza na wala sioni isipokuwa naona kiza kitupu, wananchi wanajitahidi kulima, lakini hawafikii malengo ya kilimo kwa sababu hawana zana zile zinazotakiwa au zinazoendesha kama wenzetu katika nchi nyengine, kwa mfano tunao wataalamu ambao wamesomeshwa kwa fedha nyingi sana na wanajitahidi wanakwenda *field* wanafika kwa wananchi kwa ajili ya kuonesha jinsi gani kilimo cha kisasa, lakini inakuwa ni bure, kwani huyo mtaalamu, pengine sijui hata hivyo vyombo vya usafiri vya kuweza kumfikisha shamba, sijui kama anacho. Tulikuwa tukitegemea *FAO* hivi sasa wameshaondoka, *UNDP* na wengine na hii ni hatari tegemezi, kwa sababu tukiwa tegemezi kila siku ni hatari kubwa sana.

Mhe. Spika, nafikiri serikali haijakaa na kuwaza neno "tegemezi" kuwa kila siku tunategemea tu kwa mjomba, iko siku tutateleza vibaya sana.Mimi naomba sana tuwe makini sana watendaji wetu hawa wanajitahidi katika kuendesha shughuli ambazo adhimu.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 32, nimeona jitihada za misitu, sasa hivi misitu inakatwa sana, lakini niwapongeze sana watu wa misitu wanajitahidi kutuletea majiko ya kila aina ya kusevu ili msitu usikatwe, tumeanzia gesi, tunakuja sasa hivi nimeona majiko yanatumia makaa matatu tu, basi yanapika vyungu vya sufuria ya pishi nne na wali ukawiva na kila kitu, niwapongeze sana hii yote inakuja katika kampeni ya kuwa msitu usikatwe hapo, niwape tano wamefanya vizuri sana na wamelifikiria zuri, lakini isitoshe badala ya kukata mzigo mzima wa kuni, jiko jengine linatumia kuni tatu na vile vile, kuanzia pishi tano mpaka pishi sita linaivisha, tizama teknolojia wenzetu walivyokuwa wanajitahidi, kwa kuwa serikali haina uwezo, wanatafuta mbinu wao wenyewe, Mwenyezi Mungu kawajaalia akili na *Ishaallah* waendelee na akili zao wanabuni wenyewe ili mbinu zile za kumtafutia huyu masikini aweze kuishi katika ile nchi yake.

Mhe. Spika, mimi ningeomba hapa unitafutie sheria, watu sasa hivi wanachimba mchanga, lakini wanapokwisha kuchimba mchanga, wanakuwa wanawacha wazi hampandwi miti, hapa naomba kidogo tuletewe sheria itakayomlazimisha yule mtu ambaye ni lazima asipopanda sheria, itamkamata moja, mbili, tatu, hilo naomba sana kwa mawazo yangu, naomba hiyo sheria ije haraka sana, si hivyo, pengine hiyo nchi itamalizika, toboa toboa.

Mhe. Spika, sasa ikiletwa sheria hiyo, kwa sababu mti ukiupanda unaleta rutubisha tena, kwa sababu ni sawa sawa na kuwa umechukua hamira umetia kwenye unga na ukavuvumka, sasa na mti utakaoupanda kwenye ile ardhi ambayo imechimbwa ya *second world* mle chini, kwa sababu ile ni ardhi ya mwisho, huwezi ukaendelea tana ukachimba kutokana na hali iliyopo, sasa unapoileta sheria akipanda yule mtu mti, basi rutuba ile itakuja tena juu na itapanda tena, itakuja katika uwasilia wa ile ardhi yenyewe, naomba sana na hapa kutokana na hali halisi.

Mhe. Spika, lakini niwasifu tena kutokana na kukusanya *community* na hivi karibuni *community* inakwenda nje hapa ni wapongeze sana na hivi ndiyo tunavyotaka, kwa sababu *community* ukionyesha nje dunia ya sasa, kwa kweli lile jambo linatia faraja kubwa sana, wenzetu nchi za nje, sasa hivi wanasheria kali, mti mmoja ukikatwa, unatakiwa miti kumi uoteshe na unasimamiwa kwa mujibu wa sheria, jinsi gani vile unavyoweza kuwezesha kuleta miti mingine, sasa hiyo ningeomba na wao wanajitahidi kusema ukweli, maana yake wanajitahidi, kwa sababu misumeno ukifanya mchezo wanaikamata na wanaichoma moto, kwa kweli na wao wanastahili sifa, maafisa wao ni walinzi wazuri wanaendelea katika utekelezaji wao mzuri, mimi nawasifu sana kwa hilo na ndio maana mpaka sasa hivi msitu ule wa Kiwengwa bado upo unaendelea na haiba yake, kwa sababu ya ulinzi wao mkali pamoja na *Community* inavyoendelea vizuri katika utendaji wake.

Mhe. Spika, kwa kuendelea, nakwenda ukurasa wa 40, Idara ya Umwagiliaji Maji hapa na laiti hii ningesema kuwa serikali ingeanza harambee ya kutafuta *Fund* kama tulivyofanya masuala ya meli na mambo ya maji, basi na mimi naiomba sana serikali basi na hapa ingefanya harambee, kwa sababu hapa sasa ndio tunatafuta uondowaji umasikini kwa kupitia ulimaji huo kwa kutumia maji.
Mhe. Spika, tungeweza wananchi wetu wakapata asilimia 99, wakawa katika ulimaji wa aina, ningeomba sana sasa hivi ingekuwa *Alhamdulliahi* Mwenyezi Mungu katujaali, sasa hivi wamo katika ramani ya ujenzi wa sehemu ya Kilombero na Pangeni, ningemuomba Mhe. Waziri, hebu njoo uniambie umefikia wapi kwa sababu kama utawezesha kule Kilombero na Pangeni mimi nadhani watakuwa na lishe nzuri, naamini watakuwa wanaendelea vizuri bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, naomba sana hapa patiwe nguvu sana, tena tusimamie kwa nguvu zetu zote, kwa sababu sasa hivi mvua zenyewe zinapita rasha rasha, kwa sababu tunakata miti, mazingira hatutumii na hatuyahifadhi vizuri. Katika vyanzo vya maji tunakwenda kujenga majumba, tunaacha asilimia. Sasa hii neema ya Mwenyezi Mungu kuleta mvua watu tunaikataa kwa hali ya nguvu sana.

Mhe. Spika, sasa mimi ningeomba kuwa sehemu hii, tungeomba sana, kuwa itiliwe nguvu ili wananchi sasa walime mpunga wa kumwagilia maji, tena wa kisasa ili tuone wenzetu, ndio maana wanainuka China, Thailand na sehemu nyengine na sisi uwezo huo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, wenzetu kule weupe na sisi weusi, lakini akili na sisi tunazo, isipokuwa kinachotushinda ni kule kuwa na zana za kuweza kufanyia kazi, lakini hata hivyo, wao wetengenezaji na sisi wanunuzi, nengeiomba sana serikali.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana kama unavyoeleza na naiunga hii na mimi kama siku zote ninavyokwambia siungi mkono bure bure, naiunga kwa sababu zangu maalum, naiunga kwa sababu ni masikini Wizara hii, niseme ukweli ulivyo, sijui yale Matrekta ya SUMA JK kama mshalipa na kama mmelipa nikupeni pongezi kubwa sana, kwa sababu mmejitahidi kutafuta fedha za kuweza kulipa matrekta. Kwa hayo, machache mimi naiunga mkono asilimia mia kwa mia na nyongeza zaidi kama zikiwepo *Ishaallah* nitakuongezeni mia moja na hamsini. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, kabla sijachangia lolote zaidi katika kitabu, nilikuwa nataka niende katika kitabu cha Makadirio na Mapato nataka twende katika ukurasa wa 59, kifungu 220500, Vifaa vya kuandikia, naona fungu limepanda marudugu, sababu za msingi za kuweza kupanda kiasi hiki zaidi ya mara tano, kutoka milioni tano, laki tano, tokea mwaka jana hadi miliono ishirini na nne laki mbili na sabini na nane mwaka huu.

Mhe. Spika, nikitoka fungu hilo, nataka niende katika ukurasa wa 63 huduma za kilimo fungu 221000, fungu dogo huduma za utunzaji wa misitu, mwaka jana iliomba 51,100,000/=, mwaka huu milioni 80,310,000/=. Nataka kujua tu kilichoengezeka na sababu za msingi za kuengeza karibuni milioni 80, nini kilichoongezeka kikasababisha fungu hili likazidi karibuni milioni 30 kutoka milioni 51 hadi milioni 80 katika huduma za utunzaji wa misitu? Mhe. Waziri, atakapokuja kilichoongezeka atanisaidia sana.

Mhe. Spika, fungu jengine ambalo nataka kulizungumzia ni gharama za vifaa vya huduma 220100 Mawasiliano. Pia, kifungu naona kimenona zaidi Mhe. Waziri, atakuja kunisaidia sababu za msingi za kuongezeka kila siku karibuni miaka mitatu nyuma, makisio yao yote kutoka 21112 milioni tatu, 1213 milioni tatu na elfu kumi, mwaka jana ilikuwa milioni tatu na laki sita, lakini mwaka huu milioni karibu 15,200,000/=, sababu za kuzidi kiasi hicho Mhe. Waziri, atakapokuja atanisaidia.

Mhe. Spika, fungu jengine nimeshituka na safari za nje na safari za ndani ukurasa wa 66, kifungu 220301 na 230302, karibuni miaka mitatu yote ya nyuma inazunguruka katika milioni 7, milioni 6, lakini mwaka huu kila fungu mwaka jana fungu la safari za ndani ilikuwa 7,480,000/=, mwaka huu 45 milioni na fungu la safari za nje mwaka jana ilikuwa milioni 7, mwaka huu milioni 42, ukiangalia fungu la jumla jumla kutoka milioni 14,480,000/= hadi milioni 87,240,000/=, karibuni zaidi ya milioni sitini na kitu zimeongezeka, fungu linatisha sana, Mhe. Waziri, atakapokuja atatueleza safari gani ambazo ameziandaa zaidi na kusababisha kutoka milioni 14 mpaka milioni 87.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 67, gharama za mafuta na vilainisho, fungu 220400, fungu dogo 220401, Gharama za *Petrol* kutoka milioni 5,772,000/=, mwaka jana mpaka milioni 22, mwaka huu na fungu 220402, Gharama za *Diesel* kutoka milioni 4,770,000/= hadi milioni 21,600,000/=, nielezwe kilichoengezeka kitu gani mmeengeza magari au kitu gani?

Mhe. Spika, lakini katika masuala ya mafungu, nataka nimalizie kwenye ukurasa wa 68, gharama za mafunzo sikatai tunahitaji kuwajenga uwezo vijana wetu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kwa ubora na hali halisi ambayo tunavyohitajia, huu ni wakati wa wasomi, lakini hapa atakapokuja Mhe. Waziri, anisaidie tu fungu hili kiujumla, mwaka jana walitengewa milioni 244,500,000/=, hapa mimi sitaki zaidi, kwa sababu pamoja na kwamba imezidi karibuni milioni 11 zimeongezeka. Hapa mimi nataka Mhe. Waziri, atakapokuja aje anitajiye hawa waliokwenda kupewa mafunzo mwaka jana ambapo wamegharimu kutumia karibuni milioni 244,500,000/= na wale ambao tunatarajia kupeleka mwaka huu mpaka tukafika pahala tukawatengeya milioni 335,450,000/=, wakati wa kuja kufanya majumuisho, namuomba kwa heshima kubwa Mhe. Waziri, aje aniletee hizo orodha za wanafunzi wa mwaka jana na wafanyakazi wa mwaka huu ambao wanataka kwenda kupata mafunzo.

Mhe. Spika, nataka niende katika kitabu chako cha Mhe. Waziri, mimi nataka nizungumzie katika masuala mazima ya kilimo, kwa masikitiko sana sana, suala hili mwaka jana nililizungumzia mwaka huu nimelizungumzia, lakini imekuwa ni wapiga kelele tu za kwenye debe tu, sijui sababu gani kwa sababu labda kichwa chenyewe kimekuwa hakiko makini, kwa sababu tunajua Mhe. Waziri, hayupo kunakuwa kuna kaimu muda mrefu na kaimu mwenyewe kila mtu ana majukumu yake, unajua ukaimu wakati mwengine una matatizo, huwezi kukamata watu wawili kwa wakati mmoja, jirani na wako huwezi kufanya hizo kazi.

Mhe. Spika, mwaka jana nilizungumzia namna ya mabonde ya mpunga yanavyovamiwa katika Wilaya ya Magharibi, kelele zile zimekuwa kimya, hatuoni jitihada za Wizara, hatuoni jitihada za serikali, mabonde yanamalizika, niambiwa mwaka jana nilizungumzia hatua gani ambazo zimechukuliwa katika bonde la Meli Nne Mashine ya Maji na bonde la Meli Nane Chuwini, Mabonde haya karibuni yatamalizika kabisa labda Mhe. Waziri, atwambie kama wameamua hawalimi, basi watwambie lini mabonde yale watakata viwanja kwa kuyamaliza kabisa na kujenga nyumba zao. Hapa mimi kidogo nitakuwa mgumu katika suala zima, kwa sababu hatuoni juhudi za Wizara katika kusimamia mali zao, haya mabonde yatakuwa na mabwana shamba, watu wanalipa kutakuwa na fanyakazi, lakini tunatoa gharama kubwa kupeleka kwa watu, lakini mabonde baada ya watu kuyaendeleza mabonde yanatumiwa katika shughuli za majenzi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumziye, ni suala zima la ndugu zetu wakulima ambao wamelima mbegu zile, mbegu zipo nyumbani, mbegu zinaoza, Wizara haioneshi jitihada zozote za kuweza kuwasaidia, sasa watu wanalia njaa imekuwa watu wanakula mbegu zao wenyewe. Kwa sababu kilio hichi mara nyingi unakuwa unakisia maredioni na katika *TV*. zetu, watu wanasikitika wanalima mbegu, lakini huoni jitihada za Wizara, ingawa tuliambiwa tu kwamba lile tatizo labda ni Wizara ya Fedha kuingiza fedha, lakini mimi nahisi kama sio Wizara ya Fedha kuingiza fedha, basi tungeandaa utaratibu utakaokuwa mzuri, kwa sababu mtu anapofanya kitu akategemea kitu, inakuwa ni tatizo, anakaa na mzigo ndani, lakini hali halisi hailipi, mwisho itabidi wakulima waanze kula mbegu zao wenyewe, baada ya kutegemea pesa kutoka Serikalini kuja kununua hizo begu.

Mhe. Spika, nimeona hapo ukurasa wa 5, umezungumzia suala la kilimo cha mboga mboga, wameeleza kina umuhimu mkubwa na wana mashirikiano na taasisi ya wazalishaji wa mazao ya mboga mboga. Mimi nataka kujua tu Mhe. Waziri, atakapokuja anisaidie haya mashirikiano ambayo mmeyafanya na huo utafiti baada ya kuona kilimo cha mboga mboga, sasa hivi kimekuwa kina tija, labda Wizara imetoa motisha gani, kwa wakulima wa mboga mboga na katika maeneo gani na wakulima gani ambao wamefaidika katika hili suala zima la ulimaji wa mboga mboga, kutokana na haya mashirikiano ya hivi taasisi mbili ambazo wamezitaja wao wenyewe *TAHA* na *ZAIMU*?

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 6, kitabu chake Mhe. Waziri, ukurasa wa sita ameelezea muelekeo wa bajeti ya Wizara ya Kilimoa na Maliasili mwaka 2014/2015, chini wakajinasibu kwa madaha sana kwamba mwelekeo wao ni kutekeleza dira ya 2020 Ilani ya uchaguzi, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Mimi nasema maneno mazuri, lakini sijui kama yatakuwa na ukweli ndani yake kama kweli tuna lengo la kupunguza umasikini na kama kweli tuna lengo la kutelekeza Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, sababu gani ya kusema hivyo, nimekuja na *document*, nikimaliza kuzungumza hapa, nitamkabidhi Mhe. Waziri, aziangalie kwa kina kabisa.

Mhe. Spika, kuna wananchi wetu ambao wanalima mpunga katika shamba la Kibongemzungu na katika orodha yao hii waliyonikabidhi wananchi 189, wananchi hawa waliletewa barua kutoka kwa Mkuu wa Wilaya tarehe 16/1/2014, barua inazungumzia kuhusu wito muhimu na imesainiwa na Ofisa haikusainiwa na Mkuu wa Wilaya Ofisa anayeitwa Zahara Aboud Mzee. Baada ya wito huu, wananchi hawa baada ya kwenda katika taasisi husika ya Mkuu wa Wilaya, maelezo awaliyoyapata ni kutafuta namna ya kuweza kurudisha yale maeneo ili yarudi kwenye serikali, walisikitika wananchi hao, kwamba mashamba haya wamekabidhiwa kwa muda mrefu, sio chini ya miaka 17 au 16, wengine tokea Wazee wao mpaka hii leo, sasa katika maelezo waliyoyapata kwamba tunataka kulifanyia maboresho lile shamba la Kibondemzungu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kutokana na maboresho yanayotakiwa kufanywa, kuna haja ya kupata yale mashamba wayarejeshe Wizarani ili yaweze kufanyiwa hiyo huduma na hata katika barua yao Mhe. Waziri, atakuja kuiona nitakavyompelekea, inaelezea kwamba naomba ninukuu kidogo tu inasema; "Majina ya wakulima wa Kibondemzungu Shehiya ya Fuoni Kibondeni, Wilaya ya Magharibi Unguja kwa heshima naomba uhusike na mada ya barua, hii kama inavyosomeka pamoja na barua hii, naambatanisha na majina ya wakulima wa bonde la Kibondemzungu ambao walioazimwa na kutakiwa wayarejeshe mashamba hayo".

Mhe. Spika, wakulima wale wameanza kuwa na wasi wasi mkubwa na wameanza kupata mashaka juu ya hali halisi ya shamba lile, sasa Mhe. Waziri, atakapokuja anisaidie kama hili lina ukweli ndani yake au kama wananchi wale hawajaelewa, lakini kama kuna dhamira au kuna wajanja ambao wanataka kulichukua shamba lile kwa njia nyengine, kwa sababu mimi naimani kwamba hata kama kutakuwa kunahitaji maboresho ya aina gani, kama kuna watu ambao wamekaa pale kwa muda mrefu wanalima, basi maboresho watakayofanya wafanyiwe wale ambao wanalima katika bonde eneo lile na si vyenginevyo, kuwatafuta wengine kuja kuwapa lile shamba, vyenginevyo kama kutakuwa kuna uweki huo, basi nasema ndio pale, yaani muelekeo wa dira na ule muelekeo wa kutekeleza Ilani, sitegemei kama utakuwa unatekelezeka ipasavyo Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa heshima kubwa, mimi sitounga mkono hotuba hii mpaka nitakapopata maelezo ya kina kutoka kwa Mhe. Waziri, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, ambayo imewasilishwa hapa na Mhe. Kaimu Waziri.

Mhe. Spika, nianze vile vile, kwa kumshukuru Kaimu Waziri katika Wizara hii, pamoja na watendaji wote ndani ya Wizara kwa kazi kubwa na nzito ambayo inaendelea, japokuwa kuna baadhi ya maeneo bado yanaendelea kutokutufurahisha. Mimi nianze na buku hili kubwa katika maeneo ya vifungu katika ukurasa wa 66, ambapo katika kasma namba 220300 katika huduma za safari, kama ambavyo wenzangu waliokuwa wametangulia kuzungumza.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelekezo ya bajeti kuu ya Seriali tulikubaliana hapa kwamba safari za nje tuziondoshe kabisa au tuzipunguze sana. Lakini bado katika buku hili la maombi ya kasma ambazo zinatakiwa zikubalike, ili kupitisha bajeti hii kuna ongezeko hapa tukiangalia mwaka jana Wizara hii ilituomba tuidhinishe 14,480,000 na mwaka huu wao wameomba waidhinishiwe 87,240,000 tukiangalia na yale makubaliano yetu ya kupunguza safari hapa zimezidi zaidi.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, kwa hivyo atakapokuja Mhe. Waziri naomba atusaidie hapo ufafanuzi. Kama ni safari za kikazi ambazo muhimu sina matatizo nazo lakini kama ni safari tu za kwenda hizi itabidi Mhe. Waziri utusaidie kidogo.

Nikiondoka hapo ninakuja ukurasa wa 68 ambapo kuna fungu kasma ndogo 201400 ukurasa wa 68 eneo hili vile vile kuna tatizo hili la ukodishaji la ukodishaji wa ukumbi na eneo hili, pia tulizungumza kwamba nalo tulifanyie utaratibu, ili tuweze kutumia kumbi zetu za kawaida katika kufanya mikutano yetu ya ndani. Lakini kinajionesha hapa Mhe. Spika, mwaka jana Mhe. Waziri alituomba tumhalalishie shilingi 2,700,000 na mwaka huu anaomba tumhalalishie shilingi 3,600,000. Sasa hapa naona kwamba hatujenda sambasamba na yale matakwa ambayo ilikuwa tumekubaliana.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, sasa ninakuja katika ukurasa wa 73 unaozungumzia huduma za kilimo. Lakini wakati nataka kuzungumzia suala hili la huduma za kilimo kuna maeneo katika ukurasa wa 77 ambapo nimeangalia humu ndani katika hivi vifungu nimekuta fedha nyingi sana Mhe. Spika, zinakwenda katika huduma za mawasiliano, mambo ya simu pamoja na posta lakini na *telex* na mambo ya santuri yamo zaidi. Maeneo haya yamechukua fedha nyingi sana katika buku hili la kuomba kupitisha vifungu.

Katika buku letu hili hili kuna eneo katika ukurasa wa 73 ambapo kuna huduma za kilimo na hapa kulikuwa kuna ununuzi wa mbegu za utafiti, kuna ununuzi wa mbolea, ununuzi wa dawa za kulia wadudu, maeneo haya yote kuna 00 yaani hakuna fedha ambayo ilikuwa imehalalishwa kwa sababu ya kusaidia maeneo haya na hii ni Wizara ya Kilimo na masuala haya ndio yanayolengwa kuweza kufanya hii Wizara, ikasaidiana na zile juhudi za wananchi katika kuendeleza kilimo katika nchi yetu. Lakini maeneo haya ya dawa na kila kitu hatukuona kitu. Sasa sijui Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kwa vile mwaka jana walipatiwa milioni kumi nne walinunua wanazo nyingi, bado wanaendelea kuzitumia au waliona wao kwamba eneo hili halina kipaumbele ndio maana wakaacha na wakaelekea katika masuala ya santuri, *telex*, na mambo mengine mengine. Mhe. Waziri atakapokuja hapa nitaomba atusidie majibu vile vile.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kwa namna gani tumejipanga kutunza misitu yetu. Katika buku letu hili kubwa nikiangalia fedha ambayo ilikuwa imetengwa 73,000,000 kwa ajili ya kuendeleza

kutunza misitu ndani ya maeneo yetu Zanzibar naona ni fedha ndogo sana hususan ukitilia maanani kwamba msitu unaondoka kwa kasi kubwa. Sasa sijui katika kuendeleza misitu Mhe. Waziri wamejipangaje kuhakikisha kwamba misitu yetu ya Zanzibar tunaihifadhi na miti inaendelea kuwepo sio kukatwa katwa kila mara na baadae tunakabiliwa na jangwa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika eneo ambalo la kawaida ambapo kuna uhalalishaji wa chakula. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 58 wa kitabu chetu hiki ambacho Mhe. Waziri alikuja kukisoma tumeona hapa kwamba kuna programu ya miradi mbali mbali ambayo inataka kuendelezwa, lakini mojawapo ikiwa ni eneo la chakula na lishe. Lakini katika kitabu hiki kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Spika, na pamoja na ripoti iliyokuwa imesomwa hapa na Mhe. Viwe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, ilikuwa imeelezea jinsi serikali ambavyo ilishindwa kutusaidia kuwatilia pesa Wizara hii shilingi 160,000 milioni kwa ajili ya kuendeleza suala hili la akiba ya chakula, mradi wa uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Spika, ninamuomba atakapokuja hapa Mhe. Waziri atuhakikishie katika kipindi hiki cha fedha cha 2014/2015 fedha hizi zinaingizwa, ili utaratibu na ukamilishwaji kwa mwaka wa nne wa suala hili la uhakika wa chakula na lishe liweze kukamilishwa ili tuweze kupata kuona matokeo yake katika mwaka 2015/2016.

Nasema hili kwa sababu nimekuwa na kawaida ya kufuatilia sana katika mradi huu ili tuweze kwenda sambamba na yale matakwa na maoni ya Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuhakikisha kwamba akiba ya chakula inapatikana katika nchi yetu ya Zanzibar.

Najua ni *project* ambayo ni refu, mambo yake ni makubwa lakini na inapokuwa kwamba hawakuwezeshwa kuna mwaka ukawa umepita bila kusaidiwa fedha jambo hili litakuwa ni ndoto kuweza kutimia kwake. Kwa msingi huo basi ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa heshima na taadhima ahakikishe anatuelekeza, anatufahamisha na anatupa maelezo mazuri ya kuhakikisha kwamba fedha hii itakuwa imepatikanwa na tutahakikisha kwamba yale mambo ambayo yamebakia katika kukamilisha mradi huu yanakamilika na zoezi hili linaanza kutoa matunda yake ambayo yatakuwa ni endelevu katika kipindi cha mwaka 2015/2016.

Baada ya maelekezo hayo sasa Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima mimi naunga mkono bajeti ya Wizara kwa asilimia 95 na ninambakishia asilimia tano tu Mhe. Waziri ili atakapokuja hapa anitosheleze kwa yale ambayo nilikuwa naomba ufafanuzi wake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kwa kuniptia nafasi jioni hii ya kuweza kutoa mchango wangu. Lakini vile vile nachukua nafasi hii ya kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo waliyoifanya; maelezo mazuri, yako wazi na wamejieleza kwa ufasaha kabisa pamoja na matatizo yote waliyonayo.

Vile vile niseme tu kwa upande wa Wizara hii kwamba kiwango cha fedha ambacho walitiliwa katika Wizara hii ni kiwango kidogo sana. Wizara hii ni kubwa kwa sababu inakwenda bega kwa bega na wananchi Unguja na Pemba na ndio maana ukaona kwamba mambo mengi yamekwama. Pamoja na hayo hawajasita bado kuendelea kutoa ushauri na kufanya mambo ya kilimo yawe mazuri.

Mhe. Spika, mimi nataka nizungumzie mwanzo kwenye suala la shamba la uzalishaji wa mboga mboga na maua. Shamba hili kwa taarifa tulizonazo ni kwamba liko Tunguu hapa Unguja na kwa upande wa Pemba liko Mbuzini. Kwa kweli natoa pongezi kwa Wizara hii kwa kuwafanya vijana wetu wa Unguja na Pemba wakaingia katika suala la kilimo, kwa sababu vijana tokea hapo zamani mambo ya kilimo hawayapendi, wanapenda mambo ya kisasa. Lakini kwa ushujaa wao watu wa kilimo wamejaribu kuwaweka vijana mahala pamoja ili wajishughulishe na kazi.

Kwa hivyo mimi ninawapongeza kwa hilo, kwa mfano kama mwalimu yuko darasani anasomesha au mwalimu yuko darasani mwengine hasomeshi; mwalimu anayesomesha ni sawa sawa na mwalimu aliyekuwa hasomeshi darasani yatatokea baadhi ya mambo. Kwa sababu kama hukuwasomesha au hukuwapa kazi za kufanya wanafunzi wale wanaweza kujishughulisha katika mambo wanayoyataka wao. Ni sawa sawa na sisi watu wa Zanzibar, vijana wetu kama hatukuwapangia shughuli za kufanya basi watajishughulisha katika mambo ambayo yaliyokuwa si ya msingi na tunajua mambo ambayo wanajishughulisha ni haya ya kujiingiza madawa ya kulevya. haya ni mambo mabaya.

Kwa hivyo ninawapa pongezi watu wa kilimo kwa kuchukua jitihada hizi kuwaweka vijana pahala pamoja wakaweza kufungua mashamba yao na inaonesha kwa taarifa kwamba mashamba yapo mazuri, yanakwenda vizuri, uzalishaji mzuri, mavuno mazuri na kipato kwa vijana kinapatikana.

Kwa hivyo hiyo ndoto nzuri na tukasema kwa hali yoyote kwamba hii ni selfu *employment* yaani vijana wanajiajiri wenyewe. Kwa hivyo mashamba haya ni mashamba darasa kwa hivyo kama haya mashamba ni mashamba darasa kwa hivyo ni jambo zuri na mimi nataka niwaombe watu wa Wizara kwamba haya mashmaba mawili yasiwe hayo tu, lakini waendelee zaidi kuwaendeleza katika mashamba haya kila mahala, ili vijana wetu waweze kukaa mahala pamoja kwa faida yao wenyewe, wakapata pato lao na taifa likapata vile vile.

Ila tu nataka niwaombe vijana pamoja na kuwa Wizara imechukua jitihada ya kuwawekea haya mashamba, wayatunze mashamba yao. Kwa sababu ikiwa mashamba haya hawakuyatunza inawezekana hii kazi waliopewa kuifanya itakuwa haina maana yoyote.

Vile vile niseme tu kwamba nimuombe Mhe. Waziri kwamba hawa vijana ambao wana haya mashamba wasipuuzwe; wapelekewe wataalam mara kwa mara kwani yanaweza kuathirika kwa wadudu au kutaka ushauri. Kwa hivyo kwa kuwa mashamba yashakuwa tayari na wao wanafanya kazi lakini Wizara iwapitie mara kwa mara ili kutoa ushauri na kuwaelekeza na katika hifadhi ya wadudu ikiwa watatokezea. Mradi huu ni mzuri na mwaka huu una lengo la kuongeza maeneo zaidi, ninafikiri bila shaka itakuwa una malengo hayo. Kwa hivyo kama Wizara ina malengo ya kuongeza maeneo zaidi itakuwa ni suala zuri.

Mhe. Spika, baada ya hapo nataka nizungumzie juu ya sekta ya kilimo ambayo tunasema kwa ufupi kwamba kilimo ni tegemeo letu kubwa sana la kiuchumi kwa watu wa Zanzibar. Wananchi wanaweza kujikimu katika masuala yao ya kilimo kwa kupata chakula chao wenyewe, kwa kupata chakula chengine cha kuuza na kuweza kupata lishe bora na kuweza kuuza kwa ajili ya maslahi ya mahitaji mengine. Kwa sababu ukilima unapata wewe mwenyewe binafsi.

Kwa hivyo kwa kuwa suala la kilimo katika nchi yetu ni sawa sawa na suala la uvuvi. Kwa sababu kilimo na uvuvi inakwenda pamoja. Watu wetu wa nchi hii kazi hizi mbili ndio kazi zao kubwa. Kwa hivyo hapa mimi ninafikiria kama ilivyokuwa asilimia 80 ya watu wetu ni wavuvi na asilimia 80 vile vile watu wetu ni wakulima. Kwa hivyo watu wetu zaidi wanategemea suala la kilimo na haya Mhe. Spika, hii ni *traditional system*, yaani ni mambo ya asili kwa kila atakayezaliwa. Kama baba alikuwa mvuvi na *family* inaendelea kuwa ni wavuvi, wazee wakiwa ni wakulima na watoto wao wanakuwa ni wakulima.

Kwa hivyo watoto wanarithi kazi zile za baba zao na sio kazi mbaya. Kazi ya kuvua sio mbaya na kazi ya kulima sio mbaya kwa sababu zinaleta tija.

Hata hivyo mfumo bado ni wa kutumia nguvu zaidi, hapa tu ndio nataka niseme kwamba pamoja na kuwa vijana wetu na watu wetu, hasa wanawake ndio wao wanajishughulisha zaidi na mambo ya kilimo, lakini utakuta vile vile wanatumia nguvu zaidi kuliko kutumia mambo ya kisasa. Wanatumia majembe ya zamani ya mkono katika shughuli zao za kilimo. Sasa kama suala ni hilo sisi tunasema tubadilike kwa sababu ni wakati wa kubadilika, wakati wa kubadilika ni kuondoka katika yale matumizi ya zamani na tuingie katika matumizi ya sasa. Lakini ni vyema kwa Wizara isijikite kwa mahala maalum kwa sababu hii Unguja na Pemba ni kubwa na kilimo ni nchi nzima.

Sasa kwa hivyo ninafikiri Wizara hapa isijikite kwenye maeneo maalum tu lakini ijikite na katika maeneo mengine watu wadogo wadogo tunaweza tukawasaidia wakulima wetu, badili ya kufanya kazi za mikono kwa kutumia nguvu zao za mikono wakaweza kupewa mashine za mtu mmoja mmoja wakaweza kufanya kazi zao za kilimo. Nataka nimwambie Mhe. Waziri pamoja na kutumia matrekta ambayo yanafanya kazi kubwa kwa mashamba makubwa makubwa, kwa watu wengi lakini hata hivyo tusiwasahau wale ambao waliokuwa hawana uwezo wa kukodi trekta au kulitia trekta katika mashamba yao ya kilimo.

Hata hawa mmoja mmoja, tuone tunabadilika kutoka kazi za mikono na kupunguza kutumia nguvu kwa kutumia mashine za kisasa. Kwa hivyo ziko mashine za mtu mmoja mmoja, hivi ninafikiri Wizara ijikite katika masuala haya ijaribu kutafuta shughuli zake nje ya nchi ili kuharakisha kilimo.

Kwa sababu tunapoharakisha kilimo tunamsaidia mtu mmoja mmoja, watu wengi, mapato yanapatikana kwa mtu mmoja mmoja na watu wengi na taifa kwa ujumla. Kwa hivyo nimuulize tu Mhe. Waziri ni lini zana hizi za mtu

mmoja mmoja zinaweza kupatikana katika nchi yetu, ili watu wetu waweze kufaidika na mashine hizi kwa kazi za kilimo ambayo hii itapunguza masaa ya kufanya kazi.

Baad ya hapo Mhe. Spika, nataka nizungumzie habari ya hali ya hewa. Inapokuwa nzuri tunafaidika sote, na inapokuwa mbaya inakuwa nchi yetu inaingia katika ukame. Wakati wa hali ya hewa nzuri ndipo wakulima wanapokuwa wanaingia katika harakati za kusafisha mashamba yao ili kuliweka tayari kwa ajili ya kilimo. Lakini sasa hapa baada ya mashamba kutayarishwa na mbegu kuwekwa tayari kuna mahitaji ambayo yanahitajika katika kilimo. Tunahitaji tupate *product* ya kilimo iwe kubwa. Tutakapoisaidia ardhi bila shaka matunda yake yatakuwa mazuri, chakula kitakuwa kwa wingi.

Sasa mimi nina wasiwasi kwamba wakulima wetu wengi wanaacha kutumia mbolea kwa sababu ardhi saa nyengine zinahitaji kusaidiwa. Kama ardhi hazikusaidiwa katika kupanda mpunga wetu yaani chakula kitakachopatikana au mavuno yatakayopatikana yatakuwa kidogo.

Kwa hivyo niwaombe tu kwamba wakati wa matumizi ya ardhi yale mambo ambayo yanahitajika kwa mfano mbolea kwa kuisaidia ardhi iweze kupatikana kwa haraka. Hili ni suala lina matatizo kidogo kwa baadhi ya sehemu mbolea haifiki kwa wakati. Mbolea inakuja baada ya mtu keshapanda mpunga, mpunga ushakuwa mkubwa, haifai tena. Kwa sababu inatakiwa mbolea ile uitie kabla hujapanda kitu chochote, uivurugie pamoja ili ichanganyike na udongo wakati unapanda mpunga iwe inaota pamoja. Lakini ikija baada ya mpunga ushakuwa katika ardhi inakuwa mbolea ile haina haja tena.

Bada ya hayo nataka niseme tu Mhe. Spika, katika kupanda mpunga baada ya kuisaidia ardhi tunataka na mpunge usiwe *stunted* ukawa mfupi, haukukua. Tunataka mpunga uweze kukua na uweze kutoa mashuke makubwa. Sasa hapa tunasema vile vile nimuombe Mhe. Waziri mbolea katika ardhi na dawa za kuulia magugu zipatikane mapema, kwa sababu mpunga unapokuwa mkubwa unataka kutiwa dawa uwe safi kabisa. Dawa itiwe na mpunga uje juu na mashuke yawe makubwa.

Sasa mbolea na dawa za kuua magugu zinachelewa kufika kwa wakati. Kwa hivyo, pale tunapokuwa tunategemea mavuno yawe mazuri, mavuno hapo hayawezi kuwa mazuri kwa sababu kuna baadhi ya sehemu hasa hizi ambazo zinanyeshewa na mvua kubwa zinakuwa ni ardhi ambayo zinaota magugu kwa haraka, hivyo zinamsumbua mkulima kuweza kutoa majani yale na akipata dawa haraka majani yanaweza kupungua akatia dawa za kukuza mmea na matunda yakawa mazuri.

Mhe. Spika, kwa kuwa ardhi zetu zinaota magugu kwa haraka naomba dawa zifike kwa haraka na mbolea zifike kwa haraka.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie juu ya mabwanashamba; mabwana shamba ni watu muhimu sana. Unajua watu wetu wanalima si kwa sababu kwa kuwa wao wamesoma sana, ni kwa sababu ya mazoea tu baba ana mtoto anaona kila siku kwa hiyo na yeye anakuwa mkulima. Lakini kuna mambo mengi anayakosa mkulima kwa sababu hana uwelewa wa kutosha pengine hawezi kujua wakati ambao sasa ni wakati wa kulima, wakati wa kupanda mpunga ni wakati gani, hivyo wanakuwa hawaelewi.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri hao mabwanashamba wajitahidi kama wapo kidogo waongezwe kwani maeneo ya kilimo ni mengi sana, kwa hiyo kila wakipatikana hao watu kwa wingi ni bora zaidi.

Mhe. Spika, wangepatikana watu kama hawa wakatoa elimu wao kwa wakulima, wakafanya majaribio kwa wakulima namna ya kuwaelekeza nafikiri suala hili litakuwa zuri zaidi. Kwa hivyo, wasiwe mabwanashamba wakuzunguka tu lakini watoe taaluma kwa wakulima wetu, ili wakulima waweze kufaidika na kilimo chao.

Mhe. Spika, zaidi nataka nijikite katika hiki kilimo cha maweni. Mhe. Spika, kwa mujibu wa nchi yetu imegawika katika sehemu mbili; kuna sehemu ya Mashariki na kuna sehemu ya Magharibi. Sehemu ya Mashariki ya Kisiwa chetu cha Pemba na sehemu ya Kisiwa chetu cha Unguja zinalingana kwa sababu Mashariki ya Pemba kuanzia Micheweni mpaka Kengeja yote ni ardhi ya mawe, kwa hiyo kuna kilimo chake maalum. Kwa Unguja vile vile kuna Mashariki na Magharibi sehemu zote za Magharibi zinapata mvua nyingi sana, na sehemu zote za Mashariki zenye mawe mawe zinapata mvua kidogo kidogo. Mwenyezi Mungu vile vile kawawekea kwamba na wao wanaweza

wakalima wakapata mavuno mazuri na wakafaidika vizuri. Lakini sasa mbona naona hakuna kutiliwa mkazo mkubwa katika suala la kilimo cha maweni, huku hakuna watu? Huku kuna watu wa aina mbili;

Watu wa aina ya kwanza wavuvi na aina ya pili ya watu ni wakulima; wote hao wanaishi mahala pamoja na zote hizi ni shughuli zao. Shughuli ya kuvua na shughuli ya kulima inakwenda siku moja au wakati baada ya wakati, asubuhi anakwenda shamba, baadae anakwenda kuvua. Kwa hivyo, lakini humu katika ardhi hizi za mawe bado mambo yanakuwa ni mazito na magumu kwa ukanda huu, kwa nini katika maeneo kuanzia Micheweni utaona hawa wana kipando maalum ambao Mhe. Waziri hili unalielewa. Ni watu ambao wanataka kujishughulisha kwa kilimo cha mtama, kilimo cha mahindi, viazi vikuu, mbaazi, kunde, uwele, pilipili hoho, maboga, vitango pepeta pamoja na midimu.

Sasa hili suala mbona silielewi au hatuna watu wa kutosha, kama hatuna watu wa kutosha basi tutafute waajiri wa watu wetu wa kilimo tuwapeleke kule katika sehemu za maweni ili wawahamasishe wananchi, wawapatie mbegu kama hawana ili kilimo kiendelee. Hivyo sisi tunataka tununue kila siku kutoka nje, na sisi hatutaki kununua mbaazi ambazo zinalimwa hapa, hatutaki kununua viazi vikuu *alhamdulilah* tunanunua vinakuja marikiti hapa, ndimu zinakuja lakini mtama tunanunua kutoka nje, na mtama katika maeneo yetu ya maweni kote kunaota mtama vizuri. Mahindi yanaota kwa wingi. Kwa nini hapa *emphasis* imekuwa ndogo, kuna tatizo gani, kuna kitu gani hapa hatukuelezwa hasa nini sababu, inaonesha kwamba kilimo cha maweni kinavia kuliko kilimo hiki cha mvua kwa sababu huku mvua ziko kila wakati.

Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri atoe kipaumbele kwa kilimo cha upande huu, kilimo hiki ni muhimu sana kwa hiyo wakulima wanahitaji kusaidiwa pamoja na wavuvi walioko sehemu ile wote ni wakulima hao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba utakapomaliza shughuli zako unambie hasa sababu gani ambazo zinafanya ukanda huu umepuuzwa kiasi ambacho watu hawa wameshinda kujiendeleza na kuweza kuzalisha mazao kwa wingi.

Mhe. Spika, mimi nataka kusema kwamba kama nchi hii itasimama vizuri na vijana wakawawezeshwa hawa vijana wetu wakaweza kujishughulisha kwa kazi kama hizi za miradi mingi kabisa basi tutaondosha matatizo ambayo vijana wetu wanayafanya. Mhe. Spika, wapelekwe katika maeneo haya wakajishughulishe, watakapohisi kwamba wanapata kipato basi vijana wetu wengi watajishughulisha na mambo ya kilimo. Sasa hivi asilimia kubwa ya kilimo inafanywa na watu wazima wakati vijana wako wamepumzika hawataki, kazi yao ni mazungumzo, michongo na mambo ya kipumbavu pumbavu.

Kwa hivyo, mimi nafikiri kama Wizara hii ya Kilimo kama ilivyofanya kwenye mashamba mawili ya mfano waendelee kutanua mambo haya nakuweza kuwashughulisha vijana katika kazi za kilimo.

Mhe. Spika, tukifanya hivi nafikiri matatizo mengi yatapungua ambayo yale tunayajua sisi sote kwamba vijana wetu wengi wameingia katika madawa ya kulevya. Hii ni kwa sababu serikali bado haijawa makini kwa vijana wetu, iwachukue vijana iwapeleke katika maeneo hayo, nafikiri hilo litaweza kusaidia.

Mhe. Spika, jengine upandaji wa miti ya misitu, hili ni suala zuri sana na mimi niwapongeze wizara hii kwa jitihada zao kubwa za kuweza kupanda miche ya misitu kwa wingi, na hili ni jambo la msingi. Hii wizara ina kazi kubwa sana ndio tukasema bajeti yake hii wizara lazima iwe kubwa sana. Kwa sababu wizara hii imetawanyika kila pahala visiwa vyote hivi, kila pahala inahitajika. Kwa hivyo, jitihada wanayo kubwa yakuhakikisha maeneo yaliyokuwa wazi yapandwe miti kwa wingi. Misitu hii ina faida kubwa sana. Misitu hii inatusaidia kwa hali ya kuweka hali ya hewa nzuri, tunapata kivuli tukipanda miti mingi, wanyama wetu wanapata kupumzika kwenye vivuli, na sisi wenyewe tunapata *fresh air*, tunapata *pure oxygen* tukiwa na miti mingi. Pia miti ni dawa ya binadamu, binadamu na miti wanakwenda sambamba na sisi tupande miti kwenye majumba yetu kwa sababu tunapata *pure oxygen*, sisi tunatoa *carbondioxide*, tunapata *oxygen* kutoka katika miti.

Miti ikiwepo katika miji kuna ubaya gani? Inatusaidia kwa kivuli na inatusaidia kwa kupata *pure oxygen* ambayo inakuwa *purified* katika miti. Kwa hivyo, hili ni suala na mimi nawapongeza sana watu wa kilimo, waweke na katika mji wetu usiwe una joto na jua kali sana, tupande miti ili watu waweze kupumzika wanapokwenda katika safari zao. Miti inasaidia kuondosha mambo mengi ya ukame pakiwa hapana miti ukame unaingia, pakiwa na miti ukame hauwezi kuingia.

Mvua pia inasababishwa na miti, miti ikiwepo mingi mvua inanyesha kubwa na ndio maana tukasema tuwe na misitu, na misitu tunayo, misitu hatuikati bado tunaiboresha misitu iwe mizuri, iwe mingi, iwe mikubwa na tunawaambia watu wasiikate kwa sababu kukata misitu, kukata miti ni hatari yetu ukame unaweza kuingia. Kwa hivyo, hali hii Mhe. Spika, naona kwamba inasaidia miti hata kupunguza mmong'onyoko.

Mhe. Spika, hali ambayo inajitokeza nyengine niseme kwamba watu wetu wana tabia ya kukata mikoko sehemu za pwani; tabia ambayo iliyokuwa si nzuri. Tabia hii bora watu waiwache sio tabia nzuri kwa sababu wao wanahisi ni kukata miti kwa faida yao lakini ile miti iliyokuwa pale pwani ina faida zake kuwepo. Ile miti iliyoko pale inasaidia kwanza maji kuja juu kwa nguvu, inazuia kidogo kwa sababu ina mizizi mingi. Pili ni maeneo ambayo ni mazalio ya samaki. Kwa sababu miti wakiikata ina maana maji yatasogea kwenye ardhi, yakija kwenye ardhi mabonde ya mpunga yote yanaharibika. Hii ni kwa sababu ya miti kukatwa pwani.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri katika suala hili ajitahidi sana na wananchi kuona kwamba miti maeneo ya pwani pwani haikatwi ovyo ovyo kwa sababu ni mazalio na yanasaidia katika maji kuingia ardhi kavu.

Mhe. Spika, jengine ambalo la mwisho nataka nizungumzie juu ya suala la Matangatuani. Mhe. Spika, naona hiki kilimo cha Matangatuani ilikuwa inaitwa Matangatuani *Agricultural Station* halafu ikaitwa ni Matangatuani ni eneo la…

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe nasikitika kwamba nilikuwa na shughuli kidogo hapa na muda wako kimsingi ulikwisha malizia kwa dakika mbili.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Haya namalizia Mhe. Spika, hii ya *Matangatuani Agricultural Station*. Kwa kweli Matangatuani ni mahala muhimu sana kwa kuwasaidia watu Kaskazini kwa habari ya kilimo. Kule ni mahala ambapo ni kituo cha watu kufanyiwa utafiti na watu wanakwenda kwa kutaka kuona mambo ambayo yanajitokeza pale. Mashamba yetu yanahujumiwa na wadudu, matunda yetu yanakuwa sio mazuri sana na mihogo yetu vile vile inahujumiwa na wadudu. Sasa kwa miaka mingi kituo hiki cha utafiti naona kimelala, na hapa tumeambiwa kitahuwishwa, kitafanyiwa ukarabati wa majumba, mimi sijui kama ukarabati huu wa majumba ndio itasaidia utafiti huu.

Mhe. Spika, wao walisema hivi wafanye ukarabati wa majumba sisi tunataka kazi ziwepo, majengo wanayo tunataka ile kama *laboratory* yao iko nzuri yakuweza kufanya utafiti, wataalamu wapo watufanyie utafiti juu ya haya magonjwa, hicho ndio kitu tunachokitaka na Matangatuani ile lazima iwepo kwa sababu ile inasaidia kwa Kaskazini nzima…

Mhe. Spika: Haya nakushukuru sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Sisi watu wa Kaskazini tukiwa na matatizo twende pale Matangatuani. Kwa hivyo, ningelimuomba Mhe. Waziri hili…

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mheshimiwa…

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Hiki kituo cha Matangatuani akihuwishe, akiweke vizuri ili watu wa Kaskazini wafaidike. Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa muda huu na mimi nichangie. Ahsante sana naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutupa pumzi tukawa nazo hadi sasa. Nichukue nafasi hii vile vile kukushukuru Mhe. Spika, kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, matumaini yetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kuisaidia serikali na kusaidia bajeti hizi zilizokuwa zinawasilishwa mbele yetu. Labda niseme tu Mhe. Spika, kwamba hiki kikao kinachoendelea ambapo wananchi wengi ndio wenye matumaini ya kazi ambayo tuliyopewa kuifanya sisi kwa niaba yao wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, mategemeo yao makubwa katika haya yamo ndani ya Baraza la Wawakilishi katika utekelezaji mzima wa bajeti hizi tunazoendelea nazo, na leo tumefikia bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kama ninavyosema kwamba tumo humu kwa maslahi ya wananchi na nikisema nirejee tena kwamba tumo humu si kama skuli kwa mwanafunzi kwenda kuandika mtihani akapasi au kufeli, kwa hivyo naamini kwamba humu hatuko skuli Mhe. Spika bali tuko katika kutekeleza majukumu ambayo tumepewa. Sasa Mhe. Spika, mimi niendelee kuiunga mkono na kuipongeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kazi nzuri na utekelezaji mzuri ambao wanaofanya na jitihada kwa kupitia waziri na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, niombe tu kwamba mimi niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa hasa kwa Wizara ya Kilimo naamini serikali ina-*subsidies* mambo mengi sana katika Wizara ya Kilimo kwa kuwapelekea wananchi vitu ambavyo viweze kusaidia, na kilimo ndio uti wa mgongo katika ulimwengu mzima sio Zanzibar tu ni katika kila sehemu; bila ya kilimo kusimamiwa basi tunaweza kuingia katika njaa.

Mhe. Spika, nilikuwa nakipitia kitabu hiki malengo ya idara ya mwaka 2014/2015 ukurasa wa 13. Mhe. Spika, malengo haya ni mazuri kubwa zaidi ni utekelezaji wake na tumeona hapa kutokana na hali ya serikali yetu na bajeti yetu na madeni ya wakulima ambao wanaidai serikali. Niseme kweli Mhe. Spika kwa wakulima mimi nimefurahi sana na leo wameeleza wenzangu Wizara ya Kilimo malengo ya idara kwamba ukitaka kumuondeshea mkulima umasikini ni kumuwekea miundombinu kama vile barabara za vijijini. Hilo Mhe. Spika, ni jambo moja ambalo litaondosha umasikini kwa sababu Zanzibar tabia zetu hatuna tabia ya kuombaomba, sasa kama serikali itachukua juhudi na hasa hii Wizara ya Kilimo na mipango yake, mimi nina imani kwamba hapa tutaweza kuwapunguzia umasikini wakulima.

Mhe. Spika, kwa sababu mkulima anaweza kuwa na shamba lake zuri, anaweza kuwa na mazao mazuri lakini miundombinu ya kuziondosha sehemu ile ili kufikisha katika sehemu yakuchukuliwa mizigo ile na kupelekwa marikiti basi ile sehemu inamfanya yeye arudi nyuma miaka kwa miaka, kutokana na mazingira ya miundombinu ilivyo.

Watu kama sisi wafanyabiashara tuliokuwa na magari tunachukua *advantage* yakumfanya yule mkulima anamwambia bwana miundombinu yako ni mibovu, gari ambayo ilikuwa inapaswa kutoa shilingi 2000 anatoa shilingi 10,000/= hana la kufanya, ilimradi yeye aondoshe mazao yake hapo. Kwa hivyo, anapofika sehemu ya marikiti mkulima yule matokeo yake hafaidiki kama anavyofaidika yule anayenunua kwa jumla mazao yake. Kwa hivyo, mimi ninaona Mhe. Spika, niiombe wizara hii kwa nia yao nzuri na shabaha yao nzuri kubwa zaidi ni suala la miundombinu ya barabara za vijijini; kuanzia Jimbo la Uzini naamini majimbo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, bajeti vile vile tumesomewa hapa kwa wakulima ambao naamini Wizara ya Kilimo ilikuwa na nia nzuri pamoja na serikali yetu na wizara hii ilitumia jitihada kubwa katika kupunguza hili deni kutoka milioni 240,000,000 mpaka kufikia milioni 106,000,000. Sasa mimi ningeliomba Wizara ya Fedha ikawasaidia hawa wakulima na hasa katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ili madeni haya yaweze kupungua na ikawasaidia katika maisha yao.

Mhe. Spika, suala la Ramadhani ni jambo kubwa sana kwa sisi Zanzibar hasa hivi tulivyo na asili yetu, kwa hivyo mimi ningeliomba tu Wizara ya Fedha katika hili waweze kuwaondoshea usumbufu wakulima hawa kwa kuwalipa hizi pesa zao
Kwa hivyo, nilikuwa naiomba Wizara ya Fedha na ripoti ilisema kwamba na wao Wizara ya Kilimo walikuwa wameshaipeleka Wizara ya Fedha kusaidia kuondosha deni hili na naamini vitu hivi vinafanyika kwa kuwasaidia wakulima na watu wengine kwa jumla.

Mhe. Spika, katika ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati na mimi amenigusa katika Jimbo langu la Uzini naomba ninukuu, "wakati Wajumbe wa Kamati walipotembelea Bambi walishangazwa kuona kuwa kituo hiki kinakabiliwa na usumbufu wa bomba ya kumwagilia dawa za mimea ambazo gharama yake ni ndogo. Hata hivyo, kamati imeiomba wizara itoe kipaumbele ya matumizi endapo itaingiziwa pesa hizi kwa manunuzi ya vianzio muhimu vya bei rahisi ili kuondoa usumbufu katika hili".

Mhe. Spika, mimi nimefarajika sana na ripoti hizi, zimekuwa za wazi na niko tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa jimbo langu la Uzini katika kuwasaidia wananchi, ili tuone vipi tunasaidiana.

Mhe. Spika, serikali ndio sisi, serikali ishafanya mengi sasa mimi kama Mwakilishi nimechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Uzini basi niko tayari kuona suala hili kwa upande wa Bambi vifaa na changamoto zilizopo, ili kuona jinsi gani tunaweza kuwaondoshea wananchi changamoto hizo. Kwa hiyo.

Mhe. Spika, namshuru Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake hata nikienda saa mbili ana kikao ndani au saa tatu ninachotaka kusema ananipokea na kwamba ni mtu mkweli, ni mtu ambae hapendi kutafuna maneno na ni mtu ambae anasimamia jambo na kukwambia hasa kwamba hili naliweza, hili siliwezi. Kwa hivyo, mimi naamini watendaji kama hawa tungelikuwanao. Hata kama kukiwa na wageni nikimwambia sekretari wake mwambie Ndugu, Mohamedraza Hassanali amefika basi hazichukui hata dakika kumi ananiita. Nikiingia namwambia kuna moja, mbili, tatu jimbo langu la Uzini, ataniambia hili ninaliweza tulizana, hili fanya hivi.

Kwa hivyo, mimi nina mashirikiano mazuri na wizara hii na nitazidi kutoa mashirikiano katika wizara hii na hasa ukitizama ukurasa wa sita, Mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili mwaka 2014/2015. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea kusimamia, kutekeleza malengo ya dira ya 2020 na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi CCM, kwa mwaka 2010 na 2015.

Mhe. Spika, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini MKUZA kwa mipango na mikakati ya sekta pamoja na mpango; haya ndio yaliyotuleta na ndio tunayoyasimamia. Hiyo bajeti iliyosomwa ndio iliyotuleta na tukafika hapa. Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri vitu ambavyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huku *back bencher* nataka kusema kwamba hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Umoja wa Kitaifa hakuna upinzani, tumekuja hapa kuisaidia serikali.

Kwa hivyo, ninachomuomba Mhe. Waziri kwa heshima na taadhima kwa wajumbe wanaokuja kama kuna eneo hakuliona au hakufika ningelimuomba sana Mzee wangu, baba yangu, asizungumze kitu ambacho hajakiona, ikawa kitu anachokisema sicho na hiyo ndio inayotufikisha hapa, tukawa na matatizo makubwa katika Baraza hili.

Baadhi ya mawaziri hawafiki kwenye eneo, hawajapatapo kwenda toka umri wao hawaijui hata ile njia, unapokuja kumuuliza anafika pahala anazungumza jambo ambalo linatuletea vurugu katika sehemu yetu hii.

Mhe. Spika, ningeliwaomba wenzetu Mawaziri waliobakia ama waseme tupeni muda au waseme tutajibu, kuliko kuja kufyatua mambo ni sawa sawa na mtoto, mwanafunzi aliyeko darasani anapewa mtihani anaandika ndicho, sicho basi. Lakini humu hatuko skuli. Kwa hivyo, mimi ningeliomba tuwe na mashirikiano mazuri katika kutekeleza hii dira ambayo wizara imejiwekea.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naiunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini kwa asilimia zaidi ya mia moja Wizara ya Kilimo na Maliasili, na naiombea tuweze kufanikisha mambo yetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii nikatoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Lakini kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoka huko nilikotoka mpaka kufika hapa na nikaweza kusimama hapa.

Mhe. Spika, kwanza nataka niipongeze sana wizara hii, lakini kwanza nataka niwapongeze kwa hivi vitabu vyao. Vitabu wanavyotuletea vyote mara hii ni unga vinamung'unyuka ambapo tuna vitabu vya tangu mwaka 2011/2012 havijatoka hata ukurasa mmoja, sasa sijui mara hii tatizo ni nini.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu na mimi niseme naiunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Bila ya kuiunga mkono tutakuwa hatuoneshi taswira nzuri kwa sababu wengi ni wadau katika taasisi hii ya kilimo.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu niende katika ukurasa wa 5 unaelezea kilimo cha maweni. Kilimo hiki kimezungumzwa siku nyingi sana lakini husubiri hatma ya matokeo yake na tafiti hizo ambazo zinahitajika kufanywa katika sekta hii. Katika ukanda huu wa kilimo cha maweni bado unaendelea kuwa ni hadithi katika vitabu hivi na wala hatuoni mafanikio ambayo tumeyapata. Kwanza wizara juu ya changamoto yao waliyonayo ya ukosefu wa fedha wanazoingiziwa kutoka serikalini, kweli fedha ni kidogo, lakini na mipango yao sio mizuri pia na wataalamu hawana.

Sasa ikiwa mipango si mizuri na wataalamu hawana kwa sababu kila mbuzi anatakiwa ale kwa mujibu wa kamba yake. Sasa wewe leo kama unachogaiwa ni kidogo lakini una mipango mingi, utafika pahala? Utakwama,

hufanikishi hata mmoja. Sasa ningeiomba wizara na ufinyu wao wa bajeti basi waeleze mambo ambayo wana uwezo wa kuyakamilisha.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki 2011/2012 cha mwanzo pana Mhe. Rais hapa na Makamanda mbali mbali wanavuna mpunga, kimeandikwa kuwa; "Tumeamua, tumeanza na tutaweza". Kitabu hiki ambacho humu ndani katika suala hilo hilo la kilimo cha maweni kimeelezewa kitabu hiki kuwa, "Kwa kulitambua suala hilo wizara yangu imejipanga kuwaendeleza wakulima wa maweni na kuwapatia utaalamu kupitia skuli za wakulima, na itaendelea kushajihisha matumizi endelevu ya rasilimali za ardhi, maji katika kuendeleza kilimo hiki bila ya kuathiri mazingira ya rasilimali zilizopo".

Sasa kama hili suala lilikuwa limetiliwa nia na tangu siku hizo mwaka 2011/2012 kitabu hiki kishazungumza na vitabu hivi japo kuwa waziri aliyekuwa akihusika na kitabu hiki hayupo, lakini hii yote ni mipango ya wizara si mipango ya mtu. Kama kweli kulikuwa kuna nia ya kufanya utafiti na mimi siku moja kwenye Kamati ya Kilimo nililizungumza suala hili; kuwa hawa watu wanaolima katika maeneo ya maweni huwa wanawafikiriwa nini katika mpango huu wa Mapinduzi ya Kilimo? Au wao hawana haki katika nchi hii?

Naona ardhi ile inakubali vitu vingi lakini kwa kweli Wizara ya Kilimo na Maliasili bado katika wakulima hawa wanaolima maweni hawatutendei haki kiasi fulani. Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri kama lengo lao ni hilo kwa sababu ndani ya kitabu chao na wao limo, basi wafanye *ilihali* na wao wale wenzetu kule waweze kufaidika na haya Mapinduzi ya Kilimo.

Suala jengine ukurasa wa 6 naomba Mhe. Waziri akija hapa anieleze katika kifungu cha 17, kaeleza kuhusu takwimu za mikarafuu waliyoifanya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Sasa mimi nataka aje anieleze katika takwimu hiyo wanayoifanya ya miche yao wanayoiuza kwa wanunuzi wa ile mikarafuu je, wanafanya takwimu za mikarafuu wanayokuja kuikuta ambayo ni ya kurithiwa? Kwa sababu kazi kubwa inafanywa ya uatikaji wa miche na wizara hii na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko hutoa mwelekeo wao wa upandaji wa miche watu wakapewa bura. Sasa tathmini hii wanaifanya katika hali gani? Wanaifanya katika mikarafuu ile ya zamani iliyokuwepo au katika mikarafuu hii inayouzwa, ndio wakafufua takwimu hiyo waliyoieleza katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, jengine nije katika Idara ya Umwagiliaji Maji lakini katika idara hii nataka nijikite moja kwa moja katika mabonde mawili; bonde moja la Saninga na jengine la Kinyakuzi. Kama dhamira ya Mhe. Rais alivyotoa hotuba yake katika Baraza hili kuwa moja kati ya uendelezaji wa kilimo hasa katika kilimo cha umwagiliaji maji; tutaendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji na kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua ili yatumike katika kuzalisha mazao mengi ya chakula na mboga mboga kwa njia ya umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, mabonde haya ninayoyataja ni mabonde ya zamani sana ambayo yana wakulima. Miongoni mwa mabonde hayo ni kama bonde la Saninga; lina hekta 16 lakini lina wakulima 160 na asilimia kubwa ni wanawake. Lakini ukienda bonde la Kinyakuzi lina hekta 7 lakini lina wakulima 80. Ukiangalia hapa hii ni sehemu moja wapo inayozalisha ajira, sasa laiti ingelikuwa mabonde yale yanashughulikiwa kwa miundombinu mizuri, basi watu hawa wangefaidika na mabonde haya ya umwagiliaji maji na ndio kilimo ambacho serikali inataka watu wajikite kwa kilimo hiki cha umwagiliaji maji. Lakini mabonde haya wakulima wanayakimbia kutokana na miundombinu yake iliyopo hairidhishi hata kidogo. Watu wana hiari kwenda kupanda mwani kuliko kuendelea na kazi hii.

Pia mabonde haya tulitegema kuwa tulime ndani ya misimu miwili; msimu wa mwaka na wa vuli ndio lengo la umwagiliaji maji. Lakini leo hakulimiki hata msimu mmoja. Kwanza vile kuzijenga zile *plot* ina maana tayari wewe mabonde ukishayajengea vile uyawekee ile miundombinu ya umwagiliaji maji, lakini sasa kama watu ushawajengea vile miundombinu iliyoko pale ni mibovu ina maana ushawazidishia adha katika maji ya mvua inayonyesha pale.

Mhe. Spika, kwanza nikianza na hilo bonde la Saninga. Bonde hili bwawa lake ni bovu halikidhi haja na siku zote tunaambiwa kwenye vitabu vya bajeti ukarabati wa mabwawa, lakini bwawa lile halifai. Halafu bonde hilo hilo la Saninga halina mto wa kati ambapo linakosa hasa ile sifa ya umwagiliaji maji, kwa hiyo inakuwa ni adha. Maji yanayotoka juu ya milima yote yanaingia ndani ya bonde, sasa wakulima wategemee nini hapa na tunajinasibu kuwa tunaendeleza mabonde ya umwagiliaji maji kwa kuondoa umasikini na kufanya. Huo umasikini utaondoka? Kwa hiyo, bonde hilo halina mto wa kati namueleza Mhe. Waziri anisikilize vizuri.

La tatu, *blade grain* yake ya miundombinu hiyo haifai ambapo *blade grain* ni msingi ambao unatakiwa uzuwie maji yanayotoka juu yasiingie kwenye mabonde, lakini maji yote yanayotoka juu yanaingia kwenye mabonde hatimae kinachowekwa pale hakina tija.

Mhe. Spika, kwa kweli wizara miradi hiyo hiyo midogo midogo inayopatikana, lakini hata hiyo miradi hiyo haifai, ndio nikasema kwa sababu hawana wale wataalamu.

Hivi karibuni kulikuwa na mradi mmoja wa *GP5;* mradi huu uligharimika pale ukajengwa msingi ambao unazuwia hayo maji kwa saruji lakini msingi ule umefeli; haufanyi kazi, msingi ule sasa hivi uliomo ni mchanga mtupu, ina maana kadhia ni ile ile maji yakiingia ndani ya bonde hayatoki wala hayana yanapokwenda, yanasambaratika ndani ya bonde lile.

Mradi mwengine uliofanywa vile vile ni mradi wa nafaka ambao karibuni mabonde 40 yalitakiwa kufanyiwa mradi huu. Kwa Wilaya ya Micheweni na sisi pia tulibahatika, ambapo Saninga ilikuwa ni eneo moja lililopelekwa huu mradi wa *Demo plot,* lakini pia umefeli kutokana na miundombinu tu iliyopo pale kwenye bonde. Sasa kama ni bonde la umwagiliaji maji hebu lifanywe kuwa ni la umwagiliaji maji na kama serikali haina uwezo basi iwaruhusu watu, yale matuta yachawanywe yaachiwe maji yaende yanakotaka.

Kitu cha msingi tukumbuke hasara iliyopita pale kwa sababu palichimbwa kisima hazipungui shilingi milioni mia moja, lakini kisima leo hakitumiki. Kipo kisima cha umwagiliaji maji; pesa nyingi zilikwenda lakini ukitizama miundombinu inayojengwa pale haifai na pia mradi huo umefeli kwa kusababisha kutoka maji kwenye bwawa na kuvamia zile shamba zilizopo pale. Sasa sijui kama lengo letu ni kupata wale wasaidizi lakini tukafanya jambo ambalo halina manufaa kwa serikali wala kwa wale wakulima!

Mhe. Spika, na bonde la Kinyakuzi ni hivyo hivyo. Hilo bwawa lilioko sasa hivi lishachimbika shimo, maji yakiingia pale yote yanasambaratika na pale pia napo hapana tija, wakulima hawana kulima, hawana chochote wanachofanya.

Mhe. Spika, la mwisho nataka kuzungumzia suala la mbolea. Mhe. Spika, eneo lote lile na mabonde hayo yote yaliyopo, basi watu waende Matangatuani na pesa zao kuchukua mbolea na hawana usafiri. Lakini kuna mbolea hii ya *TSP* ambayo ni ya utiliaji na siku nyingi imetoweka. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akija anieleze ni sababu zipi ambazo zimefanya mbolea hii haipatikani kwa muda huu.

Suala jengine dawa ambazo tuliambiwa kama kuna punguzo la bei; Mhe. Spika, dawa zile za kuulia wadudu bado lita moja inauzwa shilingi thalathini elfu na hiyo ndio bei ya tangu mwanzo haijapungua hata shilingi moja. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, tena naiomba sana Wizara kuendeleza mabonde haya. Kama tuna nia ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji, kwa kuandika vitabuni tu naona hatutafika. Kwa sababu tunafika pahala sisi ndio tunaolima humu mabondeni lakini mnatushinda kutokana na hali ilivyo. Sasa kama tunataka kweli kufanya hayo mapinduzi ya kilimo, tusiwe na uandikaji wa humu vitabuni tu. Kwa kuwa bonde la umwagiliaji maji, huku mnatafuta mabonde mengine mkianzisha miundombinu mingine, haya huku hayafai tutakuwa hatufiki pahala.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba Mhe. Waziri akija anipe ufafanuzi kwanza wa haya mabonde, lengo lao ni nini. Kama ni kuendeleza kuwa ni ya umwagiliaji maji au ni kuwaruhusu wananchi mabonde yakatawanywa yale matuta yaliyomo yakaachiwa maji yakachukua mkondo wake. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ingawa mchango wangu mimi utakuwa mdogo sana lakini naomba nichangie kwa sababu nina ujumbe kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nataka nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa bajeti hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri ameonesha kama ana uwezo mkubwa. Nadhani hata hili nitakalolichangia halitakuwa kubwa kwake.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze na ujumbe ambao wamenipa wananchi wa Jumuiya ya Uzalishaji wa Chumvi ambao Makao Makuu yao ni mita chache tu kutoka nyumba yangu ninayoishi, Wawi.

Mhe. Spika, Jumuiya ya Uzalishaji wa Chumvi Pemba wana malalamiko na Serikali yao, na wamejenga taswira kwamba Serikali ina upendeleo kwa Unguja na Pemba. Mhe. Spika, hata mimi hili nalikubali. Kwa sababu chumvi nyingi inazalishwa Pemba kuliko Unguja labda ndio Serikali ipo mbali nao na hawaoni jitihada hizi.

Mhe. Spika, Pemba kuna mabwawa ya kuzalisha chumvi zaidi ya 60 yakiwa kwenye Shehia ya Chambani, Pujini, Kiwani, Shengejuu, Kiungoni, Wingwi, Sinzini, Ukunjwi, pamoja na Kangagani ambapo maelfu ya wananchi wamejiajiri. Mhe. Spika, siku zote tunalalamika humu kama ajira ni kidogo, lakini eneo hili wananchi wengi wamejiajiri. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze mashamba haya yanazalisha tani ngapi kwa mwaka.

Mhe. Spika, pia kila shamba linalipia shilingi 25,000/= kwa Idara ya Misitu. Sasa namuomba Mhe. Waziri anieleze fedha hizo ni za nini. Ni jambo la kusikitisha sana kuona Serikali inachukua kodi hiyo kutoka kwa wananchi wanyonge, maskini sana lakini hakuna huduma yoyote wanayofanyiwa. Baya zaidi pale kwenye kiwanda chao panahitaji mtambo wa kukaushia ile chumvi ili ipate kusagwa, lakini wazalishaji hawa wa chumvi wametupwa na hawaulizwi.

Mhe. Spika, jambo jengine baya sana Serikali inavyoonesha kutokuwajali wazalishaji hawa wa chumvi ni kwamba wamezalisha magunia yamo ndani. Serikali imeshindwa kuwatafutia soko na baadae inaruhusu chumvi kutoka Kenya inauzwa nchini kwetu. Mhe. Spika, kwa kweli huu ni uadui. Ukenda kwa hawa wazalishaji wa chumvi kipolo kinauzwa shilingi 5,000/=, kwa kweli inasikitisha. Kazi kubwa wanayoifanya lakini Serikali bado haijaona jitihada ya watu hawa. Mhe. Spika, mimi bajeti hii siiungi mkono.

Mhe. Spika, nakubali kwamba uzalishaji huu wa chumvi mkubwa ungelikuwepo hapa Unguja basi Serikali tayari ingekuwa imeshaingiza nguvu zake. Naomba Mhe. Waziri anieleze ni kitengo gani ndani ya wizara yake ndio wenye mamlaka ya kusaidia uzalishaji wa chumvi, na elimu imetolewa lini na lini. Pia elimu hiyo imewasaidia vipi wazalishaji wa chumvi katika uzalishaji wao.

Mhe. Spika, mimi nisipopata maelezo mazuri nitazuia fungu la Idara ya Mipango na Sera. Kwa sababu inaonesha sera zinazofuatwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili hazimuendelezi mwananchi.

Mhe. Spika, sasa nataka niende kidogo kwenye kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Spika, kilimo cha umwagiliaji maji ndio mkombozi kwa mwananchi mnyonge. Kwa kweli ikiwa Serikali imedhamiria tujitosheleze kwa chakula basi ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Spika, mimi kila nikichangia Wizara ya Kilimo na Maliasili hili nitalisema. Kwa sababu nina kumbukumbu mwaka 1980-1982 nikiwa na umri wa miaka 8 katika mabonde ya Kwapweza kulikuwa kukizalishwa mpunga mwingi sana, na walikuwa na miundombinu hii ya umwagiliaji maji. Lakini hivi sasa la kusikitisha Mhe. Spika, wananchi wanalima wanachokipata siku nyengine ni ile mbegu. Sasa namuomba Mhe. Waziri atueleze atakaposimama hapa, ana mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa kule ambao wana maeneo makubwa ya kulima lakini miundombinu ya umwagiliaji maji haipo.

Mhe. Spika, pia katika bonde la Msaani ambalo tuna kikosi chetu cha JKU wanafanya kazi sana na wana eneo kubwa. Hapo nilipoingia mimi JKU walikuwa wakizalisha sana kwa sababu ilikuwa bado mvua angalau zikenda kwa msimu. Sasa hivi hakuna msimu wa mvua utakuta ni masika lakini jua kali. Namuomba Mhe. Waziri anieleze atawasaidia vipi watu wa Msaani ambapo kuna kikosi chetu cha JKU - Jeshi la Kujenga Uchumi kuwawekea hii miundombinu ya umwagiliaji maji.

Nadhani Mhe. Spika, ikiwa Serikali itajipanga lile ni jeshi ambalo tumeshasema ni la kujenga uchumi, kujenga uchumi wenyewe kwengine ni kuzalisha. Sasa leo eneo la kuzalisha lipo lakini hawawekewi ile miundombinu. Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha na wala sifikirii kama tutafika.

Pia Mhe. Spika, katika eneo la Cheju kuna *TASAF* Jendele. Wakulima hawa wana matatizo ya mtaro, kuna mtaro sehemu ndogo haikujengwa kwa saruji na kwa kweli maji mengi hupotea na baadhi ya wakulima hawapati maji, na hupelekea wakulima kupata uharibifu wa zao lao. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze ni lini atakwenda kuwaona wakulima hawa wa Cheju na kuwasaidia mtaro huo ili kuondoa usumbufu wanaoupata.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nataka nilizungumzie kidogo ni huduma ya pembejeo. Mhe. Spika, mbolea ndio kiini cha uzalishaji bora. Lakini jambo linalosikitisha eneo lenye uwezo wa kutumia kilo 10 za mbolea basi huwa mkulima anapewa kilo 4 au 5. Kweli Mhe. Spika, tupo *serious* na kuongeza uzalishaji. Kwa sababu mimi siamini

kama utachukua sufuria la maji unalotaka kupikia chai la kilo 10 ukatia kilo 4 ukasema umepika chai. Kwa hivyo, na hapa haiwezekani kuwa kilo 4 ziweze kufanya kazi kwenye eneo la kilo 10 uzalishaji utakuwa haupo.

Mhe. Spika, msimu uliopita wakulima walilalamika kwa hili. Namuomba Mhe. Waziri atueleze ni sababu ipi iliyopelekea wakulima kupewa mgao mdogo na wengine kukosa kabisa na baadae ikalazimika waende wakanunue mbolea nje kwa kilo shilingi 1,800/=. Namuomba Mhe. Waziri akija anipe sababu zilizofanya hivi.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu wizara kukopa mbegu. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atueleze ni sababu zipi zinazopelekea kuwakopa wananchi wanyonge ikisha deni hilo kuwalipa ikawa ni tabu. Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha ukifungua redio Mawio ni mbegu, hili si jambo zuri kwa Serikali.

Mhe. Spika, naomba niwapongeze sana Idara ya Misitu kwa kuweza kudhibiti ukataji wa miti lakini bado jitihada inahitajika zaidi. Mhe. Spika, ukataji wa miti bado unaendelea sana na naomba wizara ijipange kwa kweli hili ni janga kuachia miti kila siku inakatwa. Lakini pia naomba iwahamasishe na wanavijiji ikiwapa elimu labda watajua.

Mhe. Spika, mimi nitoe mfano mmoja; kule kwetu kuna kijiji kimoja cha Vikunguni kinaitwa Dutani, kuna kijiji kingine ni masafa lakini ilikuwa hapo nyuma ukipita katika njia hiyo unaogopa kwa msitu uliokuwepo. Bahati mbaya baadae palikatwa katwa mpaka mtu aliyekuwepo kijiji kingine basi utamuona wewe uliyekuwepo kijiji kingine na wakati ni masafa marefu. Lakini wale wanakijiji wenye eneo lile kwa kuujua umuhimu ule waliandika mabango wakasema kama atakayekata mti kwetu atapewa adhabu na wakaweka adhabu yao wenyewe si Serikali.

Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa ukenda utashangaa pahala pamebadilika. Msitu umeanza kurudi na pamependeza. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa hili naomba pia atoe elimu kwa sababu wakitoa elimu pengine watu wataelewa.

Mhe. Spika, ingawa kuna tatizo umeme ni ghali na wewe ndie Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, watu hawawezi kutumia umeme kutokana na ughali wake, wewe ndie mfua gesi. Mhe. Spika, nashukuru sana huyu waziri kuwa ndie anayekaimu wizara hii. Sasa bila shaka ataweza kunisaidia hili tatizo kuondoka. Kukatwa kwa misitu ni kusaidia wananchi wakaweza kutumia njia nyengine ya nishati. Kwa hivyo, umeme angalau bei iwe nafuu, gesi iweze kutumika, yakishaweza kutumika hayo misitu yetu itaimarika. Naomba Mhe. Waziri yote mawili ayatizame.

Pia Mhe. Spika, mara nyingi watu wa misitu huwa tunawakuta wamekamata mkaa ama kuni. Sasa naomba hapa Mhe. Waziri anifahamishe ule mkaa wanaokamata au kuni huwa wanagawana au huwa wanauuza, na wakishauuza hizi pesa zinakwenda wapi?

Mhe. Spika, kwa kumalizia mwaka jana katika hiki kitabu cha bajeti tulioneshwa hapa kuna lengo la kuimarisha maghala ya kuhifadhia chakula na tumeoneshwa kama lengo lile halikufikiwa kwa sababu hakukuingizwa pesa. Lakini pia mara hii limewekwa kuwa limo katika lengo hili, ingawa mara ile lilikuwa la mwanzo, mara hii lipo la mwisho. Sasa naomba Mhe. Waziri atueleze wana mpango gani juu ya hili, au hili lengo litabakia kwenye vitabu tu kama malengo mengine.

Mhe. Spika, tunatakiwa mtu akimbie mvua ndogo, asisubiri amesharoa ndio anakwenda kujificha. Sasa namuomba Mhe. Waziri akija atupe maelezo mazuri kuhusu haya maghala ya kuhifadhia chakula. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia bajeti jioni hii. Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Naibu Waziri na watendaji wake kwa utendaji wao na ufuatiliaji mzuri.

Mhe. Spika, kwa kweli kilimo ni uti wa mgongo. Kwa kuwa utoaji wa mbolea hauridhishi, kwa mfano bonde la hekta moja linatakiwa lipate kilo 50, leo hili bonde la hekta moja linapewa kilo 5. Je, hii kweli ni kilimo bora au uuaji wa kilimo?

Mhe. Spika, kilimo cha umwagiliaji maji *TASAF* Jendele kina tatizo la kisima; tatizo hilo ni la kisima kile hakijapatikana maji. Ningeiomba wizara iliangalie sana tatizo hili, labda tunafikiria kisima kile ni kifupi au pengine maji yapo mbali. Ningeiomba wizara ifuatane na *TASAF* kwa kulishughulikia suala hilo.

Mhe. Spika, kwa kuwa kilimo cha maweni ni kilimo ambacho hakijapiga hatua, kwa hivyo ningeiomba Serikali iwasaidie sana wakulima wa kilimo cha maweni. Kilimo hiki ni kilimo ambacho kina asilimia kubwa ya wananchi ambao wanakitumia sana.

Mhe. Spika, kwa kuwa mabwana shamba na mabibi shamba ndio muhimu sana katika maeneo yetu ya kilimo tunahitaji kutufikia katika maeneo hayo. Lakini la kusikitisha mabwanashamba hawa na mabibishamba hawa hatuwajui katika maeneo yetu kwa sababu hawatufikii kwenye maeneo yetu na muhimu mabwana shamba wale kutufikia katika mashamba, ma kutupa muongozo wa kilimo.

Mhe. Spika, kwa kuwa wakulima mkataba ni wanazalisha mbegu za mpunga katika mabonde mbali mbali ikiwemo bonde la Mtwango, la kusikitisha wakulima wale wanadai pesa zao shilingi milioni mia moja na sita. Ningeiomba wizara, iwafanyie kila jitihada wakulima wale wawarejeshee pesa zao. Wakulima wale ni wanyonge wanawasomesha watoto wao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali inashindwa kuwalipa pesa wakulima wale, ningewaomba wakulima na kuwashauri mbegu ile wanapoipata wasiwauzie tena serikali, wawauzie wananchi ili kupata mahitaji yao waendeshee maisha yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji maji migomba ni kilimo ambacho kina tija sana na kina maendeleo kwa wananchi. Ningeiomba serikali iwasaidie sana wananchi hawa ambao wanajishughulisha na kilimo hiki cha umwagiliaji maji migomba. Kilimo hiki kina gharama kubwa sana. Naiuliza serikali ni mashamba mangapi katika Wilaya ya Kusini wanajishughulisha na kilimo hiki cha migomba ambapo serikali imekwenda kuiangalia; kuwapa ushauri angalau ili kuwapa elimu ya ushauri kwa kilimo kile cha umwagiliaji migomba ambacho kina tija na maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuwa wizara hii ni wizara ambayo inashughulikia sana wananchi, ni wizara ambayo bajeti yake ni ndogo na finyu. Naiomba serikali iwasaidie kwa jicho la huruma wizara hii, kwa vile wizara hii haina Waziri, ningeiomba wizara hii bajeti yake ionekane. Ninasikitika sana kuwa bajeti yake ni finyu kutokana na kwamba ni yatima. Maana yake ina waziri lakini mimi ninasema haina waziri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba ya wizara hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Sasa tumsikilize Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataallah* kwa kutujaalia jioni hii tukaweza kukutana hapa. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe ambaye umenipatia nafasi na mimi niweze kusema machache kupitia hotuba ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Kaimu Waziri ambaye aliisoma bajeti hii kwa umakini na uhodari sana. Pia nimpongeze Naibu Waziri na watendaji wao wote wa wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Spika, mimi nianze na mchango wangu katika ukurasa wa 46 ambapo wizara imeelezea changamoto zake.

Mhe. Spika, nieleze kati ya changamoto hizo zilizoelezwa na wizara, changamoto moja ilisema ni mabadiliko ya hali ya hewa. Mhe. Spika, ni kweli hali ya hewa kwa sasa tunayokwenda nayo si ya kutegemea sana mvua. Kuna mabadiliko yanajitokeza katika miongo.

Mhe. Spika, kupitia hali hiyo, mimi niiombe sana wizara basi itekeleze ile ahadi yake ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji ambacho kilimo hiki kingeweza kuwapa wakulima tija, kwani wangeweza kupatiwa mbegu ndogo za kupanda. Basi wangeweza kuvuna mara tatu kwa mwaka. Mhe. Spika, hii ni ahadi ya serikali ambayo ililetwa wakati ilipoleta mswada wake unaohusu kilimo na hifadhi ya chakula.

Mhe. Spika, lakini pia serikali kupitia hali hii ya mabadiliko ya hali ya hewa, ingejipanga ikawapatia wakulima mbegu ambazo zinastahamili ukame ili wakulima hawa wakaweza kulima kilimo chengine ambacho kinaweza

kustahamili ukame na kikaweza kusaidia. Pia katika kupitia changamoto hiyo hiyo ya hali hewa ningeiomba sana wizara ingewapa taaluma wakulima wetu, kwa kuweza kuvuna yale maji ya mvua ambayo wangeweza kuyatumia na yangeweza kusaidia kutatua changamoto hiyo.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Mimi hapa nilitaka tu kwa kuwa huu pia ulikuwa ni mpango wa wizara na uliletwa kwa muda mrefu, nilitaka kujua katika haya maghala kuna maghala mangapi ya chakula, lakini pia tuna tani ngapi ambazo tumeweza kuzihifadhi ili kuweza kuwa na uhakika huo wa chakula.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nilieleze suala hili la mabibishamba na mabwanashamba ambalo wenzangu wamelieleza. Kila siku wizara inaeleza kwamba inaajiri mabibishamba na mabwanashamba. Lakini mimi ninataka kujua mabibishamba na mabwanashamba wanaripoti wapi, kwa Shehaau Madiwani. Wanaripoti wapi katika wilaya zetu. Kwa sababu mimi nilijua kuitwa bibishamba na bwanashamba, basi nilijua jina hilo wamepewa labda kwa sababu ya kuweza kuwatembelea wakulima ili waweza kujua changamoto wanazokumbana nazo wakat wa wakulima, lakini pia kuwapa ushauri wakulima wetu ili wakaweza kulima kilimo ambacho cha kitaalamu.

Mhe. Spika, changamoto nyengine ambayo wewe pia mumeieleza wizara ni upatikanaji wa pembejeo. Kwa kweli Mhe. Spika, upatikanaji wa pembejeo ni kidogo sana, hazikidhi kwa wakulima wetu lakini pia ugawaji wake sio mzuri. Wakulima wengi wanakosa kabisa. Maana bora kiwepo kidogo tugawane kidogo kidogo lakini kuliko kuwapo kingi tukaanza kukigombea. Mhe. Spika, niombe sana tuweze kuwapatia wakulima mbolea kwani mashamba yetu kwa sasa yamechoka, ndio tunayoyalima hayo kwa hayo, bila ya kuyasaidia basi mazao yatakuwa ni hafifu sana.

Mhe. Spika, mimi pia nilitaka kujua kilimo hiki cha matone ambacho munasema kuwa kuna ulimaji wa matone, sasa je, munamiminia maji? Mimi nilitaka kujua ni kiasi gani mumeweza kuwapatia elimu hii wakulima wetu, ili waweze kuitumia elimu hii na waweze kupata mafanikio katika ukulima wao.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 32 ambapo mumeelezea vitalu munavyootesha miche na kuanza kuwapatia wananchi. Mumeotesha miche kama miche ya misitu, matunda, mikarafuu lakini sikuona katika uoteshaji ule wa miche, ya minazi. Minazi kama munavyojua tushaikata sana. Zao la nazi limepungua kwa kiasi kikubwa, basi niiombe tu serikali katika uoteshaji wake miche basi na hii miche ya minazi ingeipa nayo kipaumbele ikaoteshwa, ili ikaweza kuwapatia wakulima wakaweza kuotesha minazi na tukaweza kuendelea kupata nazi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu, niiombe sana serikali kuwapatia wakulima dawa za kuuliwa wadudu. Mhe. Spika, wakulima hukata tamaa ya mazao yao yanapokumbwa na changamoto hii ya kuuliwa na wadudu. Hubakia na unyonge mkubwa lakini pia niiombe serikali kuwapatia wakulima hawa msaada wanapokumbana na changamoto kama hii ya mazao yao kuliwa na wadudu, basi serikali iweze kuwasaidia. Wakulima hawa wanapopatwa na kadhia hii huwa wanabaki na hali mbaya ya ukosefu wa chakula.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu niende katika kilimo cha mboga mboga. Mhe. Spika, kwa kweli kilimo hiki cha mboga mboga ni kilimo ambacho kinaleta tija kwa wakulima. Lakini pia niiombe serikali kwani siku hizi husikia kuna kilimo cha *green house* ambacho kilimo hiki kinaonekana sehemu ndogo inatoa tija kubwa kabisa.

Ningeiomba serikali ikafanya utafiti juu ya kilimo hiki na ikaweza kuwasaidia wakulima, ili wakulima wetu wakaweza kulima kilimo ambacho kinaleta tija badala ya kulima eneo kubwa lakini huvuna mazao kidogo.

Mhe. Spika, niende katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Chuo hiki kuna wanafunzi ambao wamesoma chuoni miaka mitatu mpaka minne iliyopita bado hawajaajiriwa. Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja basi aweze kunieleza vijana wetu hawa ni lini wataweza kuajiriwa, ili ile elimu tuliyowapatia iweze kutusaidia wakulima.

Mhe. Spika, mchango wangu mimi hautokuwa mrefu. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naona kuna muda ambao Mhe. Saleh Nassor Juma anaweza akautumia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipatia hizi dakika 15. Ninadhani kesho dakika 20 nitaweza kuchangia dakika zangu 5.

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja kwanza kwa kumshukuru Naibu Waziri kwa jinsi anavyofanyakazi kwa umakini katika hii wizara. Vile vile ninachukua fursa hii sitaki nimwite Waziri Kivuli lakini haonekani kama vile ni Waziri Kivuli, kama ana matatizo Mwenyezi Mungu amjaalie yamuondokee. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, sasa hivi niende moja kwa moja kwenye hoja. Mhe. Spika, kulikuwa na nadharia kuanzia mwaka 1964 hadi hivi sasa katika sekta ya kilimo, tumepata nadhria mbili kubwa. Hii nadharia ya mwanzo ilianzishwa katika miaka mara baada ya mapinduzi. Tukaambiwa siasa ni uti wa mgongo wa taifa letu, hii ndio nadharia ya kwanza.

Mhe. Spika, nadharia ya pili, tumeipata hivi juzi juzi tulipoingia sisi hapa wapya katika Baraza hili, tuliambiwa kwamba kuna mapinduzi ya kilimo. Kwa hivyo, kuna nadharia mbili kubwa. Ile siasa ni uti wa mgongo na hii ya mapinduzi ya kilimo. (*Makofi*)

Sasa hii nitaanza na hii ya uti wa mgongo. Mhe. Spika, kama kuna nadharia makini ambayo walikuwa wakiifanyia kazi viongozi wa enzi zile, basi ni ile ya nadharia ya uti wa mgongo. Kwa sababu ilikuwa inaendana na maneno yao. Mhe. Spika, katika miaka sabini kwa kweli kilimo kilikuwa ni uti mgongo wa taifa letu. Maana yake ili kilimo kiwe kizuri Mhe. Spika, na kishamiri katika nchi na kukidhi haja ya wadau wa nchi, basi yangehitaji mambo yafuatayo:-

1. Matayarisho ya ardhi; na
2. Kupanda mazao,kupalilia na hatimaye kuvuna.

Mhe. Spika, sasa mambo manne haya ni muhimu sana kuyasimamia hii sekta inayoshughulika na mambo ya kilimo. Sasa ninachokwambia katika miaka ya sabini na nne pale tulikuwa na Waziri Mzee Tawakali Khamis akisimamia hii wizara. Matrekta yalikuwa yakimtafuta mkulima Mhe. Spika, kipindi kile. Yale matrekta sio mkulima atafute matrekta ya mkulimia, matrekta katika kipindi cha Mzee Tawakali katika nchi hii ilikuwa yakimtafuta mkulima.

Mhe. Spika, kulikuwa na matrekta yale ya minyororo kipindi kile basi nikwambie ni ya Kichina matrekta yale, yakilala maporini kutafuta wakulima, sio mkulima ahangaike katika kipindi kile cha ukulima, uti wa mgongo.

Mhe. Spika, wakati trekta huku linakutafuta, mbolea imeshakwenda nyumbani kwa mkulima. Yaani tulikuwa tunaanza *trip super for trait* ile ya kulimia, ile mbolea ya chenga chenga. Unamaliza kulima unaweka *trip super for trait*, ndio unasia pale. Ukimaliza tu kipindi cha mvua mpunga kuota basi *sulphate of ammonium* inamsubiri mkulima. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mazao yaliyokuwa yakipatikana siku zile yalikuwa ni mengi na yakikidhi haja. Mipunga ilikuwa ikilala mabondeni kipindi kile sehemu za Umangani, Mkungupigi, Mfikiwa. Mipunga ilikuwa inalala porini kwa sababu serikali iliweka kipaumbele kilimo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba sasa juzi hapa wakati ule Mhe. Mansour Yussuf Himid ni Waziri mambo haya ya kilimo, alikuja kwa mbwembwe nyingi katika Baraza hiii hiii kutangaza mapinduzi ya kilimo. Nikasema ehe! Ama sasa tunataka kulimiwa. Akatutajia mbegu inayoitwa Nerika, akatwambia senti mita chache tu za Nerika unaweza ukavuna hapo magunia kadhaa za mpunga. Tukasema sasa umaskini mwisho Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, la kusikitisha ama kwa kweli maneno hayaambatani na vitendo. Mhe. Spika, tukaambiwa matrekta yatakuja sehemu za hapa Mzambaraumboko, sehemu za bonde hili la Javini tukakaa tunasubiri matrekta. Mhe. Spika, la kusikitisha matrekta yale mpaka mvua zilinyesha hayajafika, huku mvua zinanyesha sisi tunachimbua sasa. Matokeo yake ni njaa tupu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kimsingi tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno siku zote. Haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana wepesi, lakini ikishughulikiwa kwa maneno huchelewa kama sadaka. Kuna uhondo kunataka matendo na asiye matendo hula uvundo siku zote. Inasikitisha sana munakuja hapa na jopo la wataalamu pale; wataalamu wanatwambia... Nerika haikufika katika jimbo langu hivi karibuni mwaka jana walipewa kisagakisaga, mtu alie na heka nne anapewa kisaga cha Nerika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kisaga ni pishi. Kuna vipimo vya vikopo vikopo hivi, kuna pishi, nusu pishi ile inakuwa ndio kisaga. Yaani *one and half kilo* ya mbegu, unataka kusia vipi Mhe. Spika.

Sasa kwa kweli umaskini. Wataalamu wana maneno mengi hayawi *implemented*. Hebu wakamsikilize, hawapo tena, zile enzi za Tawakali Khamis akiwa Waziri pale walikuwa wakifanya vizuri wala hawana taaluma kubwa. Leo hapa kuna ....

Mhe. Spika: Mhe. Asha Abdu Haji ungesogea hivi kidogo asije akakugonga mheshimiwa. (*Kicheko*)

Mhe. Saleh Nassor Juma: Eeh! sogeza kiti hivi nisije nikakugonga.

Mhe. Spika, inasikitisha wakati Waziri wa Kilimo hapa hana taaluma ya kutosha enzi zile ilikuwa minazi ikitutosheleza sana na nyengine tukizifanya mbata. Zile nazi ilikuwa tunapikia hatuzishi na nyengine tunafanya mbata na baadae tunatayarisha mafuta.

Leo kilimo cha nazi Mhe. Spika, hasa hii *African Tall*, ile minazi asilia ya nchi hii imetoweka mmoja baada ya mwengine. Itafika hadi tufike ziro ikiwa hatukuwa makini. Sasa mimi ninasema kwamba kilimo tunakichezea. Haiwezekani bajeti ya kilimo wakati sisi hatuna viwanda, wakati sisi hapa hatuna biashara, wakati sisi hatuna mafuta, bajeti ya kilimo haifiki *15%* ya *total budget* ya nchi. *It's shame*!

Sasa mimi ninasema Mhe. Spika, katika hili basi lazima tujitahidi sana kupanua bajeti hii ya kilimo ili iende sambamba na matakwa ya nchi, kwa sababu sisi ni maskini ya Mungu hatuna mafuta, viwanda, tunategemea *lailla hailla llah Muhammad Rasulullwah* basi. Imarisheni kilimo kwa kupanua bajeti Mhe. Spika, Mhe. Kaimu Waziri jitahidi.

Mhe. Spika, niende kwenye kilimo cha maweni. Mimi ni mdau wa kilimo cha maweni. Mhe. Spika, katika ukurasa huu wa tano, ibara ya 1.14 pamezungumzwa sana na kitabu hiki kilimo cha maweni. Mpaka rafiki zangu au mdogo wangu pale Mhe. Haji Omar Kheir naye ni mdau, Mhe. Hija Hassan Hija mpaka Micheweni kule, tunategemea sana kilimo hiki cha maweni.

Kama kuna kitu ambacho ni tegemeo basi ni kilimo cha maweni. Inasikitisha hawa sijui hawa niwaite wataalamu wenu wa kilimo, mabwanashamba na mabibishamba. Mhe. Spika, kama kuna tatizo tunakumbana nalo sisi wakulima wa maweni ni mabibishamba na mabwanashamba. Inasikitisha sana, kwa sababu mawazo ya kitaalamu hayapatikani kule. Sisi tunafanya kitu kinachoitwa *mono culture*. Unalipanda zao hilo hilo tangu miaka zaidi ya ishirini, wewe ardhi ile ni mpunga na mpunga na wewe, hukuvuna hata ile *shift cultivation*. Mimi ninajua, ni mtaalamu katika masuala haya, nina taaluma ya kilimo lakini kuna wengine hawafahamu.

Kuna mambo kama *crop rotation*, hayahitaji hata gharama, unakwenda tu kumuelimisha mtu. Kuna kitu kinaitwa *crop rotation*, unapanda mazao tofauti kwa misimu tofauti kwa sababu mazao tofauti yana mahitaji tofauti katika ardhi. Kwa vile ukiupanda leo mtama katika ardhi hii, keshokutwa ukija kuupanda mpunga, mpunga utanawiri vile vile. Ukija kutia kunde zitanawiri vile vile. Mtu huyo anapanda mtama ardhi hiyo miaka nenda miaka rudi, atapata wapi mazao wakati ardhi imeshiba na zao lile.

Sasa mimi ninaomba sana maafisa hawa wataalamu ikiwa Mhe. Haroun Ali Suleiman ana taabu ya kukuajiria utuambie humu, sisi tutaweza kujua vya kufanya, ili akuajirie hawa maafisa wataalamu. Inasikitisha sana watu wanachoma moto, watu wanalima kwa kuchoma moto misitu. Mazao hayapatikani badala yake wanafanya *environmental degradation*, jambo ambalo ni tatizo mno kwa sababu ya *pure methods of cultivation.*

Sasa Mhe. Spika, katika hili naomba niende moja kwa moja kwamba katika hazina hizi za misitu na nyuki. Kama kuna kitu muhimu dakika zangu zinakwenda haraka haraka, ni kulinda misitu yetu. Leo inasikitisha sana watu hawana taaluma ya misitu au umuhimu wa misitu hawajui katika kipindi hiki ambacho tuna *global warming* sasa hivi. Ni tatizo Mhe. Spika. Kwanza ujue kama kuna ongezeko la hewa ukaa kwa kiasi kikubwa. Sasa kitaalamu unapoimarisha misitu, misitu inafyonza hewa ukaa, yaani *carbondioxide* na hizi *process of photosynthsis*, ikichanganyika na maji *carbondioxide* unapata kitu kinaitwa *synthesis* na *oxygen gas* inatoka. Inatoka *oxygen* ambapo ukiivuta *oxygen* hiyo wewe inakusaidia kwa sababu ni hewa safi unaunguzia chakula, unanawiri.

Sasa misitu sio kwa kuvuta mvua tu, sio kwa kuimarisha ardhi tu lakini hata kwa afya zetu ni nzuri. Sasa watu hawajui, sehemu za Bogoa kule, sehemu za Nanguji kule, Kiwani kwa Katibu wao na Bubu, hawajui, wanataka taaluma ya umuhimu wa misitu na nyuki.

Sasa namuomba sana Mhe. Waziri, mwambie Katibu Mkuu wako, jamaa kutoka Kukuu Kangani kule sehemu za Bogoa wanataka taaluma wapelekwe watu nao wapande misitu.

Sasa Mhe. Spika, niendelee na haya mambo ya nyuki. Nyuki ni raslimali kubwa. Asali ni raslimali kubwa. Mimi katika kijiji changu wamejitokeza watu wanajihusisha na mambo ya asali. Haya mambo ya asali Mhe. Spika kufuga, kwa mfano kuna kijana anaitwa Khamis Suleiman Ali, kuna kijana mmoja anaitwa Saleh Ame wanazalisha asali lakini hawatembelewi wakenda wakapewa ushauri wa kitaalamu. Wanafuga nyuki nzuri tu pale Vitongoji Umangani, kule Kibokoni na akinamama wana vikundi vya kufuga nyuki Mhe. Waziri huyo hapo ni shahidi, kavitembelea, vya mambo ya samaki na mambo mengine kule. Lakini Waziri wa Kilimo hajaenda. Naomba muende. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie katika hili kwamba sisi wakulima tuna matatizo ya mazao. Ninapenda nimpongeze Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej, tena mutashangaa ninampongeza kwa nini na yeye yupo katika Wizara ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Ninampongeza kwa sababu kamudu kuwauwa kunguru weusi lakini sisi tunashindwa kumdhibiti *cassava min bud*.

Muda unamalizika mheshimiwa. Ninamaliza

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma tunakushukuru sana kwa mchango wako huo. Waheshimiwa Wajumbe ninawashukuru wote. Naomba Waheshimiwa Wajumbe niwakumbushe tu kwamba kesho kama tulivyokubaliana kipindi cha mchana pale kabla ya kuondoka kwamba kesho tutaendelea na shughuli zetu kama kawaida. Ila tu tuelewe kwamba shughuli zetu zitakwenda kwa mfufulizo na tukenda vyema itakuwa tunaondoka mapema zaidi.

Kimsingi jioni hatutokuja ila shughuli yetu hii Mwenyezi Mungu akijaalia tunaimaliza kesho. Kwa hivyo, niendelee kuwahimiza Waheshimiwa Wajumbe juu ya mahudhurio, mahudhurio yetu yanakuwa ni mabaya sana. Wakati mwengine tunaingia ndani humu hata Wajumbe kumi hawatimii kati ya Wajumbe thamanini na mbili pamoja na mimi, kunakuwa na Wajumbe kumi au kumi na moja.

Tukiifanya asilimia ingekuwa ndio fedha inayotolewa na serikali tungepiga makelele kweli kweli. Kwa hivyo ninadhani tupige makelele vile vile kwa kuwa na asilimia ndogo sana ya mahudhurio humu ndani, ili tuweze kuleta ufanisi mzuri basi mahudhurio pia yawe mazuri.

Nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe tutekeleze wajibu wetu kwa kufika mapema na kwenda na shughulki zetu kama kawaida. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe ninawashukuru na sasa naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 21/06/2014, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1:40 Usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 21/06/2014 saa 3:00 asubuhi)